ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kwanza - Tarehe 21 Septemba, 2016

(Kikao Kilianza Saa. 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) Alisoma Dua

WIMBO WA TAIFA

(Hapa wimbo wa Taifa uliimbwa kuashiria kufunguliwa kwa Mkutano)

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue fursa hii kuwakaribisha sana katika mkutano wetu huu wa tatu wa Baraza letu la Tisa ambao unaanza leo tarehe 21/09/2016.

Waheshimiwa Wajumbe, kama mtakavyokumbuka kwamba katika mwezi uliopita, kulitokea kifo cha aliyekuwa Rais wa Zanzibar wa Awamu ya Pili Mzee wetu na mwanasiasa mkongwe nchini ambae pia ni miongoni mwa waasisi wa Taifa letu, Mzee Aboud Jumbe Mwinyi. Kwa hivyo, taarifa ya Spika ya leo kwenu Waheshimiwa Wajumbe, pamoja na mambo mengine, itakua juu ya kifo cha Mzee wetu Aboud Jumbe Mwinyi.

Waheshimiwa Wajumbe, Mzee Aboud Jumbe Mwinyi alifariki siku ya Jumapili ya Tarehe 14/08/2016 baada ya kuugua kwa muda mrefu huko nyumbani kwake Mji Mwema, Kigamboni Tanzania Bara. Maziko yake yalifanyika nyumbani kwake Migombani, Unguja siku ya Jumatatu ya Tarehe 15/08/2016.

Marehemu Mzee Aboud Jumbe alizaliwa tarehe 14 Juni, 1920, Zanzibar. Alifanikiwa kupata elimu yake hadi kufikia ngazi ya Shahada ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda. Mara baada ya kumaliza Chuo Kikuu alianza kazi ya ualimu ambapo alifundisha Skuli ya Sekondari Lumumba kwa wakati huo ikiitwa *KING GEORGE VI SCHOOL*.

Wakati wa harakati za kisiasa, Mzee Aboud Jumbe aliacha kazi ya ualimu na kujiunga na chama cha *Afro*- Shirazi (*ASP*) ili kuungana na Waafrika wengine katika kudai Uhuru wa nchi yetu. Baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, marehemu Aboud Jumbe alikuwa miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Waheshimiwa Wajumbe, mara baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa kwanza wa Zanzibar Mzee Abeid Amani Karume kilichotokea Aprili 7, 1972, Marehemu Aboud Jumbe Mwinyi ilipofika tarehe 11/4/1972 aliapishwa rasmi kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wadhifa ambao ulimwezesha pia kuwa Mwenyekiti wa Chama cha *Afro*-Shirazi na Makamu wa kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, mara tu baada ya kuunganishwa kwa vyama vyetu vya *ASP* na TANU mwaka 1977, marehemu Aboud Jumbe Mwinyi alikuwa Makamo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, nyadhifa zote hizo alizishikilia hadi tarehe 30/1/1984.

Waheshimiwa Wajumbe,Watanzania tunamkumbuka Mzee Aboud Jumbe kwa mengi aliyoyasimamia kwa moyo wake wote kama kiongozi jasiri. Miongoni mwa mambo makubwa ambayo yatabaki milele katika historia ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ni suala la kuunganishwa kwa vyama viwili vya siasa vya TANU na *ASP* tarehe 05/02/1977, kutungwa kwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1979, Katiba ambayo ndiyo iliyotoa uwezo wa kuanzishwa kwa chombo chetu hichi cha Kutunga Sheria.Baraza la Wawakilishi lilianzishwa mwaka 1980 na hatimae chombo hichi kutunga Katiba mpya ya mwaka 1984 ambayo ndio tunayoitumia hadi leo.

Waheshimiwa Wajumbe, katika kusimamia maendeleo ya wananchi, Marehemu Mzee Aboud Jumbe alijitahidi sana kuelekeza madaraka mikoani ambako kulianzishwa kamati za Mapinduzi za Wilaya na Mikoa. Kamati hizo zilikuwa pia na uwakilishi wao kwenye Baraza la Mwanzo la Wawakilishi.

Juhudi zake hizo za kujenga demokrasia ndizo zilizowezesha leo hii kuwa na utaratibu wa kuchaguana kupitia chaguzi mbali mbali katika majimbo yetu.

Waheshimiwa Wajumbe, ni dhahiri kuwa tumeondokewa na kiongozi muhimu sana katika uhai wa chombo chetu cha Kutunga Sheria kwani Mzee Aboud Jumbe Mwinyi alikuwa kiongozi mzalendo, mwenye hekima, busara na mahiri na mwenye kusimamia alichokuwa akikiamini katika kuleta maendeleo ya Taifa letu. Kupitia nafasi zake mbalimbali alizowahi kuzifanyia kazi, ametoa mchango mkubwa katika kuhakikisha ukuaji wa demokrasia, maendeleo ya watu na ukuaji wa uchumi. Bila ya shaka mchango mkubwa alioutoa

utaendelea kuthaminiwa na kuenziwa kwa kuigwa na sisi tuliobaki pamoja na vizazi vyetu vijavyo.

Waheshimiwa Wajumbe, tunamuomba Mwenyezi Mungu aijaalie familia ya Marehemu pamoja na wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ustahamilivu kufuatia kuondokewa na Mzee wetu huyu tukielewa kwamba sote ni waja wa Mwenyezi Mungu na hapana shaka marejeo yetu ni kwake yeye.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa mnasaba huo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wote kwa pamoja tusimame kwa dakika moja ili kila mmoja amuombee dua Mzee wetu na kipenzi chetu Marehemu Mzee Aboud Jumbe Mwinyi.

(Hapa Wajumbe walisimama kwa dakika moja kumuombea dua Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi)

Mhe. Spika: Ahsanteni.

Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *amin*.

Waheshimiwa Wajumbe, taarifa nyengine niliyokusudia kutoa kwenu na kwa wananchi kwa ujumla ni kuhusu miswada ya sheria iliyopitishwa katika mkutano uliopita wa Baraza.

Katika Mkutano wa Pili wa Baraza la Tisa la Wawakilishi ulioanza tarehe 18 Mei 2016, Baraza lilipitisha Miswada Mitatu (3) ya sheria ambayo ni:-

1) Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

2) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

3) Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nane na Arobaini na Moja Mia Nne na Sabiini na Saba Milioni na Laki Tano kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia siku ya tarehe Thalathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Kumi na Saba na Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo, pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Kama inavyotakiwa chini ya kifungu 91(3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012; naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo sasa imekuwa ni sheria kamili baada ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Waheshimiwa wajumbe, nawashukuru sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kabla ya kuwasilisha hati Mezani, naomba kwa ruhusa yako nitoe mkono wa pole kwa ndugu zetu waliopata na maafa makubwa ya tetemeko la ardhi lililotokea katika Mkoa wa Kagera, ambao wameathirika na wengine kupoteza maisha, wengine wameumia, kupoteza nyumba na mali. Sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi wote wa Zanzibar tunatoa mkono wa pole kwa maafa hayo.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 30 June, 2016.

Mhe.Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Hotuba ya uwasilishaji wa Mswada wa Sheria Kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 3

Tatizo la Unyanyasaji kwa Wafanyabiashara Wadogo Wadogo

Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Aliuliza :-

Serikali imekuwa ikitoa mkazo kwa watu kufanya kazi kwa kujipatia kipato, lakini wafanyabiashara wadogo wadogo wamekuwa wakinyanyasika na kudhalilika hasa wanapo kuwa katika maeneo yao ya biashara, mfano Mwanakwerekwe na Darajani.

Je, ni lini Serikali itaweza kuwawekea utaratibu mzuri ili wasihangaike na huku Halmashauri zetu zinakuwa zikiwatoza kodi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Namba 3 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba nikiri kuwa kumekuwa na tatizo la msongamano mkubwa wa watu katika maeneo ya masoko yetu makuu ya Darajani na Mwanakwerekwe. Hali hii sio tu inakuwa bughudha kwa watumiaji wa maeneo hayo bali pia inachafua haiba ya masoko na kuwavunja moyo hata wageni wanaotembelea maeneo hayo hasa soko la Darajani ambalo ni moja ya vivutio vya Watalii wanaotembelea Mji Mkongwe. Mara kadhaa uongozi wa Baraza la Manispaa linapochukuwa hatua za kupunguza msongamano huo kwa kuondosha wafanyabiashara katika maeneo yasiyoruhusiwa, hatua hizo hutafsiriwa kama unyanyasaji jambo ambalo sio kweli.

Mhe. Spika, haiwezekani hata kidogo mtu yeyote akafanya biashara yoyote mahali popote bila kufata utaratibu uliowekwa na mamlaka husika. Haiwezekani kila kona ya Mji kukawa na wachuuzi wa samaki, mama ntilie na biashara nyengine. Ni dhahiri biashara za namna hii sio tu zinaharibu mazingira na kusababisha misongamano, lakini pia zinaikosesha Serikali mapato.

Katika kukabiliana na hali hii na kwa kuwajali wananchi wake, Serikali kupitia Manispaa zake na Halmashauri zitaendelea kuweka mazingira rafiki kwa

wafanyabiashara wadogo wadogo ili kuweza kuendelea na biashara zao kwa kufuata utaratibu. Hivi sasa Baraza la Manispaa tayari limetenga sehemu maalum eneo la Saateni kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo ili kupunguza msongamano katika maeneo ya Darajani na Mwanakwerekwe.

Mhe, Spika, Baraza la Manispaa linaendelea kuwaelimisha wafanyabiashara waliopo katika maeneo ya Darajani na Mwanakwerekwe kuondoka katika maeneo hayo na kuelekea katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Kwa kufanya hivyo, zile hisia za manyanyaso yanayolalamikiwa dhidi ya wafanyabiashara wadogo wadogo hazitakuwepo tena.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini naomba kuuliza masuali mawili ya nyongeza.

a) Kwa kuwa Mhe. Waziri, kikiri kwamba Wafanyabiashara hao wamekuwa wanapata adha kwa namna moja au nyengine, na jihada za mahusi kabisa zimefanyika kwa wale wafanyabiashara wadogo wadogo waliokuwepo pale maeneo ya Darajani, na kwa kuwa jitihada za Serikali zimekuwa zikionekana.

Je, ni lini sasa Serikali itatafuta namna kwa hao wafanyabiashara wengine wadogo wadogo hususan waliokuwepo katika Soko la Mwanakwerekwe, maana hali inazidi kuwa mbaya.

b) Kwa kuwa Serikali na Manispaa zimekuwa zikijitahidi katika kuweka mji katika hali nzuri na kuwarahisishia wafanyabiashara wetu, sasa ni lini sasa Ujenzi utaanza kwa haraka katika yale maeneo ya Darajani ambayo wafanyabiashara wengi wameondolewa kwa kupisha ujenzi ule.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye (a) na (b) kama ifutavyo:

a) Serikali tayari imetengeneza mazingira ya kuwahamisha wafanyabiashara wa Darajani kwenye soko la Darajani na soko la Mwanakwerekwe kuwahamishia soko la Saateni, kilichobakia sasa hivi ni mazoea ya wafanya biashara kutokuamini kwamba wakifika Saateni wanaweza wakafanya biashara kama walivyokuwa wakizifanya biashara katika maeneo hayo.

Hata hivyo Serikali kupitia Baraza la Manispaa tutaendelea kuwashajihisha na kuwaelimisha wafanyabiashara ili wafuate utaratibu huo na waweze kufanya biashara zao katika eneo la Saateni.

b) Ni lini ujenzi wa Darajani *Corridor* utaanza, ujenzi wa Darajani *Corridor* utaanza pale tu baada ya Serikali kukamilisha taratibu ambazo hivi sasa inaendelea nazo za kuhakikisha kwamba eneo lote la ukanda wa Darajani kutoka Mnazimmoja mpaka uwanja wa Malindi michoro yake yote ikiwa imekamilika na hasa baada ya kupata ridhaa ya *UNESCO* kufuatia utaratibu wa kufata uhifadhi wa Mjimkongwe.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza katika swala la Mhe. Waziri wa Nchi. Mhe. Waziri, kama inavyofahamika katika miaka 7 iliyopita kuna baadhi ya wafanyabiashara waliondolewa katika soko lisilo rasmi la Mlandege wakapelekwa Kinazini, ambalo sasa hivi Taasisi yako inaifanyia ukarabati. Kuna wafanyabiashara wengi sana pale walikuwa wanafanya kazi zaidi ya miaka 6.Cha kusikitisha hivi maeneo yale yamehodhiwa na Manispaa na kuanza ujenzi. Je, wale vijana ambao walikuwa pale zaidi ya miaka 6 watafanyiwa utaratibu gani kupatiwa maeneo hayo, la kwanza.

La Pili, vile vile, kuna suala zima la ukusanyaji wa kodi katika soko la jioni Darajani, kuna baadhi ya wafanyabiashara mbali mbali pale wa madafu, wa samaki na wa mitumba, wakati sasa hivi wote wale wanafanya biashara ile na kodi inatozwa, lakini wiki mbili zilizopita mpaka tatu wale watu wamezuiliwa wasifanye biashara hiyo pale na wakati baadhi wamebakishwa. Je, Serikali hili inatoa tamko gani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, ni kweli kabisha wako wafanyabiashara wa Mitumba walioondoshwa katika eneo la Mlandege na sio Soko la Mlandege.Wameondoshwa katika eneo la Mlandege karibu miaka 6 iliyopita. Kwanza nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru sana wafanyabiashara wale kwa kuitikia wito na kufuata maelekezo ya Serikali. Mimi mwenyewe binafsi miaka 3 iliyopita nyuma nilikwenda nikakaa na kuzungumza nao, moja katika ya jambo ambalo walikuwa wakililalamikia kwamba katika eneo la Saateni hakuna biashara. Mimi niliwaahidi kwamba tutahakikisha kwamba eneo la biashara la Saateni linakuwa kwa kuwahamisha wafanyabiashara waliopo katika maeneo ya Darajani wanaofanya biashara kiholela kuwapeleka sokoni Saateni ili wakaungane nao.

Kabla ya kuwahamisha wafanyabiashara nilikwenda nikazungumza nao na Baraza la Manispaa pamoja na Mkoa wa Mjini Magharibi walinihakikishia kwamba watawazingatia kwanza wafanyabiashara ambao wapo katika maeneo ya Saateni kuwapa nafasi za kufanya biashara ili wao waweze kufanya

biashara. Mimi naamini kama kuna taarifa zaidi ya hizo ambazo ninazo mimi nipende kukuarifu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba nitazifatilia, lakini kwa imani yangu naamini kwamba wafanya biashara hao wapo isipokuwa sasa wamewekewa utaratibu wa namna biashara zao watakavyokuwa wanazifanya. Kwa sababu eneo la Saateni si eneo ambalo linatakiwa limilikiwe na wafanya biashara, linamilikiwa na Serikali kupitia Baraza la Manispaa na wanapewa nafasi kwa ajili ya kufanya biashara zao.

Sasa tatizo liliopo kwa baadhi ya wafanya biashara wanataka waendelee kumiliki maeneo ili wasiweze kufuata ule utaratibu uliowekwa. Hata hivyo, napeda niseme kwamba kama lipo tatizo basi nitalifatilia na tuweze kulitatua kwa sababu nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunawajengea mazingira mazuri wafanya biashara wadogo wadogo.

Pili, wapo wafanya biashara katika soko la jioni wanaofanya biashara na hatimaye wameondoshwa. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba wafanya biashara ambao hawana maeneo maalum katika maeneo yetu ya masoko ni kuhakikisha wanaondoka na kwenda katika Soko la Saateni. Sasa kama bado wameondoshwa na wengine wameachwa mimi siamini, kinachotokea kwamba hao waliobakia wanafanya biashara kwa nguvu kwa kuvizia, wakiona watu wa Manispaa hawapo wanafanya biashara, kwa hivyo, hao wanavunja utaratibu. Lakini wafanya biashara wote katika eneo la Darajani tumeamua Serikali waondoke.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, na mimi naomba nimuulize swali dogo la nyongeza Mhe. Waziri. Kinachoonekana Mhe. Waziri, kwenye masoko yetu yaliyojengwa zamani na ninazungumza zaidi Soko la Darajani na Soko la Mwanakwerekwe na *population* ya Wazanzibari kupitia wafanyabiashara pamoja na wenye mahitaji imeongezeka kwa kasi kubwa sana na hicho ndicho kinachoonekana ndio tatizo la watu kukosa maeneo ndani na kuja kufanya biashara nje. Je, Serikali ina mpango gani ya kujenga soko la kisasa ambalo litakwenda na mahitaji ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, nakiri kwamba masoko yetu hasa Soko la Darajani ni soko ambalo limejengwa zamani na halikidhi mahitaji ya wafanyabiashara wa hivi sasa. Kwa sababu ya ongezeko la idadi ya watu na upanuzi katika mji wetu hasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi, ndio maana Serikali ilifanya juhudi ya kujenga Soko la Mwanakwerekwe, Soko la Mikunguni na Soko la Mombasa na kabla ya hapo ilijenga Soko la Kwahani pale Kijangwani.

Hata hivyo, masoko yote hayo nakiri kwamba yamezidiwa na idadi kubwa ya wafanya biashara wadogo wadogo. Serikali kupitia Halmashauri na Manispaa inao mpango wa kujenga masoko katika maeneo mengine yaliyo wazi kwa ajili ya kuondosha tatizo hilo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuzingatia Kanuni ya 27(4), naomba tuyaruke maswali ambayo yanafuata, twende moja kwa moja kwenye swali namba 192 la Wizara ya Ardhi ili kumuwezesha Mhe. Waziri, baada ya kujibu swali hili aweze kwenda kukamilisha zinazohusiana na Baraza la Wawakilishi. Kwa maana hiyo sasa nitamwita Katibu ili sasa aitangaze hiyo Wizara ili tuweze kuendelea, baada tutarudi tena kwenye utaratibu wa kawaida.

Nam. 192

Ukosefu wa Huduma za Uungaji Umeme katika Kijiji cha Paje

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Wananchi wa Kijiji cha Paje wamelipa gharama za kuunganishwa umeme tangu mwaka 2015, lakini mpaka leo hii wameshindwa kupata huduma hiyo wakati umeme ni nguzo ya uchumi kwa wananchi masikini katika kuongeza kipato cha kujiajiri.

a) Je, ni sababu gani mpaka leo hii washindwe kuunganishiwa umeme pamoja na kulipa gharama za kuunganishiwa umeme.

b) Je, ni muda gani mtu anatakiwa kupelekewa huduma hiyo ya umeme tangu alipolipa na munawaeleza nini wananchi hao ambao wanasubiri umeme usiofika.

c) Je, kwa kuwa wananchi hao walitarajia kuvuta umeme na kutumia katika shughuli zao za kiuchumi mtawalipa fidia kiasi gani baada ya shughuli zao kukwama.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje swali lake namba 192 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kwa kumbukumbu zilizopo ndani ya Shirika langu la Umeme hakuna mwananchi hata mmoja aliyekamilisha taratibu zote za kuungiwa umeme na kulipia katika mwaka 2015 hadi leo ambaye hajaungiwa huduma hiyo. Hata hivyo, kama yuko mwananchi yeyote ambaye amekamililisha taratibu na mpaka leo hajaungiwa umeme basi tunaomba awasilishe katika Shirika vielelezo vyake vyote ili Shirika lichukuwe hatua za kumuungia umeme.

b) Mhe. Spika, kutokana na Shirika kuboresha huduma zake kwa kawaida mwananchi anapokamilisha taratibu ndani ya siku 21 sasa hivi basi anapata huduma ya kuungiwa umeme akiwa ndani ya mita 30 ya eneo ambalo anatakiwa kuungiwa umeme. Lakini akiwa nje ya mita 30 basi ndani ya mwezi maana ya siku 30 atakuwa ameungiwa umeme.

c) Vile vile, naomba nimjibu swali lake la (c) ambalo aliulizia kuhusu kulipa fidia kwa wachelewaji. Naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Paje Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwamba Shirika lina utaratibu wa kulipa fidia kwa wale wanaounguziwa na umeme labda umeme mkubwa, lakini halina utaratibu wa kulipa fidia kwa ucheleweshaji wa kuunga umeme.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu wa kusikitisha na kwanza nimpe pole Sheha wangu na wananchi wake kwa kwenda mara kadhaa katika Shirika na kufanya mazoezi bila ya kukusudia kupanda ngazi na kushuka. Mhe. Spika, kuna Kanuni za Baraza sitaki kuzitumia Waziri angali mpya zinatukataza, lakini ninamuomba muhusika aje achukue vielelezo hivi na kama utaomba radhi Baraza itakuwa si vibaya ili uchukuwe kama ninayozungumza mimi ni cha uhakika au si cha uhakika, unajua ukijipanga ujipange.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, naomba uulize swali vielezo utamkabidhi baadae Mhe. Waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sijesha Mheshimiwa, bado.

Mhe. Spika: Umekaa chini Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ukazungumza Kanuni natakiwa nikae chini, ukazungumza wewe natakiwa niheshimu kiti chako.

Mhe. Spika: Uliza swali Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Waziri, vielelezo ninavyo, lini wananchi hao utakaa nao ili wapate huduma hii ya umeme na wameshachoka kufanya mazoezi ya viungo, vielelezo hivi hapa, ninachozungumza ni sahihi, risiti hizi hapa, orodha yao ni hii. Ni lini utakaa nao wananchi hao.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, hakuna mwananchi wa Jimbo la Paje aliyekamilisha taratibu, kama taratibu hazijakamilika na kama vielelezo vyake havijastahiki kuungiwa umeme, hatoungiwa umeme mpaka atakapokamilisha taratibu na masharti aliyopewa na Shirika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, mimi kwanza ninampongeza Mhe. Waziri, Meneja wa Shirika la Umeme na watendaji wake kwa kazi nzuri wanaojitahidi kufanya ili kuhakikisha kwamba kero la umeme linaondoka katika nchi yetu. Swali langu lipo hapa, wananchi wengi hasa viongozi, Wawakilishi na Wabunge wako tayari kuwahudumia wananchi wao ili kupata huduma ya umeme.

Lakini baadhi ya wakati taratibu zinakosewa kidogo, tunakoelekea huwa kunakosekana. Je, kwa kuwa kuna eneo fulani ambalo Mhe. Waziri, analijua upande wangu mimi tumetekeleza kama inavyotakiwa na Shirika, lakini bahati mbaya nguzo zilizokusudiwa kupelekwa kule kwetu hazikupelekwa, zimepelekwa kwengine, hili ataniamulia nini na wananchi wangu wasikie kwamba wananchi wanapata ile huduma ya umeme kama tulivyokubaliana katika Baraza hili.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, sina uhakika sana, lakini naomba nilichukue na nilifuatilie. Kwa sababu mimi ninachojua kuhusu hili kwamba kweli alikuja kwetu akaomba na alikabidhi na mafundi waliamua kufanya kazi. Lakini sina uhakika sana narudia kwamba utaratibu wa upelekaji labda uko tofauti kidogo, lakini naomba nikuhakikishie kwamba nikitoka hapa nitalichukua na nitalifanyia kazi ipasavyo na kukuletea majibu sahihi. (*Makofi*)

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri, kwa majibu yake mazuri kwenye Baraza hili, lakini pamoja na kumpongeza naomba kuuliza swali langu kama ifuatavyo. Serikali ya

Mapinduzi Zanzibar imekuwa na malengo na sera za kuwapelekea umeme wananchi wake ili kupata huduma hii ya nishati. Ni mambo gani katika miundombinu ambayo yanatakiwa yafanywe na Shirika na mambo gani yafanyiwe na wananchi wenyewe; mfano nguzo, mita na kadhalika. Ni mambo gani ambayo yanakwenda kwa wananchi na mambo gani yanakwenda kwa Shirika ama Serikali.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, Shirika lina majukumu yake katika kupeleka umeme vijijini kama Serikali. Sisi tuna mpango mzuri kuhakikisha kwamba wananchi katika maeneo yote mijini na vijijini wanapata umeme. Jukumu letu kama Shirika kufikisha umeme katika sehemu husika. Mfano tunasema tunafikisha umeme Jimbo la Bumbwini, kwa hivyo, ndani ya Jimbo la Bumbwini umeme umevutwa umefika katika eneo moja, ukifika pale kuutoa kufanya *network*, yaani *connection* kutoka pale kuingia katika majumba ya watu na sehemu nyengine, yaani ni jukumu la muhusika mwenyewe ambaye ataomba umeme. Lakini hata hivyo, kama eneo liko mbali zaidi kutoka eneo moja kama nilivyosema kama eneo linahitaji nguzo zaidi ya nne au tano au sita, Shirika basi pia linachukua nafasi ya kuona kwamba umuhimu wa kumsogezea umeme mwananchi yule alipie nusu ya zile nguzo na baadhi ya nguzo husaidiwa na Shirika.

Vile vile, katika kuona ugumu wa suala hili pia Shirika limetoa ruhusa na limetoa fursa kwa wananchi wake ya kuchukua mkopo pale ambapo hana uwezo wa kulipia kuunga umeme. Kwa hivyo, anapojaza fomu ile ya mkopo Shirika linakuwa ule mzigo na anaweza kulipia kidogo kidogo, lakini ana jukumu la kulipia umeme na gharama fulani ambazo zitaweza kumuwezesha apate umeme na Serikali kama Shirika linafikisha umeme katika eneo husika.

Nam. 156

Tatizo la Ajira kwa Vijana wenye Elimu Ndogo

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Serikali hutangaza nafasi za kazi na kusema waombaji wawasilishe vyeti vyao na masharti mengine. Lakini kwa kuwa tuna vijana wengi wanaomba kazi na wengine elimu yao ni ndogo na elimu hiyo ndogo kwa kazi iliyotangazwa hata elimu ya darasa la saba au la kumi inafaa, lakini matangazo yanatangazwa kwa vijana anayetaka kuomba kwa elimu yoyote ile.

a) Je, Serikali haioni kuwa inawanyima ajira wale wenye elimu ndogo na wao wanaiweza kazi hiyo.

b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutowa Taaluma kwa waombaji wa ile kazi inayoombewa ili wale wenye elimu ndogo nao wafaidike na Serikali yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake Nam. 156 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi naomba kwanza kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe.Spika, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake kuhusu utaratibu unaotumiwa na Serikali kutangaza nafasi za kazi kwa kuwataka waombaji kuwasilisha vyeti na sifa nyengine zinazohitajika. Aidha, ni kweli kwamba tuna vijana wengi wanaomba kazi ambao wana elimu ndogo, lakini pia wapo vijana wengi wenye elimu kubwa ambao hadi sasa hawajaajiriwa kutokana na uchache wa nafasi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, uajiri katika serikali unazingatia matakwa ya muundo wa utumishi wa kada husika kwa nafasi iliyopo na mahitaji ya taasisi husika, ambapo katika nafasi hiyo huelezwa kiwango cha elimu kinachohitajika na sifa nyengine mbali mbali ili iweze kujazwa. Aidha, kwa nafasi za kada ndogo za elimu ya sekondari zinapotokezea nazo hushughulikiwa kwa mujibu wa mahitaji na sheria iliyopo.Kwa mantiki hiyo, serikali haiwezi kuwanyima nafasi za ajira vijana wake bali inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

b) Mhe. Spika, utaratibu wa utoaji wa mafunzo kwa vijana ambao wana elimu ndogo kwa ajili ya kuwawezesha kuajiriwa katika nafasi za kitaalamu haujaanzishwa kwa sasa. Hata hivyo, serikali imeandaa

mipango kadhaa ya kuwasaidia vijana wenye elimu ndogo kupata ajira, ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo vijana hao ili waweze kuajiriwa au kujiajiri kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na mikopo. Kwa sasa mafunzo hayo yanatolewa na Vyuo vya Mafunzo ya Amali na pia husimamiwa na Wizara inayoshughulikia masuala ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru na mimi, nitoe shukurani zangu kwa Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, pamoja na utaratibu wa serikali wa kuajiri kwa taaluma zake, lakini inaonekana kama uajiri wake ni uajiri wa mazoea, maana yake hauzingatii na matakwa ya sasa hivi. Sasa hivi kuna ajira nyingi tu kama vile za madereva na maeneo mengine sijamuona mwanamke hata mmoja akiwa na ajira ya udereva, na serikali haijatia motisha kwamba tunataka madereva wa mawaziri wawe wanawake. Kwa hivyo, serikali imejipangaje kuwatia motisha wanawake hawa ili na sekta hizi waweze kufanikiwa.

b) Mhe. Spika, nilikuwa nazungumzia suala la ajira kuhusu habari ya elimu. Sasa hivi tukienda kwenye taaluma za elimu tunakuta eneo la hospitali kama vile ma-*orderly* tunamjua ni mtu wa kiwango cha chini, lakini anaweza kufanya kazi nzuri kutokana na elimu ndogo aliyonayo. Lakini wakati wa kusema kama tunataka ajira anakwenda mtu wa chuo kikuu ukimjua fika huyo chuo kikuu hatofanya kazi ya *orderly*, anapita njia tu na kuhamisha. Kwa hiyo, wale wenye taaluma zile na wenye uwezo wanakuwa wamezuiwa kutokupata zile nafasi. Je, serikali ina mpango gani kuhusu watu wale ambao elimu yao ni ndogo lakini ni nguvu kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma:

(a)Mhe. Spika, serikali inapotoa ajira hufata utaratibu wote ule ambao unahitajika kulingana na sheria na kanuni zilizokuwepo. Hivyo, nafasi hizo huwa wazi kwa wanawake pia na kwa wanaume. Sasa kutokuwepo kwa wanawake katika nafasi hizo za madereva hiyo haisababishi kwamba kunakuwa kuna upendeleo. Isipokuwa wanawake wenyewe tu huwa hawajitokezi kuomba nafasi hizo za madereva, lakini iwapo wangeweza

kujitokeza hakuna upendeleo wowote, wote wana haki sawa na wangeweza kupatiwa ajira hiyo.

b)Mhe. Spika, ukweli ulivyo ni kwamba serikali inapotoa yale matangazo kwa ajili ya kuajiri wale vijana huwa zinatakiwa sifa maalum. Kwa hivyo, ikiwa sifa zile zinamuhusu mwananchi mwenye elimu ya kidato cha pili au mwananchi mwenye elimu ya kidato cha nne utaratibu hufuatwa kama ilivyo kawaida. Kwa mfano, kama wanatakiwa vijana wenye elimu ya *Form IV* utaratibu ni kwamba wao wanapoomba huwa haangaliwi yule ambaye mwenye cheti cha chuo kikuu, hapana kwa sababu ajira ile imetoka kwa *Form IV*, kwa hivyo utaratibu ni kwamba wale vijana wa *Form IV* ndio ambao wanaochaguliwa kwa ajili ya ajira hiyo na sio chuo kikuu. Lakini iwapo zitakuja ajira kwa chuo kikuu na akiomba *Form IV* bila shaka atakuwa hana sifa ya ile nafasi ambayo iliyoombwa. Kwa hivyo, huwa tunaajiri kulingana na zile sifa husika zilizotajwa katika lile tangazo la ajira.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa ruhusa yako ningependa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu cha (a) na (b).

a) Mhe. Spika, katika kikao kilichopita Mhe. Naibu Waziri, alikiri mbele ya Baraza lako kwamba atatumia mpango wa kuorodhesha vijana wetu ambao wanatafuta ajira katika Halmashauri zetu pamoja na Serikali zetu za Mitaa ili kuweza kujua wale ambao wana uwezo tofauti kuweza kuunganisha kwa pamoja katika sekta binafsi na wale ambao katika sekta ya umma wanaohitaji, kuna idadi maalum ya vijana ambazo tutazita kama ni *Job centre*. Ni utaratibu gani hivi sasa Mhe. Naibu Waziri, ameweza kutekeleza katika ahadi hiyo aliyoieleza hapa katika Baraza hili pamoja na ushauri huo.

b) Kwa kuwa serikali imeazimia katika Baraza letu hili kuunganisha vyuo vyetu vyote kwa pamoja ambavyo vimetajwa katika tangazo lao na hasa kule katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Lakini je, haoni kwamba katika kuunganisha vyuo hivi Mhe. Naibu Waziri, hasa katika Chuo cha Maruhubi kinaweza kikasababisha kuvunja nguvu hasa kwa vijana katika kutafuta ajira.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, utajibu swali moja tu, hili swali la (b) lipo katika shughuli ambazo zitakuwa zinafanywa na Baraza.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, utaratibu huo bado unaendelea, nia na lengo lipo pale pale la kuwaweka vijana wetu pamoja ili kuwakwamua na maisha yao magumu ili waweze kupata ajira inayostahiki.

Nam. 10

Uchakavu wa Skuli ya Chaani

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Kwa kuwa nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwa skuli zote zipo katika mazingira bora yatakayomuwezesha kila mwananchi kupata elimu bila usumbufu wowote. Hata hivyo, kukosekana kwa madawati na ubovu wa skuli ya Chaani kunasababisha wanafunzi walio wengi kusoma katika mazingira magumu na yasiyostahiki na hivyo kupelekea ufaulu mdogo wa wanafunzi.

a) Ni lini ukarabati wa skuli hiyo utaanza kufanyika.

b) Serikali imejipanga vipi katika kuwapatia madawati wanafunzi ili kuondokana na changamoto inayoendelea hadi hivi sasa katika skuli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 lenye vingu (a) na (b). Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanasoma katika skuli zenye mazingira bora, yenye madarasa mazuri vikalio vya kutosha. Mazingira mazuri huchangia katika kuinua ubora wa elimu, kwani inawahamasisha walimu na wanafunzi kujituma zaidi. Adiha, ni kweli skuli zetu nyingi ikiwemo skuli ya Chaani zinakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa majengo na uhaba mkubwa wa madawati.

Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na wahisani wakiwemo Shirika la Misaada la Kimataifa la Sweden (*SIDA*) na Milele Zanzibar *Foundation* inayafanyia ukarabati baadhi ya majengo ya skuli pamoja na vyoo kila hali ya kifedha inaporuhusu. Kwa mwaka 2015 – 2016 jumla ya skuli 19 zilifanyiwa ukarabati. Skuli hizo ni skuli za sekondari Langoni, Bububu Msingi, Kidagoni, Mbuyutende, Fukuchani, Kiongwe, Kituo cha Walimu Mwanda, Chwaka kwa

upande wa Unguja. Kwa upande wa Pemba skuli ya Mitiulaya, Gando, Ukunjwi, Wingwi Msingi, Msuka Msingi, Sizini, Makoongwe, Chambani Msingi, Kiwani Msingi, Ngwachani na Kwale zilifanyiwa ukarabati kwa upande wa madawati.

Mhe. Spika, wizara kwa kutumia fedha za ada ya bandari imekuwa ikichonga madawati na kuyasambaza katika skuli mbali mbali. Kwa mwaka 2015 – 2016 jumla ya madawati 300, viti vya wanafunzi 90, meza za wanafunzi 90 na viti na meza za ofisini 10 zilinunuliwa kutokana na fedha za ada za bandari. Samani hizo ziligaiwa katika skuli zifuatazo:-

Kwa upande wa Unguja ni Skuli ya Msingi ya Abdalla Sharia, Skuli ya Msingi ya Kidoti, Skuli ya Sekondari ya Fukuchani na Skuli ya Sekondari ya Kombeni.

Kwa upande wa Pemba ni Skuli ya Msingi ya Michakaini, Skuli ya Msingi ya Jadida na Skuli ya Msingi ya Uwandani.

Hata hivyo, uwezo wa wizara yangu kuzifanyia ukarabati mkubwa skuli zote na kuzipatia madawati bado ni mdogo ukilinganisha na mahitaji halisi. Hadi tarehe 30 June, 2016 skuli zetu zilikuwa na upungufu wa madawati 47,448 na viti na meza 45,716. Suala la kukabiliana na upungufu wa madawati katika skuli zetu hivi sasa imepata msukumo mkubwa baada ya serikali kuunda kamati ya kitaifa ya kuhamasisha jamii kuchangia fedha na madawati kwa ajili ya skuli zetu. Ni matarajio yetu kuwa upungufu wa madawati utapungua sana kwa kipindi cha hivi karibuni. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Wizara itaifanyia ukarabati Skuli ya Chaani kwa kadri ya fedha zitakavyoweza kupatikana.

b) Madarasa yatakayofanyiwa ukarabati yatapatiwa madawati ili kupunguza uhaba wa madawati katika skuli hiyo. Nina furaha kuwaeleza kwamba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imetuarifu kuwa watasaidia katika kupunguza tatizo la madawati katika skuli ya Chaani kupitia Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kaskazini. Kwa hiyo, wizara inaipongeza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa nia yao njema na naomba mashirika na taasisi nyengine isaidie katika kupunguza tatizo la madawati katika skuli zetu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, kwanza niwapongeze Wizara ya Elimu kwa kufanya ziara ndani ya jimbo langu nawashukuru sana.

Mhe. Spika, swali langu la nyongeza nitaomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa wazee wanyonge ndani ya Jimbo la Chaani ikiwemo Skuli ya Chaani pamoja na Skuli ya Pwani Mchangani wamechangishana kwa kuhakikisha kwamba madarasa pamoja na mabati kutokana na wanafunzi wana mitihani na kunavuja na matatizo mengine. Kwa upande wa Wizara ya Elimu ningependa kusikia kauli kutoka kwao ni kiasi gani wataweza kuchangia haraka iwezekanavyo ili tukapata kuweka mabati katika skuli zile mbili na kuziba sehemu ambazo ni za muhimu kwani wanafunzi wanapata matatizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, tumesema kwamba hatua zote za ukarabati wa skuli na madawati pamoja na mambo mengine yote itafanyika wakati wowote pale fedha itapopatikana. Wizara inajitahidi kutafuta fedha hizo kupitia wahisani wa maendeleo, lakini pia kupitia watu wengine ambao wana moyo wa kusaidia. Kwa hivyo, kama tulivyojibu katika swali mama ni kwamba tutatengeneza wakati ambapo fedha zitakapopatikana.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, kufuatia kauli yako ya kusema kwamba skuli utazitengenza hapo utakapopata fedha, tunakoelekea ni mazingira ya mvua skuli yangu ya Furaha ambayo iko katika Jimbo la Wawi ikinyesha mvua wanafunzi inabidi watoke wakajifiche kwenye majumba yao hawawezi kusoma.

Je, hatua gani za haraka utachukua kuhakikisha skuli ile ikifika kipindi cha mvua Februari, Machi na Aprili wanafunzi wakasoma mule kwa usalama na uhakika kama lengo la serikali inavyotaka. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya skuli zinakabiliwa na tatizo hili. Kwa hivyo, wizara inatoa wito kwa wahisani wengine mbali mbali akiwemo Mhe. Mwakilishi, mwenyewe aliyeuliza swali hili kutusaidia katika kutatua tatizo hili. Lakini hata hivyo, wizara italifuatilia suala lako kwa kushirikiana na wewe mwenyewe Mwakilishi tuone tunachukua hatua gani.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Mhe. Spika, ahsante na mimi nimshukuru na kumpongeza Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri, lakini pia niipongeze serikali kupitia Wizara ya Elimu kwa kuendeleza mabanda na kuongeza vyumba vya madarasa katika maeneo yetu ya maskuli. Lakini kwa masikitiko makubwa katika skuli hizo ikiwemo Mkoa wangu wa Kusini kwenye Skuli ya Charawe, Ukongoroni bado kuna tatizo la uhaba wa vyoo, na

ukizingatia madarasa yameongezeka na wanafunzi wanaongezeka, lakini bahati mbaya matundu vya vyoo ni machache. Nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, anatuhakikishia vipi wananchi wa Charawe na Ukongoroni ili kuweza kutusaidia angalau hii huduma ya vyoo katika maeneo yetu. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kuna upungufu wa matundu ya vyoo katika skuli mbali mbali za Unguja na Pemba, hilo wizara inaelewa na pale ambapo uwezo wa kupatikana wizara husaidia. Hivi karibuni tumeweza kusaidia matundu mbali mbali katika skuli nyingi za msingi na sekondari Unguja na Pemba. Hata hivyo, ningemshauri Mhe. Mwakilishi, kushirikiana na kamati za skuli kuona tatizo hili wanalitatua, mimi katika jimbo langu kwa mfano nimeshirikiana na kamati za skuli kuweza kusaidia utengenezaji wa matundu ya vyoo katika skuli mbali mbali. Kwa hivyo, na wewe nakuomba tushirikiane na pale wizara itakapopata nguvu itatia msukumo wake. Ahsante.

Nam. 43

Malipo ya Pensheni kwa Wazee

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetimiza ahadi yake ya kulipa pensheni kwa wazee waliofika umri wa miaka 70.

a) Je, ni wazee wangapi waliolipwa pensheni hiyo kati ya wazee 21,000 waliopaswa kulipwa.

b) Je, ni wazee wangapi waliokufa kabla ya malipo kuanza, na hatua gani zimechukuliwa.

c) Je, serikali imejipanga vipi kuongeza kima cha pensheni cha 20,000/= ikizingaitiwa kwamba wazee hawa wanamahitaji mengi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 43 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kama inavyoeleweka kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetimiza ahadi yake ya kulipa pensheni kwa wazee wote wenye umri wa miaka 70, na kuendelea kuanzia mwezi Aprili mwaka huu. Jumla ya wazee 21,263 walitarajiwa kulipwa katika mwezi huo; Unguja ni 12,722 na Pemba ni 8,541. Jumla ya wazee 18,371 walilipwa, Unguja ni 11,019 na Pemba ni 7,352. Wazee waliokuwa hawajalipwa wamefanya asilimia 14 ya wazee wote waliotarajiwa kulipwa. Miongoni mwa sababu zilizopelekea kutolipwa ni ucheleweshwaji wa taarifa kutoka kwa masheha kwenda kwa walengwa. Mvua kubwa iliyonyesha katika siku hizo, umbali wa masafa na baadhi ya wazee kufariki.

(b) Jumla ya wazee 107 Unguja na Pemba ambapo Unguja wazee 63 na Pemba 44 walifariki kabla ya kuanza hatua ya malipo.

(c) Hatua zilizochukuliwa na masheha kupitia ofisi za wilaya kuleta taarifa wizarani ambapo majina yao yaliorodheshwa katika orodha ya malipo. Ni dhahiri kima cha pensheni cha shilingi 20,000 ni kidogo ikizingatiwa kwamba wazee wana mahitaji mengi, lakini nia ya serikali ni kuongeza kima hicho sambamba na kupunguza umri wa kuingia katika programu hatua kwa hatua kadri ya hali ya uchumi utakavyoruhusu. Aidha, kwa vile ndio kwanza tumeanza utekelezaji wa mpango huo itakuwa vigumu kutoa tarehe maalum ya kuongeza kima hicho.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa amekiri kwamba kuna wazee ambao hawajalipwa fedha zao. Je, ni lini wizara au serikali itawalipa *arrears* zao za miezi ya nyuma baada ya kukamilishwa taratibu.

(b) Kwa kuwa fedha nyingi za serikali zinapotea kwenye malipo hewa. Je, wizara imejipanga vipi kuepukana na kulipa malipo hewa ya wazee.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba arejee swali lake la mwanzo.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Swali la kwanza nimesema kwamba, waziri amesema asilimia 14 ya wazee hawajalipwa kutokana na sababu mbali mbali na kuchelewa kwa taarifa zao. Je, ni lini serikali italipa malipo yao ya nyuma.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa wale wote ambao watakuwa waliingizwa majina yao katika tarehe za nyuma na orodha ile ipo wanapokwenda kwenye kituo kwa mara ya pili wanalipwa *arrears* zao zilizokuweko nyuma.

Swali la kwamba tunajipangaje juu ya suala la wazee hewa, tunaomba atusaidie sana wazee hewa kama wapo, ili tuthibitishe kwamba ni wazee hewa na tuweze kuwatafuta na kuwatoa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna manung'uniko ya baadhi ya wazee kwamba kuna watu ambao hawastahiki kulipwa, yaani hawajafikisha umri wa ile miaka 70 wanalipwa na wanaachwa wale wenye ule umri wa miaka 70 kwamba wao hawapati ile haki.

Je, hii wizara ina mpango gani wa kufanya uhakiki kuthibitisha kuwa wale ambao wanalipwa wamefikisha muda wa umri wa miaka 70 na wale ambao hawajafikisha umri ule wanaondolewa katika mpango huu wa malipo ya pensheni ya wazee.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, napenda kusema kwamba wizara imefanya jitihada ya hali ya juu kuhakikisha kwamba wale wote waliyoorodheshwa wanalipwa baada ya uthibitisho wa kuwa wana miaka 70. Lakini kuna wengine ambao wamewekwa na hawajafikia umri huo, itabidi wachukuliwe hatua, kwa sababu wanafanya wizi. Kama kuna mtu yeyote anayehusika kuwasaidia waweze kulipwa pasipo uhalali anakwenda kinyume na sheria na kama Mheshimiwa yeye mwenyewe anawajua mahali walipo, atuletee hiyo orodha na kwa kuwa tuna utaratibu wa kwamba mtu yeyote halipwi pasipo kwenda kuthibitisha.

Kuna wale wengine bahati nzuri wanaonekana vijana, lakini ni wazee wa miaka 70 waliojaaliwa na Mwenyezi Mungu, sijui wanakula nini tuwaulize, lakini kuna wale wanaoonekana ni wazee sana lakini bado ni wadogo hawajatimia umri huo. Sasa kama anaona watu hao anaweza kuthibitisha, tafadhali kwa heshima, naomba kabisa atusaidie ili tuweze kufanya kazi vizuri.

Nam. 77

Ukaguzi wa Vyakula Vilivyopitwa na Muda

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Aliuliza:-

Bismillah Rahmani Rahyym. Mhe. Spika, ahsante sana naomba kwanza niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi zake na uzima na kuweza kusimama hapa nikiwa katika hali ya uzima.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niendelee kuiombea dua nchi yetu, Mwenyezi Mungu atujaalie amani na utulivu na ampe hekima Rais wetu azidi kuendelea kutenda yale mazuri yote kwa wananchi wake aliyoyakusudia.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba swali langu lijibiwe.

Tumeona hivi karibuni Maafisa Biashara wakitembelea madukani kukaguwa vyakula ambavyo vimemaliza muda kwa matumizi ya binaadamu, jambo ambalo Serikali inastahili pongezi.

Je, Mhe. Waziri, anafahamu kuwa kuna baadhi ya wafanyabiashara hao wasiokuwa waaminifu hubadilisha *package* na kuweka *package* nyengine ili kudanganya tarehe sahihi ya kumaliza muda wa matumizi ya bidhaa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimpe pongezi Mhe. Shadya Mohamed (*Hajjat*) kwa kutimiza nguzo muhimu ya Uislamu kwenda kuhiji na namuomba atuombee sisi sote Mwenyezi Mungu atuongezee baraka na nchi yetu kama alivyofanya Rais wetu mpenzi.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 77 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inajuwa uwepo wa wafanyabiashara wasio waaminifu ambao hubadilisha *package* za bidhaa zilizokwisha kupitwa na wakati na kuweka *package* nyengine zenye tarehe za mbele ili kudanganya tarehe sahihi za kumalizika kwa muda wa matumizi ya bidhaa hizo. Hili limekuwa likifanyika sana kwa bidhaa zinazofungashwa kwa vipolo kama vile mchele, unga wa ngano na sukari. Ubadilishaji wa *package* hizo hufanyika katika maghala ya wafanyabiashara wakubwa wa bidhaa hizo.

Mhe. Spika, katika kulidhibiti suala hili wakaguzi wetu mbali ya kupitia kukaguwa bidhaa madukani, wamekuwa pia na ufuatiliaji wa kila mwezi wa bidhaa zikiwa ndani ya maghala ambapo ukaguzi wa ndani ya maghala hufanyika kwa ajili ya kuangalia upangaji wa bidhaa ndani ya maghala, uwepo wa bidha muhimu za chakula (mchele, unga wa ngano na sukari) na tarehe ya kumalizika muda wa matumizi kwa bidhaa zilizopo maghalani. Wakaguzi wakigundua kuna bidhaa zimebakia muda mchache wa kumalizika muda wake wa matumizi huziwekea alama bidhaa hizo na kufanya ufatiliaji wa karibu wa mwenendo wa bidhaa hizo kila wiki. Hatua hii imesaidia sana katika kuepusha suala hili la ubadilishaji wa *package* kwa bidhaa zilizopitwa na wakati.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri, wana hatua gani zinazochukuliwa kwa wafanyabiashara kama hawa wakigundulika.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, hatua mbali mbali zinachukuliwa pindi inapojulikana kwamba ndani ya ghala au ndani ya duka yule mfanyabiashara anabadilisha *package* kwa sababu ya tarehe ili bidhaa zile zitumike.

La kwanza la muhimu, bidhaa zile huwa zinachukuliwa zinawekwa pembeni halafu zinatekelezwa; ama zinachomwa moto, ama kuteketezwa kwa njia mbali mbali ambazo zinafanywa.

La pili, yule mfanyabiashara anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria kwa sababu sheria ya biashara inakataza kuweza kubadilisha tarehe za *package* ili kuuza, hii ni kuhatarisha maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii asubuhi kuuliza swali la nyongeza. Naomba nimuulize Mhe. Waziri, katika zoezi lote hilo analofanya, je, ni wafanyabiashara wangapi ambao wamebainika kufanya ubadhirifu kama huo na hatua zilizochukuliwa Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba nitamletea majibu yake kwa maandishi kwamba wafanyabiashara wangapi ambao wamekamatwa na bidhaa hizi.Lakini niseme tu kwa mwaka huu tunaoendelea nimeshapata kesi mbili Pemba, kesi ya kwanza ilikuwa sukari ambayo ilikuwa imemalizika muda na kesi ya pili ni mchele umemalizika muda. Walilalamika kwamba vyakula hivi vinaweza kuliwa, lakini tulichukua hatua na tukaviangamiza, lakini taarifa yote ya toka mwaka jana ni wangapi mpaka mwaka huu nitaleta kwa maandishi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yake ameelekeza zaidi katika bidhaa zinazoingizwa nchini ambazo zina *brand* na kuonekana kwa *expire date* yake, lakini ziko bidhaa pia zinaingizwa kama mchele, unga wa sembe hauna hata ile *useful life* yake, kwa maana hakuna hata hiyo *expire date* tutayoweza kuangalia. Ni mkakati gani wa serikali wa kudhibiti na kulinda hii hali. Kwa sababu ukiruhusu kuingiza maana yake umeruhusu kuuza na hauonekani muda wa kuishia yale mauzo yenyewe.

Kwa hiyo, nataka majibu ya serikali mkakati gani wanaoweka katika bidhaa kama hizi kwa huu mchele tunaouona unaingizwa kutoka Tanzania Bara na unga na maduka hayo hayo ndio yanayouza bidhaa hizo ambazo zimetengenezewa kwa *brand*, ndio hayo yanayouza unga na mchele huo. Tunataka mkakati huo ili tuone serikali inawalinda wananchi wake.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kama nilivyosema jukumu la kumlinda mlaji ni jukumu la serikali na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa hivi wizara yetu tumepewa *mandate* ya kuanzisha idara maalum ya kuweza kuleta biashara kuondosha ushindani uliokuwa unaathiri wananchi na vile vile kumlinda mlaji.

Mhe. Spika, mkakati uliopo kwa sasa hivi ni kwamba bidhaa zote zinazokuja nchini zinatakiwa vile vile hata kama zinatoka Bara, kwa sababu Bara kuna utaratibu wa kuzikagua, kuna ile Mamlaka ya Chakula na Madawa na hapa Zanzibar kuna Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi iko chini ya Wizara ya Afya. Pindi watendaji wangu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko wakigundua kwamba chakula, kwa mfano unga wa sembe wanapokwenda kukagua madukani unga wa sembe uliokuwa mzima na wenye matatizo unaonekana. Kwa hiyo, wanauchukua wanaupeleka katika maabara unafanyiwa utafiti na ukionekana haufai unaangamizwa.

Kwa hivyo, utaratibu sio kwamba kwa bidhaa tu zinazotoka nje ambazo zina *brand*, lakini hata za ndani, unga wa ngano pia ukionekana kwamba umepatikana ndani una matatizo na vyakula vyengine pia vinapelekwa kukaguliwa na kuharibiwa, vile ambavyo vinaonekana kwa ripoti ya Mkaguzi wa Bodi ya Vyakula na Madawa vinaharibiwa mara moja.

Nam. 41

Marejesho ya Ripoti za Vyama vya Michezo kwa *ZFA*

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Kwa kuwa Vyama vya Michezo vilivyosajiliwa chini ya wizara yako kwa mujibu wa sheria huwa vina jukumu la kisheria kufanya marejesho kila baada ya miezi mitatu.

(a) Je, ni mara ngapi *ZFA* wameshawasilisha wizarani kwako ripoti ya kila miezi mitatu tokea waliposajiliwa.

(b) Je, ni vyama gani vyengine vya michezo vilivyosajiliwa ambavyo havirejeshi marejesho.

(c) Je, ni vyama vingapi vilivyo sajiliwa vinavyorejesha marejesho kwa wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye rehma ambaye ametujaalia kukutana hapa leo kwa kikao hiki. Baada ya hayo sasa naomba kwa idhini yako nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 41 lenye vipengele (a), (b) na (c).

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu swali lake naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria Nam. 5 ya Mwaka 2010 ya BTMZ kifungu 34 - 36 Vyama vya Michezo vilivyosajiliwa havina jukumu la kuwasilisha ripoti na matumizi, isipokuwa Baraza la BTMZ pamoja na ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndizo zinazowasilishwa kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mjumbe swali lake lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, *ZFA* hawawasilishi wizarani ripoti zao za fedha.

(b) Kwa mujibu wa Sheria za BTMZ kifungu Nam. 34,35 na 36 vyama vya michezo havipaswi kufanya hivyo.

(c) Mhe. Spika, vyama vyote vilivyosajiliwa vinafuata taratibu za sheria na usajili na katiba zao. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) ni chama ambacho huwa kinasimamia timu za taifa; ikiwemo Timu ya Taifa ya Zanzibar na Timu ya Taifa ya Wanawake ambayo inaitwa *Zanzibar Queen*. Kwa kuwa hivi karibuni timu yetu hiyo (*Zanzibar Queen*) ilikuwa imeshiriki katika mashindano ya Afrika Mashariki (*CECAFA*) kwa upande wa wanawake na kwa huzuni na masikitiko ambayo timu yetu imefanya vibaya, mbali ya kwamba timu hii imeshiriki mashindano kwa mara ya kwanza.

Je, ni sababu gani iliyoifanya timu yetu kufanya vibaya katika mashindano haya na kutia aibu kufungwa magoli 30.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza napenda niwashukuru sana *Zanzibar Queen* kwa kuonesha ujasiri wao na kuionesha serikali kwamba wanawake wana moyo wa uvumilivu. Pamoja na magoli waliyofungwa lakini waliionesha serikali moyo wao wa ujasiri na hawakujali yale magoli waliyofungwa yote waliendelea na mchezo mpaka wakakamilisha mchezo ule.

Mhe. Spika, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba, serikali ikishirikiana na wizara ina mpango maalum wa kutafuta vijana kuwaendeleza zaidi kimichezo, lakini niombe tu kwamba na yeye Mwakilishi awe mdau kwa kuwaboresha vijana hawa ili lililotokea lisije likatokea tena. Pia, nisema kwamba wamelitangaza taifa letu vizuri na sasa hivi niseme pia Taifa letu linajuulikana kwa sifa zilizoonesha. Ahsante.*(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, *ZFA* ni Taasisi ambayo sheria zake zinapitishwa na mrajisi wa Vyama vya Michezo.

(a) Kwa nini *ZFA* Zanzibar ina kamati tendaji mbili Pemba yao na Unguja yao wakati ni nchi moja.

(b) Zanzibar tuna ***Premier League*** lakini kutokana na mfumo huu wa *ZFA* Unguja ***Premier League*** ni timu 16 Pemba 18, jumla ni 34

duniani kote hakuna suala kama hilo. Ligi zote kuu za Ulaya ni timu 20 na wenzetu Tanzania Bara ni timu 16. Kwa nini ligi yetu iko katika hali kama hii. Hali ambayo inasababisha mechi kuchezwa asubuhi na kuwafanya watu wasiende kazini wakaangalie mipira.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kunaonekana kuna matatizo na napenda sana nitoe pongezi kuona kuna Wawakilishi wanafuatilia sana suala zima la michezo.

Tatizo lililokuwepo kwa *ZFA* kwa kweli halihusu moja kwa moja suala la wizara. *ZFA* wanakwenda kwa mujibu wa sheria za *FIFA* na kufanya makosa wanayoyafanya kweli wanakiuka sheria za *FIFA* na ndio maana inaonekana kunajitokeza migogoro ya hapa na pale. Lakini wizara kwa jitihada zake imeweza kukaa sana na *ZFA* vikao visivyopungua viwili na imekaa na vyama vilabu vyote vya mpira wa miguu na tatizo hilo linapatiwa ufumbuzi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Machano Othman Said, awe mvumilivu kwenye hilo, tatizo lililokuwepo ni la kimakosa lakini litapatiwa ufumbuzi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 68

Jitihada za kukabiliana na wadudu waharibifu

Mhe. Mussa Foum Mussa: Aliuliza:-

Kwa muda mrefu serikali imekuwa ikichukuwa jitihada za kupambana na wadudu wanaoshambulia mimea na matunda kama vile embe, kunde, tungule na inapelekea wananchi wengi kutofanikiwa katika uvunaji wa mazao hayo kwa kutokuwa na uwezo wa kununulia dawa za kuulia wadudu hao.

Je, serikali inawasaidia vipi wananchi hao katika kukabiliana na tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Alijibu:-

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani, ni kweli lipo tatizo la wadudu waharibifu katika mazao aliyoyataja na mengine, kwa mfano zao la embe linashambuliwa na nzi wa matunda anaesababisha athari kubwa za kiuchumi, mnamo miaka ya 1990 kiasi cha tani 100 za embe zilikuwa zinasafirishwa katika nchi ya Ghuba na wakulima wakijipatia kipato na tija. Mwanzoni mwa mwaka 2000 usafirishaji wa embe ulipigwa marufuku

kutokana na kuwa embe zetu zinashambuliwa na kuathiriwa na nzi wa matunda.

Mhe. Spikia, zao la tungule nalo linashambuliwa na wadudu hatari sana anaeitwa *Tuta absoluta*. Mdudu huyu kwa mara ya kwanza amegunduliwa hapa Zanzibar mwaka 2015, ni aina ya kipepeo ambaye hushambulia mitungule katika majani na tungule zenyewe. Uharibifu unaofanywa na mdudu huyu unaweza kupeleka hasara ya asilimia mia moja katika maeneo yaliyoathirika. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imechukuwa juhudi zifuatazo katika kuwasaidia wananchi hawa;

Kufanya utafiti wa kujua aina ya nzi wanaoshambulia na kuathirika matunda pamoja na mitego ya kuwanasa kwa kuwapatia taaluma wakulima juu ya udhibiti wa wadudu hawarabifu wa zao la tungule, sambamba na kuwahamasisha wafanya biashara kuleta mitego ya kuwanasa vipepeo na dawa za kuulia mafunza.

Kumarisha ukaguzi wa mazao katika bandari ya viwanja vya vindege kwa lengo la kuzuia waingiaji zaidi ya wadudu waharibifu wa mazao na mimea. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri, amekiri kwamba wadudu hawa wapo na wapo kwa muda mrefu sana hususan wadudu wa embe.

Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani kabambe wa kulimaliza tatizo hili kwa vile limekuwepo kwa muda mrefu sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, Wizara yangu kwa sasa hivi ina lita 120 za dawa hiyo ambayo wameanza kuigawa katika wilaya 6; kwa Unguja wilaya 6, lakini kati wataanza kesho na hivi sasa ninavyoengea tayari wamo katika kazi ya kufanya kazi hiyo.

Vile vile, kutokana na bajeti yetu kwamba inachelewa labda kuingia tumebuni ubunifu mpya wa kutafuta chupa zile za *drop* na kutengeneza mitego kwa ajili ya kuwatilia dawa hiyo. Kwa hiyo, tunaendelea kuhangaikia tatizo hili tuhakikishe linaondoka kwa Zanzibar hii.

Nam. 166

Kuimarisha kwa Kilimo cha Viungo

Mhe. Hidaya Ali Makame: Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa watu wengi wanaonesha dhamira ya kulima kwa kasi kilimo cha viungo kama kungumanga, hiliki na vyenginevyo.

Je, serikali ina mpango gani katika kuwatafutia masoko ya nje na ndani wakulima ili kunufaika na kilimo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake namba 166 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Mifugo na uvuvi kupitia wataalamu wake wa Idara ya Misitu imekuwa ikishajihisha wakulima kulima mazao ya matunda na viungo kwa lengo la kujiongezea kipato na tija. Aidha, wizara imewashajihisha wafanyabishara wa mazao wa viungo kununua mazao hayo kwa wakulima na kuuza soko la ndani kusafirisha nje ya nchi. Lakini kwa bahati mbaya uzalishaji wa mazao ya viungo ni mdogo hata hautoshelezi soko la ndani isipokuwa karafuu tu. Hata hivyo, napenda kumuhakikishia Mhe. Mussa Foum Mussa, kwamba soko la ndani lipo zuri na zuri kama ifuatavyo:-

Bei ya kungumanga kilimo moja ni Sh. 35,000 - 45,000, Vanila kilo moja sh. 50,000 - 70,000 na Hiliki kilo Sh. 10,000 mpaka Sh. 40,000.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri, kama alivyotwambia kwamba zao la viungo kwa sasa halijakuwa na soko hapa ndani yaani Zanzibar.

(a) Je, kama serikali ikishirikiana na wizara imejipanga vipi katika kuliimarisha hili soko na je, wamejipanga vipi kwa hawa wakulima kuwapa moyo zaidi ili waweze kukiendeleza hichi kilimo chao.

(b) Je, Wizara imejipanga vipi kwa hichi Chuo cha kilimo ambacho kama mwazo ndio ambao ni waanzilishi waliyoianzisha hii biashara ya viungu kama kungumanga, hiliki na vyenginevyo kuipa eneo zaidi ili iwezwe kuendelezwa biashara hii kwa wale wanafunzi

ambayo wanaingia pale chuoni ili waweze kuimairisha huko mitaani wanaporudi katika mafunzo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

(a) Mhe. Spika, katika jibu langu mama nilisema kwamba soko humu ndani lipo vizuri sana. Isipokuwa uzalishaji bado ni mdogo, kwa hivyo, tunaendelea kuwashajihisha wakulima kupanda mazao ya viungo.

(b) Linasema kwamba wanahitaji sehemu zaidi ya kupandisha mashamba ya viungo. Labda nimwambie chuo chetu cha Kizimbani kina eneo kubwa sana sana. Kwa hivyo, ni kuomba tu kwa Mkurugenzi na wanaweza wakapandisha viungo vya aina yoyote kwa sababu pale ni zaidi wamepandisha mihogo. Kwa hivyo, nafasi ipo kubwa sana kwa Chuo cha Kizimbani.

Mhe. Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba vile vile kujibu suala la soko la mazao la viungo.

Mhe. Spika, ni kweli soko la ndani lipo kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ndani.Lakini ili tuweze kujibu suala la soko la viungo lazima tutafute wawekezaji ambao watatuletea hapa viwanda vya kutengeneza viungo, kwa mfano kufanya yale masala zile za kupikia vyakula na vitu vyengine muhimu. Kwa hivyo, sasa hivi serikali iko mbioni kutafuta wawezekezaji kwa ajili ya kuja kuweka viwanda vya kuja kupengeneza viungo lakini katika unga.

Pamoja na hayo Mhe. Spika, Kiwanda cha Makonyo kilichopo Pemba na shamba la Makonyo lilioko Pemba litasaidia vile vile kuongeza kuwasaidia wakulima kupata vile vile soko, kwa sababu kiwanda kile cha makonyo kikifanya kazi kitaweza kununua baadhi ya viungo kutoka katika mashamba ya wakulima na kuweza kuyatengeneza na kufanya mambo mbali mbali ambayo yanatakiwa yauzwe nje. Siri ya soko ni kutafuta wawekezaji wa kuweza kutengeneza viwanda vyetu. Mkakati huo upo Mhe. Spika, na serikali imejiandaa vizuri sana. Soko la ndani bado halitoshi, kilimo kinachozalishwa ni kidogo sana, tuzalishe kwa wingi kwa ajili ya kuweza kukidhi soko la nje.

Mfano hivi leo tani 10,000 za pilipili manga zinatakiwa nje, hakuna mtu ambaye anaweza akatupa tani 10,000 za pilipili, kama yupo sasa hivi tunamuomba afike *ZSTC* kwa tuweze kuzisafirisha kwa wateja ambao tunao mikoni mwetu. (*Makofi*)

Mhe. Simai Mohamed Said:

(a) Mhe.Spika, kwa kuwa tunatambua kwamba katika masuala ya kulimo kuna *food crops* na *cash crops* na sisi kwa upande wetu wa Mkoa wa kusini Zanzibar pamoja na wilaya ya kati tumekuwa na wakulima wengi ambao wamekuwa wanalima mazao ya kula kama mboga mboga, lakini wameshindwa hasa katika jimbo langu la Tunguu katika maeneo ya Dunga pamoja na Tunguu, Binguni, Mtakuja, Bungi, Kipele, Kikungwi kote, ni juhudi gani za serikali watazifanya za makusudi ili kuweza kuwasaidia wakulima kuwaunganisha katika kuweza kuzalisha mboga mboga pamoja na kuonesha na soko ambalo lililokuwepo la utalii pamoja na wananchi kwa ujumla.

(b) Tumeona kwamba kila ***Azam*** *Sealink* inapofika hapa Zanzibar tumeona jinsi gani watu kutoka kisiwa cha pili Pemba wanakuja na mikungu ya ndizi, lakini ni dhahiri kwamba katika kisiwa cha Pemba wana uwezo mkubwa wa kuzalisha vyakula kwa sababu ardhi yao ni nzuri tunaweza tukawaunganisha pamoja na soko la Unguja kuliko kuhakikisha kwamba hizi mboga mboga na haya matunda mengine yanatoka Tanzania Bara. Ni juhudi gani ambazo serikai wanazifanya ili kuwasaidia wakulima wetu wa Pemba kuwaunga na soko la Unguja la wananchi pamoja na soko la utalii la Maruhubi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kwanza serikali katika kuwasaidia wakulima kupitia wizara ina mpango wa kutoa taaluma kwa wakulima wa mboga mboga na wakulima wengine na kazi hii imekuwa ikifanyika kwa muda mrefu.Lakini vile vile kupitia Wizara ya Kilimo ina mpango wa kutafuta mbegu bora ambazo zina uzalishaji mzuri na zinastahimili magonjwa na wadudu. Lakini pamoja na hayo inasaidia wakulima katika kuwahamasisha Pembejeo za kisasa ikiwemo mbolea za samadi, madawa ya kuulia wadudu na magonja, lakini vile vile kuwashajihisha wakulima kuunda vikundi vyao (*Associations*) kwa ajili ya kuwapatia ya kuwarahisishia upatikanaji wa masoko.

Lakini pamoja na hayo, ziko fursa mbali mbali za kupata mitaji kupitia Wizara ya Uwezeshaji ambazo wakulima nao wanaweza kupata fursa hivi kwa ajili ya kupata mitaji ya kuendeleza mazao yao. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali umekwisha, lakini kama mtakavyokuwa mnakumbuka kwamba kipindi kilichopita kwa kiasi kikubwa sana maswali tulikuwa tumeyanyima fursa ya kujibiwa. Kwa hivyo, nakuombeni sasa kwa kuwa muda umekwishamalizika lakini kuna swali kwa Wizara ya Afya limebaki, kwa hiyo, naomba tuchukuwe nafasi hii tumalize hili swali baada ya hapo tuende kwenye shughuli zinazoendelea. (*Makofi*)

Nam. 56

Ujenzi wa Nyumba ya Daktari Kituo cha Afya Finya

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Aliuliza:-

Naipongeza sana serikali katika jitihada zake kuhakikisha kuwa Jimbo la Mgogoni lililopo Wilaya ya Wete kwa kujenga vituo vitatu vidogo vya afya na kituo kimoja kikubwa ambacho pia hutoa huduma ya mama na mtoto na kujifungulia akina mama wajawazito katika Shehia ya Finya.

Je, wizara yako ina mpango gani wa kujenga nyumba hiyo ya daktari ili kupunguza usumbufu kwa madaktari na wagonjwa na lini itajengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar suala lake Nam. 56 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza wakati nikijibu suala Nam. 18 katika kikao cha Baraza lililopita kwamba sera ya afya ya mwaka 2011 imeeleza bayana kuhusu umuhimu wa kujenga nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya vituo vya afya.

Ni kweli serikali ina nia ya kuondosha kabisa usumbufu kwa madaktari ya wafanyakazi wa hospitali na vituo vya afya. Wizara imekuwa ikiwashajihisha wananchi na viongozi kujenga nyumba za wafanyakazi baada ya kujenga vituo vipya vya afya.

Mhe. Spika, wizara iko tayari kutoa mashirikiano ya kutosha kwa Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wenye nia na dhamira ya dhati ya kujenga nyumba za wafanyakazi katika vituo na hospitali zetu. Kwa sasa wizara haina mpango wa ujenzi wa nyumba, lakini hali ya fedha itakaporuhusu haitasita kujenga nyumba hizo. Ahsante.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, pamoja na kuwa haiko tayari kujenga nyumba hizo sasa hivi, lakini lile lengo halijafikiwa la kuweza kuweka kituo kama kile cha pale cha Finya kwamba akina mama waweze kujifungulia pale. Lakini mimi niseme kwamba kwa kushirikiana mimi mwenyewe pamoja na wananchi sisi tuko tayari na hatua tumeshaanza kuzichukuwa za kuwa na kiwanja. Je, ni kiasi gani nguvu na wao pamoja na kutafuta njia yoyote ile ili kuweza kutusaidia ya kujenga nyumba hiyo ya daktari.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba anisaidie kueleza tena, sikumfahamu.

(Hapa Mhe. Spika, kaendelea mbele)

Nam. 132

Tatizo la Matumizi ya Condom

Mhe. Ali Khamis Bakar: Aliuliza:-
Mhe. Spika, afya ni sehemu ya maisha ya binaadamu ambayo sasa kuna ongezeko kubwa la matumizi ya kondom jambo ambalo linaongeza hali ya kuchochea ngono na kuwafanya vijana waharibike zaidi.

Je, ni hatua gani za sheria zimechukuliwa kutokomeza matumizi ya kondom.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi Mhe. Ali Khamis Bakari wa Tumbe swali lake Nam. 123 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, utumiaji wa kondom ni moja ya njia inayokubalika kitaifa na kimataifa katika kujikinga na maradhi yanayoambukiza kwa kujamiana kwa mfano UKIMWI, Kaswende, Kisonono na kadhalika. Na pia ni moja ya njia ya kupanga uzazi ulio bora. Tafiti zinaonesha kuwa kama kondom inatumika ipasavyo ina uwezo mzuri wa kuzuia maambukizi ya *VVU* kwa asilimia 98.

Mhe. Spika, kuna mazingira mengi ambayo yanafanya kondom ziendelee kutumika. Kuna baadhi ya wana ndoa ambao mmoja anaishi na maambukizo na mwengine hana maambukizo. Ili watu hawa waendelee kuishi na kuitunza ndoa yao vizuri ni lazima mmoja atumie njia ya kinga ili kumkinga mwenzake. Kwa sababu hiyo na nyingi nyengine matumizi ya kondom yameendelea kusisitizwa kama ni njia moja kuu ya kujikinga na maambukizi ya *VVU*.

Mhe. Spika, ipo haja ya kuimarisha maadili ya vijana ikiwemo kuwapatia elimu ya Dini ambayo itawajenga katika desturi zinazokubalika kimila na hili ni jukumu letu sote kuanzia mtu mmoja mmoja hadi jamii kwa ujumla.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Ali Khamis Bakari, kwa swali la nyongeza.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Mhe. Spika, ahsante sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yako muzuri, lakini ninapenda kukuuliza swali jengine la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mara nyingi serikali inawachukulia hatua wafanyabiashara ambao wanaleta bidhaa zinazopelekea majanga kwa jamii. Je, ni hatua gani zitachukuliwa dhidi yao hawa ambao wanaingiza hizi kondom.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kweli serikali haina nia wala haitofanya kuwachukulia hatua wanaoingiza kondom wala wanaotumia kondom, kwa sababu lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wananusurika na maambukizi mabaya ya *VVU* pamoja na maradhi yanayoambukizwa kwa njia ya kujamiana.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri, maswali yamekwisha na muda ulikuwa umeshamalizika muda wa maswali.

Waheshimiwa Wajumbe, kuna wageni. Wageni wetu leo ni wageni wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Paje ni viongozi wa Kijiji cha Paje. Jumla yao ni watu wanane wakiongozwa na Sheha wa Paje Bwana Haji Kitete, naomba musimame musalimie. *(Makofi)*

Ahsanten. Karibuni sana kwenye ukumbi wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa).

KUWEKA KANDO KANUNI YA 42

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, naomba ninyanyuke kwa Kanuni ya 42 ili basi tuweke kando kazi zetu ambazo tumejipangia na kuona

kuzungumza hoja ya dharura angalau kwa saa moja ili kuonesha jinsi gani mambo haya nitakayoeleza tuweze kwenda mbele.

Mhe. Spika, kama...

Mhe. Spika: Ahsante sana na nimeruhusu hilo lifanyike. Lakini kabla halijafanyika sasa namuomba Mhe. Naibu Spika, aje achukue hii nafasi halafu baada ya hapo utaendelea. Mhe. Naibu Spika, tafadhali.

(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mohamed Said Mohamed, endelea.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, kabla ya Mhe. Spika, kuondoka kwenye kiti chake, niliomba nitumie Kanuni ya 42 ili tujadili jambo la dharura na tuweke kando zetu za kila siku, ili tujadili jambo hili ambalo nitalizungumzia.

Mhe. Naibu Spika, kama unavyokumbuka kwamba mnamo tarehe 10 ya Septemba, 2016, Watanzania tulipata taarifa ya janga la tetemeko la ardhi lililowatokea Watanzania wenzetu huko Bukoba Mkoani Kagera. Tokeo hilo la kusikitisha liliacha athari kubwa kwa vifo, majeruhi na uharibifu mkubwa wa mali za wananchi wa huko. Na kwamba hadi kufikia tarehe 16 ya Septemba mwaka huu idadi ya vifo vilikuwa ni 17, nyumba zilizoanguka zilikuwa ni 840 na zile zilizopata maharibiko ni 1,264 ambapo majengo mengine 44 taasisi za umma nayo yaliathirika. Ukiachilia mbali mashamba mbali mbali yaliyoharibika na kupata athari kubwa.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili lililowapata Watanzania wenzetu nasi limetugusa mno kwa kuamini kwamba furaha yao ndiyo furaha yetu, lakini vile vile huzuni na msiba ni yetu sote. Hivyo, sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar tunawapa pole sana wenzetu hao kwa maafa yaliyowafika kama Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais alivyozungumza mwanzoni. Tukiwakilisha kwamba tupo pamoja nao katika janga hili kubwa huku tukiwaombea Mwenyezi Mungu awape subra na uvumilivu wafiwa wote waliopata athari kubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kujadili hili tuendelee kulijadili ili tuweze kuweka kando hizi kazi zetu za siku, ningeomba sasa niseme tuweze kuchangia hoja hii ili basi tuweze kutoa angalau posho letu la siku moja Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukawachangia ndugu zetu wale tukaonesha jinsi gani ambapo

Watanzania wenzetu wamepatwa na janga letu kubwa. Lakini vile vile tukumbuke na sisi tulipata janga kubwa la meli ya *Spice Islander* tulichangiwa na ndugu na jamaa wa sehemu mbali mbali. Hivyo, tuoneshe Baraza hili masikitiko yetu makubwa kuweza kukata posho angalau ya siku moja na tuweze kulichangia suala hili. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae Mhe. Mohamed Said Mohamed, ametoa hoja ambayo kwa dharura aliyoisema ninafikiria ni muhimu sana kwetu sisi, lakini ni wajibu kuuliza kama hoja hiyo imekubaliwa na kama imekubaliwa, mimi ninafikiri kutokana na shughuli zetu nyengine basi tufanye dharura hiyo tuikubali, nitauliza baadae tutaendelea na shughuli zetu nyengine.

Waheshimiwa Wajumbe, hoja iliyotolewa na Mhe. Mohamed Said Mohamed, ninauliza.Waheshimiwa Wajumbe, tunaijadili au tunaulizana ikisha tunaendelea na shughuli nyengine.

Naam Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nimetoa hoja na hoja imeungwa mkono. Hivyo, kwa Kanuni zetu tunapaswa kuijadili angalau saa moja au nusu saa kwa maelekezo ya kiti chako. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tuijadili lakini mimi ninafikiria nafasi hiyo nimepewa mimi kama nitaona ina ulazima wa kuijadili ijadiliwe. Kwa hivyo, mimi nitatoa ruhusa kwa watu wasiozidi watatu, kwa sababu tuna shughuli nyingi Waheshimiwa Wajumbe, tukae tukijua, tuna mengine mengi ya kufanya na hoja hii tunafahamu ni muhimu. Kwa hivyo, nitatoa nafasi, fursa kwa watu watatu tuzungumze kwa dakika tano tano zisizozidi zaidi ya dakika tano na baadae tutaulizana na baadae tutaendelea na shughuli nyengine. Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii. Pia, nikushukuru wewe kwa kunipa kuchagia kidogo hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed, ambayo tunaiunga mkono sana hoja hii.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, wenzetu wa Mkoa wa Kagera na zaidi katika mji wa Bukoba na miji mengine ya jirani wamepata madhara makubwa kutokana

na tetemeko la ardhi. Sisi kama Watanzania hatuna budi kuwaunga mkono kwa kushirikiana nao katika janga hili kwa kutoa kidogo ambacho tunacho.

Sasa mimi Mhe. Naibu Spika, naunga mkono sana lile wazo la Mhe. Mohamed Said Mohamed, la kuchangia posho letu la siku moja. Lakini pia nilikuwa nifike mbali kidogo kwamba kutokana na hali ya Baraza kwamba ni dogo na pengine posho yao ni ndogo, basi sisi kwa sababu asilimia 90 nao humu ni Waheshimiwa Wawakilishi wa CCM. Basi tufanye maarifa na tukubaliane kwamba tuwaongezee juu walau tufike shilingi milioni ishirini kwa umoja wetu.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa ninataka kusema hayo.

Mhe. Naibu Spika: Ninakushukuru Mhe. Machano. Sasa ni Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa upande wangu hatuna budi kwa ujumla kutoa masikitiko ambayo mwenzetu aliyetoa hoja kaeleza vizuri Mhe. Mohamed Said Mohamed, lakini kiubinaadamu mtu anapokutwa na janga lazima yule aliyekuwa yupo vizuri kidogo atoe msaada wake wowote ule.

Mhe.Naibu Spika, mimi ninaunga mkono hoja ilivyoeleza kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutoe mchango wetu katika posho letu la siku moja ili kuona imani kwa wale wenzetu imewafikia. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, nina nyongeza kidogo. Kwa kuwa hili janga ni kubwa na wenzetu waliokutwa na janga hili, pia wanalia kwa mambo mbali mbali. Basi ukitoka ujumbe wowote kwenda kule angalau na baadhi ya Wawakilishi nao washirikishwe kwenda kuupeleka msaada ule ili itakuwa kama ni imani tumeonesha kuwa tupo pamoja na wenzetu waliokutwa na maafa hayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi baada ya hayo sina pingamizi, naomba posho la siku moja likatwe lakini naongezea maneno ya Mhe. Machano Othman Said, angalau tujipige pige posho letu Wawakilishi kidogo sana la siku moja, lakini twende mbio tufanye kila mbinu Chama cha Mapinduzi na wenzetu waliokuwa sio wa Chama cha Mapinduzi ambao wamo humu pia watoe msaada zaidi kidogo tuhakikishe kwamba tunafikia shilingi milioni ishirini au zaidi iwe kama ni sauti ya Wajumbe wote wa vyama vyote tuliokuwemo humu. (*Makofi*)

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wamemalizika wachangiaji. Mhe. Shamata Shaame Khamis.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kupata fursa ya kuweza kulichangia hili ambalo lipo mezani hivi sasa.

Mimi kwa upande wangu Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba tatizo limetokea au majanga yametokea kwa ndugu zetu wa Mkoa wa Kagera. Lakini pia naomba nichukue fursa ya kusema kwamba michango mbali mbali kweli inahitajika katika maeneo yale kwenye kuwasaidia ndugu zetu ambao wamefikwa na majanga hayo.

Lakini mimi ningeshauri kwamba katika kulifanikisha hili vyovyote vile ambavyo itakuwa ningeshauri kwamba tungeweza kuona kile ambacho kitakachopatikana kwa mujibu wa wingi wetu au idadi yetu, basi ninadhani kwamba tungetafuta namna ya kuona kuwa tuingie na upande mwengine kuwahamasisha angalau na wafanyabiashara kwenye majimbo yetu ili nao kuweza kuona tunaongeza nguvu zaidi, lakini kile ambacho kwa kweli kimepangwa kwa ajili ya kutokana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, basi tuweze kufikia maamuzi kwamba kipelekwe hicho hicho na badala yake tuwe tayari kuwahamasisha watu wetu ili kuweza kuona kwamba na wao mchango wao unahitajika kwa nguvu zaidi ili kuwasaidia, kwa sababu mimi ninadhani vyovyote itakavyokuwa hata tukichangia zaidi basi bado mahitaji ni makubwa mno kutokana na lililotokea.

Sasa niombe tu kwamba mimi niunge mkono kuwa hili tufanye lakini tusitafute tena namna nyengine na badala yake hicho ambacho kwa kweli kimepangwa na kimeshapatikana, basi tuweze kuharakishwa na kifike kwa wakati ili kiweze kukidhi mahitaji kwa muda ambao labda ni muafaka zaidi kulikoni kutafuta tena muda au kutafuta namna nyengine ambayo pengine inaweza ikachukua muda mrefu zaidi.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Shamata. Sasa nilikuwa naomba Mhe. Mohamed Said Mohamed, atoe hoja.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuniona.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niwatambue wachangiaji wa hoja hii. Waliochangia ni Mhe. Machano Othman Said, Mhe.Ali Suleiman Ali na Mhe. Shamata Shaame Khamis.

Niwashukuru wote lakini niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kuiunga mkono hoja hii ili kuona uzito wa wenzetu uliotokea. Baada ya hayo ningeomba kutoa maazimio mawili ili kuweza kumaliza hoja yetu.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya mwanzo ni kuazimia basi Baraza lako Tukufu:-

1. Tukatwe posho letu la siku moja ili kuwachangia waathirika hao, na

2. Tuangalie kwenye mfuko wetu wa Chama kama zisipungue mchango wetu zaidi ya shilingi milioni ishirini ili ku-*support* janga hili kubwa ambalo limetokea.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na Mjumbe; ametoa hoja mbili na nitaziuliza kwa pamoja kwa sababu zote zinahusiana na jambo moja. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubali na hoja zote mbili wanyooshe mikono, wale wanaokataa.

Waheshimiwa Wajumbe, hoja imepita. Mhe. Mjumbe, tunakushukuru sana kwa hoja yako na ni matarajio yetu sasa watendaji wetu wataweza kuendelea kutekeleza hilo ambalo tumelifanyia maamuzi hapa.

Tunaendelea. Katibu.

HOJA YA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar ya Mwaka 2016

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar ya mwaka 2016 (*The Zanzibar Institute for Education Act 2016)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nitanguliza shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kukutana leo hii katika Mkutano huu wa Tatu tukiwa wa wazima wa afya na salama na kuendelea na kazi hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Pili, nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii wa kuwasilisha Mswada mbele ya Baraza lako Tukufu kwa niaba ya wizara yangu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu Mswada wa Sheria ujulikanao kama *The Zanzibar Institute for Education Act 2016*, wenye lengo la kutunga sheria ya kuanzisha taasisi ya elimu ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo kwa madhumuni ya kuimarisha mitaala na uthibiti wake ili kuleta ufanisi mzuri katika sekta ya elimu.

Mhe. Naibu Spika, natoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Dimani, kwa kuujadili kwa kina Mswada huu na kutoa ushauri wao.Vile vile, ninawashukuru wadau mbali mbali mbali ambao kwa nyakati tofauti wametoa mapendekezo yao kwa lengo la kuimarisha Mswada huu.

Vile vile, ninamshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wake kwa ushirikiano wao mkubwa waliotuonesha wakati wa maandalizi wa Mswada huu. Ninapenda kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba Mswada huu umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii pamoja na wadau wengine ambao wamesaidia sana katika kuimarisha Mswada huu.

Chimbuko la Mswada:

Mhe. Naibu Spika, chimbuko la Mswada huu ni Sera ya Elimu ya mwaka 2016 ambayo imeelekeza kuanzishwa kwa chombo cha kuratibu na kusimamia mitaala na utafiti wa elimu. Aidha, kutokuwepo kwa chombo chenye mamlaka ya kisheria kumesababisha kutokuwepo na utaratibu na usimamizi mzuri wa mitaala na utafiti wa kielimu.

Katika mwaka 1982, aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Marehemu Mhe. Mzee Aboud Jumbe Mwinyi aliunda tume ya kupitia mfumo wa elimu wa Zanzibar. Ripoti ya tume hiyo ilipendekeza kwamba, ili shughuli za mitaala za utafiti wa elimu ziweze kuendeshwa kitaaluma na kwa uhakika, iundwe taasisi ya elimu ambayo itaratibu, kuziendesha na kusimamia shughuli za ukuzaji mitaala na utafiti wa elimu.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa matakwa ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ni kuwa, kila nchi mwanachama iwe na chombo maalum chenye sheria, kwa ajili ya kuandaa na kudhibiti mitaala, kutayarisha vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kufanya utafiti wa kielimu. Hivyo, ni busara kuwa na sheria ya chombo cha kitaifa kinachoshughulikia mitaala, kuwepo kwa chombo hicho kitakachoanzishwa kisheria, kitawezesha kujitegemea na kuwa na vyonzo mbali mbali vya kupata fedha kwa kufanya utafiti na ukuzaji mitaala, kwa kuuza vifaa vya kufundishia, kutoa mafunzo na kutoa ushauri wa kitaalamu unaohusiana na utekelezaji wa mitaala.

Athari zitakazojitokeza iwapo chombo hicho hakitaanzishwa, ni pamoja na kutokuwepo na ufanisi katika ukuzaji mitaala, utekelezaji mitaala na utafiti wa kielimu endelevu. Aidha, kutokuwepo kwa taasisi ya ukuzaji wa mitaala na utafiti unaotambulika kisheria, unapunguza kasi ya mafanikio katika ukuzaji mitaala na utafiti wa kielimu hapa Zanzibar, na hivyo kudumaza michango ya mitaala na utafiti katika maendeleo ya ubora wa elimu na taifa kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, hali ilivyosasa na uzoefu wa nchi nyengine. Hivi sasa ukuzaji mitaala katika sekta ya elimu hapa Zanzibar, unatekelezwa na kusimamiwa na Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, iliyoundwa kutokana na matakwa ya Sera ya Elimu ya mwaka 2006. Taasisi inafanyakazi zake bila ya kuwa na mamlaka ya kisheria ya kusimamia na kuratibu ukuzaji mitaala na utafiti. Hali hiyo inapelekea baadhi ya skuli za binafsi kutumia mitaala kinyume na taratibu zilizowekwa na wizara, huu ni upungufu mkubwa uliopo katika mfumo wa elimu wa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, uzoefu wa taasisi za nchi nyengine kama *Kenya East African Curriculum Development* (*KEACD*) ya Kenya, *National Curriculum Development Centre (NCDC*) ya Uganda, *Rwanda Education Boards (REB)* ya *Rwanda, Tanzania Institute of Education (TIE)* ya *Tanzania Bara, Malawi Institute of Education (MIE)* ya *Malawi, Mauritius Institute of Education (MIE)* ya *Mauritius,* na *National Institute of Education (NIE)* ya *Singapore*, inaonesha kuwa taasisi hizo zina utaratibu mzuri wenye ufanisi, kwa vile zimeanzishwa kwa sheria maalum.

Mambo Muhimu katika Mswada:

Mhe. Naibu Spika, mambo muhimu yaliyosingatiwa katika mswada huu ni kama yafuatavyo.

1. Kuanzisha Taasisi ya Elimu kwa ajili ya ukuzaji mitaala, kuandaa vifaa vya kufundishia, kusimamia na kuratibu shughuli zote za utafiti wa elimu nchini.
2. Kujenga uwezo wa wataalamu na miundombinu katika fani za ukuzaji mitaala na utafiti.
3. Kuweka wazi kazi na majukumu ya taasisi bodi ya ushauri na Mkurugenzi wa Taasisi.
4. Kuweka mfuko wa utawala na usimamizi wa fedha na
5. Kuweka taratibu za kuwezesha sheria kutekelezwa.

Ushirikishwaji wa Wadau:

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umetayarishwa kwa kuwashirikisha wadau mbali mbali, ikiwemo kamati ya uongozi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Kamati Tendaji ya Elimu, Kamati ya Makatibu Wakuu, Baraza la Mapinduzi, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, wadau wa elimu na wastaafu wa elimu na maoni yao yote yamezingatiwa.

Matokeo ya Sheria Inayopendekezwa Kutungwa:
Mhe. Naibu Spika, matokeo ya sheria inayopendekezwa kutungwa ni kama ifuatavyo.

1. Kuongezeka kwa ufanisi katika utekelezaji wa mitaala na utafiti wa elimu kulingana na mahitaji ya soko.
2. Kuwepo mfumo madhubuti wa kusimamia shughuli za mitaala, utafiti wa elimu na ubora wa elimu na
3. Kuimarika kwa ushirikiano kati ya taasisi, mashirika na wadau wengine wanaoshughulikia mitaala na utafiti wa elimu ndani na nje ya nchi.

Mahitaji ya Rasilimali:

Mhe. Naibu Spika, jumla ya fedha zisizopungua shilingi milioni 10, zitahitajika kwa ajili ya kuandaa sheria, kuchapisha, kusambaza, kutayarisha kanuni na

kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria hii. Fedha hizo tayari zimetengwa katika bajeti ya taasisi ya elimu ya mwaka wa fedha 2016/2017.

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar hivi sasa ina jumla ya watumishi 23, miongoni mwa watumishi hao, 16 ni wa kada ya taaluma na watumishi 7 ni wa kada mbali mbali. Ili kuweza kufanyakazi ipasavyo, watumishi wapya 98 wanahitajika, wakiwemo 48 wa kada ya taalamu na 50 wa kada mbali mbali. Pia, miundombinu kama vile majengo ya ofisi, maabara, maktaba na karakana zinahitaji kujengwa.

Mpango wa Utekelezaji:

Mhe. Naibu Spika, mpango wa utekelezaji utakuwa kama ifuatavyo.

1. Kuwasilisha mswada katika Baraza la Wawakilishi, ambapo tunafanya katika mwezi wa Septemba 2016.
2. Kuchapisha na kusambaza vitabu vya sheria katika mwezi wa Januari 2017.
3. Kutunga kanuni mwezi wa Februari 2017 na
4. Kuelimisha jamii kuhusu sheria katika mwezi wa Machi 2017.

Maudhui ya Mswada:

Mhe. Naibu Spika, mswada huu una madhumuni makubwa yafuatayo.

1. Kuainisha masuala ya kisheria yanayohusiana na mitaala katika sheria hii, ambayo itaiongoza Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, kama ilivyo kwa vyombo vyengine vinavyosimamia mambo anayohusiana na mitaala. Pendekezo hili litawezesha kueleweka kwa majukumu ya taasisi na mipaka yake.
2. Kuimarisha usimamizi wa mitaala katika skuli za serikali na binafsi, ili kudhibiti mitaala isiyoruhusiwa.
3. Kuimarisha majukumu na kuifanya taasisi kuwa chombo huru kinachoweza kutekeleza majukumu yake ya ukuzaji mitaala na kufanya utafiti kwa ufanisi na
4. Kurekebisha mapungufu mbali mbali yatakayojitokeza katika utekelezaji wa mitaala.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, ili taasisi iweze kuishauri vizuri serikali kwa kupitia bodi yake juu ya mambo yanayohusiana na mitaala, mswada huu unapendekeza kuwepo bodi ya taasisi ambayo itakuwa na wajumbe wenye dhamana zenyekuendana na mitaala. Wajumbe wenyewe ni:-

1. Mkurugenzi wa Taasisi ambaye ndiye mwenye dhamana ya kuandaa mtaala.
2. Mkurugenzi Mkuu wa Elimu mwenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa mitaala, Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani Mwenye dhamana ya kupima viwango vya kujifunza kwa wanafunzi.

Vile vile, mwakilishi kutoka Baraza la Watu Wenye Ulemavu, ili kuhakikisha kwamba mitaala inazingatia mahitaji maalum. Pia, Wakili wa serikali ili kuhakikisha haki miliki inazingatiwa katika uandishi wa vitabu. Pia, Mwakilishi kutoka Jumuiya ya skuli binafsi, ili kuhakikisha upimaji sahihi wa mitaala uliothibitishwa na kuruhusiwa na serikali na vile vile, Mwakilishi kutoka Jumuiya ya Waajiri kwa lengo la kushauri juu ya taaluma inayofaa kulingana na mahitaji ya jamii na soko la ajira.

Majukumu ya Taasisi ya Elimu Zanzibar:

Mhe. Naibu Spika, Taasisi ya Elimu ya Zanzibar imepewa dhamana ya kubuni na kuandaa mitaala na vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kuanzia ngazi ya maandalizi hadi vyuo vya ualimu. Taasisi hii ilianzishwa mwaka 2011 kutokana na kutenganishwa kwa iliyokuwa Idara ya Mitaala na Mitihani. Aidha, misingi ya taasisi hii ni kama zifuatazo.

1. Kuandaa Mitaala na mihutasari kupitia *panel* za masomo.
2. Kufanya utafiti majaribio na kutathmini vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ili kufanya ufundishaji uwe fanisi na unaofaa kulingana na mahitaji ya nchi.
3. Kuratibu uandaaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
4. Kutoa mafunzo kwa walimu na wahusika wa elimu juu ya majaribio na utekelezaji wa programu mpya za kielimu.
5. Kushirikiana na taasisi nyengine za elimu, idara, wizara, mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi katika mambo yanayohusiana na mitaala.
6. Kushiriki katika uandaaji wa mitihani na tathmini ya elimu, ili kuhakikisha mitihani inaendana na mahitaji ya mitaala.
7. Kutoa ushauri unaohusiana na sera ya uandaaji na mapitio ya mitaala na
8. Ufuatiliaji na upitiaji wa utekelezaji wa mitaala katika skuli na vyuo vya ualimu.

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya taasisi hii yatatekelezwa kupitia idara zifuatazo.

1. Idara ya Kubuni na Kuandaa Mitaala.
2. Idara ya Kubuni na Kuandaa Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia.
3. Idara ya Utafiti wa Kielimu na Uendelezaji wa Utaalamu na
4. Idara ya Fedha na Utawala.

Vile vile, taasisi ya elimu ina ofisi ya uratibu Pemba.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umegawika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya Kwanza, ni sehemu yenye kifungu cha kwanza, kifungu cha pili na kifungu cha tatu, vinahusu masuala ya utangulizi kama vile jina na tarehe ya kuanza kutumika, ukomo na ufafanuzi.

Sehemu ya Pili, inaelezea uanzishwaji wa Taasisi ya Elimu, uanzishwaji wa bodi, kazi za bodi, uteuzi wa Mkurugenzi na uwezo wa waziri kutoa maelekezo.

Sehemu ya Tatu, inazungumzia masharti ya kifedha ukijumuisha fedha na rasilimali za taasisi, pamoja na kutumika kwa sheria ya fedha za umma na sheria nyengine za fedha, kwa mambo yanayohusiana na matumizi ya fedha za taasisi.

Sehemu ya Nne, inazungumzia masharti mengineyo ambayo imejumuisha uwezo wa waziri kutunga kanuni. Mwisho, ni jaduweli ambalo limeelezea masharti yanayohusiana na utaratibu wa uendeshaji wa vikao vya bodi.

Pendekezo

Mhe. Naibu Spika, Baraza lako tukufu linaombwa likubali Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo itungwe.

Hitimisho

Mhe. Naibu Spika, mtaala ni kitu muhimu sana kwa ajili ya kutoa mwelekeo wa jamii na taaluma kwa jumla. Kwa hivyo, ni muhimu kuwa na mfumo huu wa kisheria utakaosaidia kuleta ufanisi na utekelezaji mahiri wa majukumu ya taasisi.

Madhumuni Makuu ya Taasisi ni kuandaa mitaala na vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kuanzia ngazi ya maandalizi mpaka ngazi ya vyuo vya ualimu, pamoja na kufanya utafiti wa kielimu. Dhana ya mtaala inajumuisha uzoefu anaoupata mwanafunzi ndani ya maisha ya skuli, ukuzaji mitaala unaohusiana na kuandaa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, mpangilio wa ufundishaji na ujifunzaji, ambao unaakisi malengo ya kielimu yaliyokusudiwa. Kazi ya taasisi ya elimu ni kupanga mtiririko wa vitendo vya mwalimu na mwanafunzi katika mazingira ya kufundisha na kujifunza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi, waujadili mswada huu pamoja na marekebisho yake na hatimaye waukubali kuupitisha kuwa sheria.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Naibu Spika: Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea. Sasa hivi ni zamu ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, karibu Mwenyekiti.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Naibu Spika, ifuatayo ni hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, katika Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kutujaalia uzima na afya njema, iliyotuwezesha kukutana na kujadili Mswada huu muhimu wa kuanzisha Taasisi ya Elimu Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nitangulie kusema kuwa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, inaunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuleta Mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu, kwa madhumuni ya kuimarisha sekta ya elimu Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila endapo sitowashukuru wadau ambao Kamati yetu ilikutana nao kuujadili mswada huu kwa undani na

kutupatia maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yameisadia kamati kutoa mapendekezo muhimu katika marekebisho tuliyoyafanya.

Mhe. Naibu Spika, Taasisi inayoanzishwa itakua na jukumu la Kuandaa mitaala, vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kufanya tafiti za elimu zinazohusiana na maendeleo ya mitaala.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, inaishukuru sana Wizara ya Elimu kwa kuipatia fursa Kamati ya kwenda kujifunza katika Taasisi ya Elimu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Dar-es-salaam. Ziara hiyo ya kimafunzo imeisaidia sana Kamati kupata ufahamu mzuri wa Taasisi ya Elimu kama tunavyotaka kuanzisha hapa Zanzibar.

Madhumuni ya Mswada

Mhe. Naibu Spika, kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya uwasilishwaji mswada. Madhumuni ya Mswada huu ni kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, ambayo itakuwa ni Wakala wa Serikali. Taasisi itakuwa na jukumu la kuandaa mitaala, vifaa vya kufundishia, kufanya tafiti za elimu zinazohusiana na maendeleo ya mitaala na kuimarisha vifaa vya kujifunzia ili kuhakikisha utoaji wa elimu kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, Miongoni mwa mambo muhimu yaliyotajwa katika Mswada huu ni pamoja na suala la bodi ya ushauri iliyotajwa katika kifungu cha 6, kazi kubwa iliyotajwa itakuwa ni kushauri tu jambo ambalo kwa mtazamo wa kamati, ni vyema bodi hii tukaipa mamlaka ya kuamua katika baadhi ya mambo ambayo ni ya msingi katika uendeshaji wa taasisi hii.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijatoa mapendekezo ya Kamati kuhusiana na Mswada huu, naomba kwanza nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

1. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi -Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ame Haji Ali - Mjumbe
4. Mhe. Hidaya Ali Makame - Mjumbe
5. Mhe. Massoud Abrahman Massoud - Mjumbe
6. Mhe. Makame Said Juma - Mjumbe
7. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mjumbe
8. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe

9. Ndg. Aziza Waziri Kheir - Katibu
10. Ndg. Khamis Hamad Haji - Katibu

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, iliupitia mswada huu kwa makini na kufanya marekebisho kadhaa katika baadhi ya vipengele.

Maoni ya Kamati (Marekebisho)

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba uniruhusu nitoe maoni ya kamati. Aidha, naomba niwatanabahishe Waheshimiwa Wajumbe kuwa, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho na kamati, hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo hayo naomba muangalie katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe, tayari mmeshapatiwa.

Mhe. Naibu Spika, kamati inapendekeza kazi za taasisi kamati inapendekeza ziwe katika kifungu cha 5(1) kama ifuatavyo:

(2)Kuundwa kwa idara ndogo ndogo au vitengo vya taasisi husika ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi wa taasisi, Aidha, kamati inashauri taasisi iunde vitengo vidogo 2;

1. Kitengo cha Fedha, Mipango na Sheria.
2. Kitengo cha Utengene zaji Mitaala,vifaa vya kujifunzaia na kufundishia, vitabu vya kiadana Utafiti.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 2 cha Mswada huu kinachohusiana na matumizi, kamati imependekeza katika kifungu kidogo cha (b) mwishoni mwa kifungu hicho yaongezwe maneno “vya serikali na binafsi” ili kuweka bayana vyuo vinavyohusika na sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu pia inapendekeza katika Sehemu ya Pili ya mswada huu ambayo inahusiana na kuanzishwa na Uongozi wa Taasisi pamoja na kazi zake, kamati imetoa mapendekezo katika kifungu cha 4 kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 4(1) neno “Wakala”, kamati imeomba neno hili litolewe ufafanuzi wake, ili kamati iweze kujiridhisha, taasisi hii inaanzishwa na kuwa wakala na itaendeshwa vipi. Aidha, kamati imependekeza

kuwa taasisi hii itakapoanzishwa hata kama ni wakala wa serikali, lakini iwe na mamlaka katika baadhi ya maamuzi yake na iwe "*Semi-Autonomous*".

Mhe. Naibu Spika, kamati imependekeza hivyo ili taasisi hii iweze kujiendesha na kupiga hatua katika kukabiliana na changamoto za kiuendeshaji na kwenda sambamba na soko la Afrika ya Mashariki katika masuala ya kielimu.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inashauri kwamba Taasisi ya Elimu itakayoundwa haidhuru itakuwa chini ya wizara, lakini iwe na mamalaka katika baadhi ya mambo ambapo inaweza kufanya miradi midogo midogo bila kuingiliwa. Miradi ambayo huisaidia taasisi katika kutatua baadhi ya changamoto zake za kibajeti.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 5(j) Kamati yetu inapendekeza neno "uboreshaji" liliopo baina ya neno "na" na "wa" linarekebishwa na lisomeke "uandaaji". Pia, yanaongezwa maneno "na visaidizi vyake" mwishoni mwa sentensi ya kifungu hiki. Sababu ya mapendekezo hayo ni kuhakikisha kuwa Taasisi inafanya kazi kwa ufanisi ya kuhakikisha upatikanaji wa mitaala iliyo bora pamoja na zana bora za kufundishia.

Mhe, Naibu Spika, Kifungu cha 6(1)(f) Kamati inapendekeza kuwa kifungu hiki kifanyiwe marekebisho kwa kumuondoa wakili kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu na badala yake awekwe Mwanasheria wa Taasisi kutokana na unyeti wa taasisi yenyewe na shughuli zake. Mwanasheria wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu abaki kuwa mtetezi wakati itakapotokea masuala ya Taasisi kushtakiwa au mambo mengine kama hayo.

Mhe, Naibu Spika, Kamati yangu inaendelea kushauri kuwa Mwanasheria wa Taasisi ni muhimu zaidi kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Bodi ya ushauri kutokana na ukweli kwamba mambo mengi yanayohusiana na Taasisi yeye atakuwa anayafahamu zaidi ukilinganisha na wakili wa Serikali anaetoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe,Naibu Spika, Utaratibu kama huu ndio unaotumika katika Taasisi ya Elimu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Kamati inahisi kuwa kuna mgongano wa kimaslahi pale ambapo inaweza kutokezea tatizo katika Bodi na itakapohitajika ushauri wa kisheria ambapo mshauri Mkuu huwa ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Hivyo, endapo Mwanasheria huyo akiwa ni miongoni mwa Wajumbe wa Bodi hiyo hapo patakua na tatizo. Hivyo, ni vyema Mwanasheria Mkuu wa Taasisi akawa ni miongoni mwa Wajumbe wa

Bodi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikabaki kuwa ni washauri pindi linapotokea tatizo au patakapohitajika ushauri wa kisheria kutoka kwao.

Mhe, Naibu Spika, mwisho kabisa tunaiomba Serikali kuyazingatia yale yote yaliyopendekezwa na Kamati baada ya kupata ushauri mzuri wa wadau na wananchi kwa ujumla ambao wamesaidia kutoa maoni yao ili kuifanya sheria hii itakapoanza kutumika iwe bora zaidi. Kufanya hivyo ni kuisaidia Serikali na Taasisi husika kutengeneza msingi imara na bora katika sekta ya elimu kwa ajili ya vizazi vya sasa na baadae katika taifa letu.

Mhe, Naibu Spika, Kamati inapenda kuishauri Wizara kukipa meno chombo hiki kipya kinachoanzishwa, ili kiweze kusimamia vyema utayarishaji na uzalishaji wa mitaala iliyo bora nchini mwetu.

Mhe, Naibu Spika, Kwa suala zima la kupata ufanisi, tunaiomba Wizara kuzingatia mambo yafuatayo:

1. Upatikanaji wa Wataalamu wa kutengeneza Mitaala katika Taasisi ya kawaida kuchukua walimu tu kutoka katika skuli na wakawekwa katika Taasisi hii jambo hilo halitotosha, lazima wapatiwe mafunzo maalum ya kuunda mitaala.

2. Hata uandishi wa vitabu vya kiada unahitaji wataalamu wa uandishi.

3. Udhibiti wa Ubora wa Vitabu lazima usimamiwe vizurina Wizara.Vitabu visichapishwe mpaka Wizara ivihakiki.

Mhe, Naibu Spika, baada ya kueleza hayo, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu, wauchangie, waukosowe na waurekebishe Mswada huu kwa kutoa mawazo yatakayosaidia katika kuufanya uwe bora zaidi na hatimaye kuupitisha ili usaidie kuleta ufanisi katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mjadala unaendelea na mchangia wetu wa mwanzo Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako hili fukufu na kuchangia mswada huu wa Sheria ya Kuanzishwa taasisi ya Elimu.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara pamoja na Kamati yetu chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini kwa taarifa hii ambayo muhimu na nzuri, juu ya kuhakikisha kwamba mswada huu unakuwa bora wa maisha ya wanafunzi wetu na vizazi vyetu vinavyokuja baadae.

Mhe. Naibu Spika, katika nchi zote duniani tunaamini kila nchi inapiga kelele juu ya kupata elimu bora, na bila ya elimu bora huwa hatuna maendeleo katika nyanja mbali mbali hasa tukizingatia kwamba kubwa tunalolihitaji katika nchi yetu ni watalam wa fani mbali mbali na ndio maana kuundwa taasisi hii, pana haja na kuna uwezekano mkubwa wa kuhakikisha kwamba mapungufu yaliyojitokeza yanapatiwa ufumbuzi kuwaendeleza wanafunzi wetu.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalie hali ya elimu ya msingi si nzuri na tunaamini hayo, tumeona katika matokeo mbali mbali yaliyojitokeza bado pana changamoto kubwa ya kutafuta taasisi mbali mbali kusaidia ili hili tulilokuwa nalo liondoke kabisa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, taasisi ni chombo ambacho kimepewa mamlaka ya kuhakikisha kwamba inatafuta kila uwezo iliyokuwa nao kwa bidii zake na njia zake ninazoelewa kuweza kusaidia Wizara yetu ya elimu juu ya mitaala mbali mbali ambayo itasaidia kuwaendeleza wanafunzi wetu juu ya hatima ya baadae tunakokwenda, elimu ni nyenzo panatakiwa nyenzo mbali mbali, panatakiwa utaalam mbali mbali, kwa hivyo, kama nilivyosema Mswada huu umesema moja kwa moja kwamba utakwenda sambamba skuli zetu za Serikali pamoja na skuli zetu za *Private,* yaani binafsi, tutakwenda sambamba katika kuhakikisha kwamba taasisi hii inafanya kazi kwa pande zote mbili, mimi hilo nalipongeza kwa dhati kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi kilio chetu kiko kwa wanafunzi wetu wa msingi na Sekondari tukiangalia matokeo ya mwaka huu si mazuri katika nchi yetu Tanzania nzima, lakini Zanzibar ilizidi kwa sababu matokeo ambayo yametufadhaisha watu wengi kama wanavyosema watu kwamba kuna skuli zetu hizi ambazo tunasema kama ndio skuli bora kama Lumumba, Benbella na kwengineko, lakini safari hii zilikuwa za mwisho kabisa. Kwa hivyo, niseme tu kwamba Mhe. Naibu Spika, Mswada huu umekuja wakati mzuri wa kupanga mipango mizuri na kutafuta nyenzo mbali mbali za kusomea na kufundishia ili wanafunzi wetu wapate taaluma nzuri kwa huko mbele wanakokwenda.

Mhe. Naibu Spika, leo katika dunia yetu tuliyokuwa nayo na siye tuzungumzie Afrika ya Mashariki na Kati, sote tunahusika katika Jumuiya zetu bado kuna

ushindani mkubwa wa elimu, na ushindani huu tunauona katika baadhi ya maeneo, lakini mitaala hii ikipewa kipaumbele au kusimamiwa vizuri tutakwenda vizuri katika kuhakikisha kwamba elimu yetu inakuwa bora na wanafunzi wetu wanakuwa bora kuhakikisha kwamba wanapata elimu kwa manufaa ya taifa letu, na maisha yao wenyewe vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, kubwa ninalotaka kulizungumza hapa katika ukurasa wa 39, Sehemu ya Pili ya Mswada, kuanzishwa uongozi wa Taasisi, kazi za Taasisi Nam.5 inasema hivi:

a) Kubuni, kukuza, kufanya mapitio, marekebisho na kutathmini mitaala kwa ajili ya skuli na vyuo.

Mhe. Naibu Spika, nimelitanguliza mwanzo hili nasema kweli dhamira hii ikisimamiwa hayo kuna mwelekeo mzuri huko mbele tunakokwenda kwamba penye kasoro yoyote itafutiwe njia iondoke na kilichokuwa bora zaidi kiongezwe ili tuhakikishe kwamba elimu yetu inakwenda kutokana na wakati tuliokuwa nao.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hilo (b), nashauri Serikali kuhusiana na ukuzaji wa utekelezaji wa mitaala, yaani mambo yote niseme tu kwamba dhamira kubwa au madhumuni makubwa taasisi au mswada huu madhumuni yake kukuza viwango vya elimu yetu katika nchi yetu, tunahakikisha kwamba wataalam wenye fani mbali mbali ambao wameelekezwa humu watasimamia vyema suala hili na kuhakikisha kwamba ubora wa elimu unapatikana siku hadi siku.

Ninalotaka kushauri zaidi kwa Mhe. Waziri, bado ufuatiliaji uwe karibu zaidi kwa sababu walimu tunao, wanafunzi wamo, lakini mara nyingi kuna matatizo ya hapa na pale huwa yale madhumuni hayapatikani hasa ya kukusanya baina ya walimu na wanafunzi kutokana na ushiriki unaotokana na mambo mbali mbali ya nyenzo ambazo hazipatikani. Kwa hivyo, kwa kuwa taasisi hii itafanya kazi ya ziada kuhakikisha kwamba inasimia vyema kwenye mapungufu, kwenye mapato, kwenye nini, ilimradi yapatikane kwa maslahi ya nchi yetu na wanafunzi wetu ili tuweke taifa letu hili au nchi yetu hii katika mwelekeo mzuri wa ushindani wa elimu katika Afrika ya Mashariki na Kati.

Mhe. Naibu Spika, jengine ninalitaka kulizungumza ni kwamba, elimu haina mwisho na tunaamini kwamba mwalimu akisoma leo sio mwisho wa safari ataaka kujifunza zaidi, nimuombe sana Mhe. Waziri, vyuo vyetu vya ualimu tuviangalie kwa hali na mali, kwa sababu vyuo visimamiwe vizuri na walimu

wajue wajibu wao basi elimu itakuwa zaidi. Tuna ushahidi Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tumezungurukwa na maskuli mbali mbali na wanafunzi tunao lakini inakuwa kidogo wingi wa wanafunzi katika maeneo naamini taasisi hii itatafuta ufumbuzi tufanye nini ili tupunguze wingi wa wanafunzi katika madarasa, kwa mfano Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, shahidi, Naibu Waziri, shahidi, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, kuna skuli mpya kule Kwarara inajengwa ya Tumaini, shule hii Mhe. Naibu Spika, madarasa yake huamini, wenzetu wataalam wale Wakorea wamekata madarasa kama holi na wao hisabu yao wasizidi wanafunzi 40 mpaka 45, yaani kama enzi yetu sie wakati huo tulikuwa tupo 25 au 30.

Mimi nataka kumhakikishia Mhe. Waziri, Skuli ya Mahonda mimi mwanafunzi wa mwanzo tena kiongozi wao nilikuwa mimi Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) leo naringa nipo katika Baraza hili, lakini wakati huo katika kusoma kwetu tulikuwa watu 14 au 15, Jullian Raphal, Shihata mimi mwenyewe nipo hapa, Mhe. Samia kafuata nyuma kidogo Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kina Kidawa Hamidi Mheshimiwa nae na wengine wengi tulisoma pamoja. Lakini mimi nilikuwa kaka yao na wao walikuwa nyuma kidogo, kwa hivyo, niseme tu uhaba wa wanafunzi katika darasa ni chachu ya maendeleo katika kusomesha, lakini wingi wa wanafunzi katika darasa ni kumpa adha mwalimu hajifahamu anafanya nini.

Mhe.Naibu Spika, wakati huo walimu walikuwa wanalala mjini asilimia 99 wote, lakini saa moja kamili wako skuli kwa magari ya walimu na wanafanya kazi zao kwa ujasiri na wanafanya kazi kwa utaalam wa hali ya juu, lakini anaamini mwalimu akiondoka na madaftari yake 20 hayazidi 30 anafanya kazi yake vizuri na ana uhakika anafanya nini. Kwa hivyo, naomba Taasisi hii itakapokuja iangalie wingi wa wanafunzi katika darasa, darasa likiwa na wanafunzi wengi ni hatari kwa walimu kuweza kufanya kazi zao ipasavyo. Mimi napongeza sana hilo na namshauri Mhe. Waziri, tusimamie zaidi suala hili kwa ajili ya manufaa ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, mimi baada ya ushauri wangu huo nawaomba Waheshimiwa wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi tunalozungumzia hapa ni hatima ya wanafunzi wetu na watoto wetu, Serikali inataka watoto wetu wasome, wazazi wanataka watoto wao wasomeshwe. Lakini taasisi iliyoundwa humu itatusaidia kwa asilimia kubwa kuharakisha kwamba maendeleo ya elimu yapatikane ili kwenda na ushindani wa nchi zetu za Afrika ya Mashariki na Kati au duniani kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono Mswada huu wa Taasisi ya Elimu kwa asilimia mia moja, sina tatizo nalo, naomba na wenzangu wachangie tuwaunge mkono wenzetu ili tupate manufaa katika nchi yetu. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wale ambao wanataka kuchangia Mswada huu naomba wangeleta majina yao ili kupata kuwaelewa na nikawataja kabla ya kuondoka kwa ajili ya kujipanga kwa jioni, mpaka sasa hivi nina mchangiaji wa mwisho Mhe. Machano Othman Said, kwa hviyo, Mheshimiwa kama utaweza kutumia dakika zote unakaribishwa sana na kama hutoweza basi Mheshimiwa yeyote anaweza kunyanyuka kwa ajili ya kuomba dakika zilizobakia.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kendelea vyema na majukumu yetu ya baraza. Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na timu yake, lakini pia Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa taarifa yao ambayo imesomwa na Mhe. Masoud Abrahmani, nawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, taasisi hii ya Elimu ni muhimu sana katika msingi wa kuendeleza elimu yetu, maelezo ya Mhe.Waziri,yamejieleza sababu za kupelekea kuanzishwa kwa taasisi hii tangu zamani tukiwa na Idara za Mitaala na mambo mengine hadi kufikiria kuwa Taasisi, kwa hivyo, sisi kama Wawakilishi wa wananchi tuna wajibu wa kusaidiana na Serikali kuhakikisha kwamba tunapata elimu bora kwa vijana wetu ili waweze kuja kulitumikia taifa lao.

Mhe. Naibu Spika, naweza kusema taasisi hii imekuja kwa wakati, bali tunaweza kusema imechelewa kidogo kwa sababu ilihitajika mapema zaidi kuliko sasa, wakati mwengine mafanikio ya elimu mwaka mmoja au mwaka wa pili unakuta kuna dhoruba ya anguko la kielimu, hali ambayo imesababisha wazazi na viongozi wa nchi kuwa na taharuki na tulimsikia Mhe. Rais wetu akiwaagiza watu wa Wizara ya Elimu kwamba badala ya kukaa ofisini waende huko kwenye taasisi zao kushughulikia na kuboresha masuala haya ya elimu.

Mhe.Naibu Spika, ni kweli kwamba Zanzibar tuno mfumo wetu wa elimu, lakini hatimae tukifika elimu ya juu inabidi tuungane na ndugu zetu wa Tanzania Bara kwa ajili ya kufanya mitihani ya kitaifa kwa elimu ya juu kuanzia *Form VI* na kuendelea mbele.

Sasa kama hatukujipanga vizuri katika suala hili kwa nafasi ya elimu ya huku ya maandalizi, msingi, kati na sekondari inawezekana juhudi zetu zikawa zina matatizo na faida zake zikaonekana kwa uchache sana.

Mhe. Naibu Spika, mitaala ya elimu ni jambo la msingi sana kwa skuli za serikali na skuli za binafsi. Kwa sababu leo mtu anaweza kusoma skuli ya binafsi kesho akawa serikali au leo akawa serikali kesho akawa ya binafsi. Kwa hivyo, ni wajibu wa taasisi hii kusimamia na kutoa maelekezo ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na utaratibu mzuri wa elimu. Nakumbuka kama miaka 12, 13 iliyopita Serikali yetu ninafikiri ilikuwa 2006 kama sikosei ilipitisha Azimio au Sera ya Elimu kwamba, miongoni mwao ni kuanza elimu ya maandalizi. Ni kipindi kirefu kidogo wakati ule alikuwa Mhe. Haroun ndio Waziri wa Elimu, lakini sisi Waheshimiwa Wawakilishi na wenzetu Wabunge na Madiwani tunapotembelea katika skuli zetu za majimboni kwetu na kwa bahati nzuri mimi na Mhe. Mbunge na Madiwani wetu tumeshatembelea skuli zote za jimbo letu.

Tuna skuli 6 katika Jimbo letu la Mfenesini, lakini tulilolibaini kwamba baadhi ya skuli hazina madarasa ya maandalizi na hili linawezekana sio kwa jimbo letu ila inawezekana kwa majimbo mengi kwamba hawana madarasa maalum ya maandalizi. Kutokana na tatizo hilo wengi wao wanafunzi wa maandalizi wengine wanasoma chini ya mti, wengine wanadowea madarasa wenyewe wametoka wanaingia wao, kwa hivyo, bado tumetoa sera lakini utekelezaji wake bado ni mgumu.Tunaomba wizara kwa kupitia Taasisi kama hii hili suala walipe nguvu ili lionekane kwamba tunajenga elimu bora.

Jambo jengine ambalo ni shida katika elimu sasa hivi ni wingi wa wanafunzi kwa darasa moja katika Skuli za Serikali. Baadhi ya maeneo darasa lina wanafunzi 125 mpaka 200 na bahati mbaya sana kwamba hilo darasa pengine hata madawati halina. Sasa mfikirie mwalimu ambaye anataka kumfundisha mwanafunzi kujua kuandika na kusoma, zaidi kuandika, ina maana huyo mwalimu lazima na yeye aende chini amfate mwanafunzi.

Sasa kama mwalimu ataenda chini mara 150 kwa siku hiyo ni mara moja tu na lazima aende mbele aangalie wanaandikaje, arudi nyuma aangalie wanaandikaje huyo mwalimu akirudi nyumbani kiuno hana. Kwa sababu atachoka na atakuwa sijui katembea kilomita ngapi, anaenda anaangalia bahati mbaya hakuna dawati ainame, amsaidie mwanafunzi anyanyuke, hajasahihisha madaftari yao, hajapanga programu za siku ya pili za skuli. Kwa hivyo, ukiangalia Taasisi hii itakupambana na vikwazo vya kuwasaidia walimu. Mhe. Naibu Spika, walimu ni watu ambao wanapata tabu sana, wanafanya kazi

katika mazingira magumu na tunasema kwamba elimu ni wito au walimu ni wito kama ulivyo udaktari nao ni wito. Lakini na askari pia wanasema uaskari nao ni wito.

Sasa kwa maoni yangu ni kwamba uanzishwaji wa Taasisi hii utasaidia kupunguza baadhi ya kero na matatizo haya ambayo yanawakabili walimu na wanafunzi kwa ujumla. Taasisi hii ninaiomba sana isaidiwe na Wizara, tunaanzisha chombo ambacho tunataka kukipa mamlaka, lakini tusije kukibania katika utekelezaji wa kazi zake. Yapo matatizo ukiacha wingi wa wanafunzi, lakini walimu wenyewe pia wana matatizo makubwa na kama mwalimu ana matatizo makubwa ina maana akili yake wakati wa kufundisha inakuwa ni ndogo sana kwa sababu anafikiria nyumbani, anafikiria na skuli.

Miongoni mwa matatizo yao walimu kutokulipwa kwa fedha zao za likizo ambazo zinatolewa kila miaka 3 mara moja. Lakini walimu wengi fedha hizi hawalipwi, kuna madai ya madeni makubwa ya fedha hizi. Kwa hivyo, tunatumia fursa hii ya kuanzisha Taasisi, pia kuikumbusha wizara kwamba hili nalo ni muhimu katika kujenga uwezo na uwelewa wa walimu. Lakini jengine pia kutokulipwa fedha zao za usafiri kwa baadhi ya walimu ambao wanastahiki kulipwa ambao wanakaa mbali na skuli ambazo wanafundisha.

Mhe. Naibu Spika, unaweza kwenda kwa baadhi ya skuli ambazo ziko nje ya mji, kwanza mwalimu anaweza akachelewa, lakini anaweza akajivuta asichelewe asubuhi na zaidi wale wanaoingia katika vipindi vya jioni, wakati wa kurudi majumbani kwao ni pirika kubwa sana. Hawana uhakika wa kupata usafiri pengine wizara ingeliwafanyia utaratibu basi kwa wale ambao wanataka au sijui kama wanao wa kuwakopesha vipandio ili waweze kurudi majumbani kwa haraka zaidi kuliko ilivyo sasa.Walimu wetu wanadhalilika sana unawakuta wengine wanangojea magari ya michanga, wengine wanangojea gari za mizigo mengine wanaomba *lift* ili waweze kufika majumbani mwao, kwa hivyo, pia hilo ni tatizo la walimu.

Lakini lipo tatizo na nimefurahi kwamba katika bodi yao pia kutakuwa na mwakilishi wa Skuli Binafsi ni vyema na ni vizuri zaidi. Tunalo tatizo la ada kwa Skuli Binafsi, hakuna pengine ada elekezi, skuli hii inatoa pengine laki tano, skuli hii laki saba, skuli hii milioni tatu. Je, hili nalo wizara huwa hawaliingilii kwa sababu ndio tuko katika biashara huria, lakini biashara huria yoyote usafiri baharini ukienda, Wizara Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji wanaweka bei elekezi kwamba nauli isizidi hii. Ukienda Taasisi nyengine wanakwambia bei isizidi hii, lakini huku kwenye elimu, kwa nini nako hakuna

bei elekezi ambayo itakuwa sio hasara kwa wawekezaji lakini pia haiwaumizi watumiaji wengine.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka kulizungumzia ni huu utaratibu mpya ambao tunatarajia utaanza wa kuwatoa wanafunzi wa darasa la sita na kwenda darasa la tisa, sijui tafiti gani zilifanywa na kuonekana ubora wa suala hili. Kwa sababu kama nilivyoanza mwanzo kwamba hatimaye tutamalizana na wenzetu, kama mtu ametoka la sita, la tisa na kule Bara katoka la saba, la tisa, hatuoni kwamba litakuwa ni tatizo, wakienda huko *Form IV* kwamba, huyu kapiga sita na yule saba halafu wanakwenda mbio moja, haiwezi kuwa matatizo kwetu na kama itakuwa hivyo, je, huu umri wa mwanafunzi si utakuwa mdogo sana, wanafunzi wanamaliza skuli hata *Form IV,* lakini mzazi huna uhakika kama namtuma dukani atarudi na kile kitu ambacho nimemtuma kwa sababu ya umri wake.

Kwa hivyo, hatuoni kwamba je, kama tunakwenda katika mfumo huu hatuwezi kupandisha kidogo umri wa mwanafunzi, kwani tunakimbilia wapi na hawa wanafunzi wakesha wanakwenda wapi. Siku hizi hakuna JKU ya lazima, hakuna chochote, akimaliza *Form IV* chini ya miaka 16 anakuwa mzigo nyumbani. Angalau amalize *Form IV* miaka 16, 17 halafu aende *Form V* na *VI* pengine chuo akianza miaka 20 sio tatizo. Sasa hili Mhe. Waziri, na wataalam wako hebu tusaidieni ili tulijue hasa faida zake ni nini kurusha hili darasa la saba na kuliondoa.

Lakini Mhe. Naibu Spika, jengine lipo tatizo la vitabu pamoja na juhudi ya serikali na ninafikiri kwa kuanzisha taasisi hii inaweza kutusaidia kulimaliza hili tatizo, wakati mwengine si kwamba kila mwanafunzi anapata kitabu, pengine anagawana na mwenzake. Lakini pia hata wale walimu mafunzo yao yanakuwa hayakutimia katika mifumo mipya, tunabadilisha mfumo, lakini walimu hawakupata ile elimu yenyewe ya kuja kukabiliana na changamoto za ule mfumo mpya. Sasa ili kujiweka sawa na kuhakikisha kwamba tunafanikiwa katika Taasisi hii, lazima kwanza vitabu vya kiada na ziada vipatikane vya kutosha, lakini pili na walimu nao wajue wanafanya nini katika mfumo huo.

Mhe. Naibu Spika, hata Bara nao wanalalamika kwamba kila awamu wanabadilisha mfumo, mara kule ulikuwa mfumo wa Mungai, katoka Mungai kaingia Kawambwa na yeye katoa wake, katoka Kawambwa kaingia Ndalichako na yeye kaweka wake. Sasa na hapa Zanzibar isije ikawa katoka Mhe. Haroun na mfumo wake, kaingia Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban akaweka wake, kaingia Mhe. Shamhuna na yeye akaweka wake, leo anaingia

ndugu yangu Riziki Pembe na yeye anaweka wake, watu wanasema 'miyunzi mingi unampoteza mbwa usasini' kwamba itakuwa haijulikani ufate myunzi upi.

Sasa ni vyema mimi ninawaamini sana Mhe. Riziki ambae ni waziri na ninamuamini Mhe. Mjengo kama Naibu Waziri, hawa wote ni walimu na watu wenye maadili na taaluma wanayo. Kwa hivyo, ni matarajio yangu kwamba wakiambiwa na watendaji wao kwanza watajifikiria wao wenyewe. Maana wakati mwengine ukiwa mwalimu halafu ukiwa Waziri wa Elimu inasaidia, kuliko kwa mtaalam mwengine kwenda Wizara ya Elimu. Unaweza kuwa pale wataalam wa elimu wapo waliobobea wakakudanganya kidogo ukaingia kwenye mkenge.

Lakini matarajio yangu kwamba kwa nyinyi mtakuwa na uwezo wa kubaini kwamba hili tunaloambiwa na wataalam wetu lina faida kwa wananchi na vizazi vyetu na hili tunaloambiwa na wataalam wetu pengine la kuchapisha vitabu vipya vya skuli nyengine pengine ni maslahi ya muda tu ya wataalam. Hili litasaidia kuepusha kuporomoka kwa mfumo wetu wa elimu na kusababisha vijana wetu wengi kufeli.

Pia, hii Taasisi mimi naomba iangalie sana katika zile zile sera za zamani kwamba, tulikuwa na sera na hili litasaidia kupunguza pengine wingi wa watoto kwenye darasa moja. Kulikuwa na sera zamani kwamba wananchi wakijenga darasa mpaka katika sehemu ya lintana wizara inamalizia kuezeka na kuweka samani. Je, hii sera bado ipo na kama ipo, mahitaji yakoje na tumejipanga vipi kuhakikisha kwamba tunalimaliza.

Jengine Mhe. Naibu Spika, tuweke nguvu sana katika madawati, bahati nzuri zipo juhudi za serikali katika suala hili na mimi kwanza nimpongeze Rais wetu kwa kuona kwamba hili ni kero na tatizo kwa wanafunzi. Lakini pia tumpongeze Mhe. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mhe. John Pombe Magufuli baada ya uamuzi wake kwamba zile fedha za Bunge, Bunge lililopita la kumi ambazo zilikuwa kama bilioni sita zilizorejeshwa serikalini akaamua kwamba zinunuliwe madawati na yagawanywe kwa nchi nzima bila kujali upande wowote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani.

Kwa bahati nzuri Ofisi ya Bunge kwa kupitia Waheshimiwa Wabunge wetu wameshapewa na karibu wote wameshayatoa majimboni kwenye shule mbali mbali, hili ni jambo la kupigiwa mfano na linaonekana kwamba viongozi wetu wanatujali wananchi. Sasa nilimsikia Mheshimiwa mwenzangu akisema kwamba tutilie mkazo na ninafikiri mpango kama ule uliofanyika kwa Bunge

yakipatikana madawati nayo kwa serikali ya SMZ basi na Waheshimiwa Wawakilishi nao washirikishwe katika ugawaji wake moja kwa moja ili na wao waonekane na wananchi na wao wamefanya kazi ya kuwatetea na kuwasaidia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, sina mengi katika mswada huu, lakini matarajio yangu kwamba Waheshimiwa wenzangu na wao watatoa mchango wao katika kusaidia kuimarisha na kuanzishwa kwa Taasisi hii muhimu ya elimu. Lakini niseme tu kwamba taasisi hii tunaomba sana iwe na mashirikiano sana na Baraza la Taifa la Mitihani la Zanzibar. Kwa sababu huyu ndio atakua mzazi wa kuibua, kutengeneza, vipaji vya vijana na kuwapa elimu bora. Lakini Baraza la Taifa la Mitihani wao kazi yao ni kuangalia hiyo kazi ambayo imefanywa na Taasisi katika kuwapiga uwezo hao vijana ambao wataambiwa wako tayari kwa ajili ya kusaidiwa na kufanyiwa mitihani na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mfenesini naunga mkono mswada huu na matarajio yangu kwamba tutaupitisha vizuri ili Wizara ya Elimu wakaendelee na majukumu yao. Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nina jina la mwisho la mchangiaji natarajia kwamba mswada huu wengi wameuridhia ndio maana labda wanataka waupitishe na nimpongeze sana waziri kwa hilo, kwa hivyo, ninaamini kwamba leo tutaumaliza mswada huu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika, na mimi napenda kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa nafasi kunipa niweze kuchangia mswada huu ambao ni muhimu, nimpongeze Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa kuja na wazo hili pamoja na Serikali kwa pamoja. Lakini kwa ujumla niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendeleza juhudi za makusudi katika kuwasaidia wananchi wetu hasa katika masuala matatu muhimu ambayo ni elimu, afya na maji, lakini hapa tupo katika suala la elimu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nikiri na niseme kwamba katika kipindi ambacho kitakuwa muhimu katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika awamu zote za Serikali iliyopita basi naamini katika Wizara yetu hii ya Elimu kuelekea katika mfumo huu tunaokwenda nao 2015/2020, sina budi kusema kwamba Wizara hii ya Elimu itakuwa na changamoto nyingi na Mhe. Waziri, ambaye amepewa majukumu haya na Mhe. Rais basi katika suala zima ambalo la kusimamia *port folio* hii basi nimtakie kila la kheri na ninaamini Mhe. Riziki

Waziri wa Elimu ni jembe ataweza kuyasimamia haya yote, kwanza ni kijana mwenzetu mwenye maarifa na mtu wa kuleta mageuzi tofauti katika nchi yetu.

Sasa baada ya kuongelea hayo, ningependa niende moja kwa moja katika kuchangia huu mswada. Mhe. Naibu Spika, kila mwaka serikali itakuwa inawasilisha ripoti zake tofauti katika mpango mzima hasa katika kuomba ridhaa sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuweza kuwapatia ruhusa au idhini au kuidhinisha bajeti ya serikali.

Mhe. Spika, katika taasisi nyingi ambazo serikali tunazipata ni kwenye mafungu ya fedha yanapotolewa katika bajeti kuhakikisha kwamba Hazina wanawatilia au Mhe. Waziri wa Fedha, kuweza kuwapatia. Kwa hiyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri, katika mwaka wa utekelezaji juu ya taasisi hii aweze kusimamia suala la kifedha katika mpango wote mzima ambao amejipanga kwenye majukumu ambayo ni ya kisheria watakayopewa na serikali pamoja na Baraza la Wawakilishi katika utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, la pili, nisome katika madhumuni na sababu ya uendeshaji wa taasisi hii. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako. Katika eneo ambalo linazungumzia madhumuni na sababu inasema kwamba;

"Madhumuni ya mswada huu ni kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, ambayo itakuwa ni wakala wa serikali.Taasisi itakuwa na jukumu la kuandaa mitaala, vifaa vya kufundishia, kufanya tafiti za elimu zinazohusiana na maendeleo ya mitaala, na kuimarisha vifaa vya kujifunza ili kuhakikisha utoaji wa elimu kwa wananchi|".

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kifungu hiki ambacho kimeandikwa katika mswada huu, basi mambo yote ya elimu Zanzibar utayakuta yapo hapo na yamejifunga. Lakini ukienda katika kifungu cha (3) kinasema kwamba;

"Wanatekeleza majukumu ya mswada huu na mapendekezo yote juu ya ripoti ya Mhe. Rais wetu..." Mwenyezi Mungu amrehemu "...Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, ripoti ya mwaka 1982".

Mhe. Naibu Spika, Sasa katika maeneo ambayo ripoti hii iliyoandaliwa wakati huo ni vizuri pia Mhe. Waziri, akaangalia kufanya utafiti juu ya ripoti kuangalia hayo majukumu yanayokwenda juu ya ripoti ya mwaka 1982 na sasa je, yapo sawa? Mambo mengi yamepita dunia imesogea imekuwa kama kijiji, nchi, wananchi, watu wanazungumza lugha sasa hivi tofauti.

Mimi katika hilo eneo la utafiti ambayo taasisi hii itakwenda nayo ningemuomba sana Mhe. Waziri katika maelekezo baada ya sheria hii kutungwa na kupitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, basi elimu 4 ningependa azipe kipaumbele katika tafiti zao ambayo ni; lugha ya Kiarabu, lugha ya Kiingereza, lugha ya Kichina na lugha ya Kifaransa.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu katika maeneo mengi ambayo Wazanzibari watahitaji katika lugha nyengine mbali ya Kiswahili na Kiingereza, basi katika hizi tatu nilizozitaja watakuwa hawachezi mbali. Kwa hiyo, katika tafiti zao na majukumu ambayo atawapa hizi taasisi na kuangalia ni jinsi gani katika skuli zetu wataweza kufaidika hawa vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, pia katika eneo moja ambalo ni muhimu ambalo limetajwa na kuangalia suala la vifaa ambapo Mhe. Mwakilishi wa Mfenesini na pia ni Mbunge wetu kutoka Baraza hili Mhe. Machano Othman Said amezungumza kwenye suala la vifaa. Mhe. Naibu Spika, kuna changamoto kubwa sana katika skuli zetu pamoja na vyuo vyetu vingi juu ya vifaa. Mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri, sehemu moja ambayo naililia siku zote na nimetaja katika Baraza hili ni Chuo cha Karume. Pia, katika skuli zetu za Sekondari kuangalia kwenye *practical science* hasa katika masuala ya *dissection,* walimu wetu wanavyohangaika kwenda kutafuta hayo mapanya na mambo mengineyo *laboratory* kufanya hizo *tests,* kuwa na *filtration, bunsen burner* na vyenginevyo. Haya yote yanakuwa ni changamoto, hasa katika skuli zetu zilizokuwa zipo vijijini na Pemba.

Mimi ningependa kuona katika awamu hii ya serikali yetu ambayo ni 2015 – 2020 masuala ya vifaa madogo madogo kwenye skuli zetu tuache kuimba wimbo wa Taifa tubakie sasa kwamba tunaendeleza elimu, lakini vifaa sasa iwe tayari kwa skuli zetu zote vimekamilika. Katika mnasaba huo ninapochangia hapa katika suala hili ningependa nimshauri pia katika bodi ambayo inataka kuundwa nimeangalia vile vifungu kwenye utaratibu wa wajumbe wametajwa, ningependa nimshauri kama itawezekana wajumbe ambao wametajwa, nampendekeza pia Mkurugenzi wa *Diaspora* awe pia ni mjumbe katika bodi hii ili aweze kuwaunganisha vijana wetu na pia katika fursa ambazo ndugu zetu wengi Wazanzibari wanataka kusaidia katika nchi yao, basi waweze kupata uwakilishi katika taasisi hii.

Mhe. Naibu Spika, Kuna mambo mengi ambayo vijana wataweza kufaidika kama vifaa, kuna mambo tayari vijana wetu, wazee wetu, kaka zetu wapo nchi tofauti za Ulaya, nchi za Arabuni, nchi za Marekani Magharibi wanataka kutusaidia Zanzibar katika masuala ya elimu basi angalau wawe na mwakilishi

wao katika hiyo taasisi ikiwa Mhe. Waziri na Wajumbe wataona kwamba lina mtu muhimu.

Mhe. Naibu Spika, pia katika uwakilishi wa wajumbe kwenye hiyo Nam. 6 Bodi ya Ushauri (h) ametajwa pia mwakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Wafanyakazi Zanzibar. Lakini kwa mtazamo ambao Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inakokwenda sasa hivi wanaangalia mfumo mkubwa wa kufanya kazi pamoja na sekta binafsi. Sasa kama itawezekana katika mwakilishi mmoja aliyetoka Jumuiya ya Wafanyakazi Zanzibar basi iwe katika sekta binafsi kuna Jumuiya ya Wafanyakazi wa biashara na viwanda na pia kuna jumuiya ya wawekezaji katika sekta ya utalii pia na usafirishaji.

Kwa hiyo, mimi ningeshauri hapa mbali ya jumuiya kutoka kwa wafanyakazi, basi kama wataongeza pia katika jumuiya moja katika sekta binafsi ambayo inayotambulika na iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za sheria za Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika hilo suala la *Diaspora* ni vizuri wakati waziri sheria itapopita Mwenyezi Mungu akimjaalia itakapopitishwa na Wajumbe wa Baraza, basi suala zima la *Diaspora* ni kuliangalia kwa upana mkubwa zaidi hasa baada ya mkutano mkubwa uliofanyika na umeleta matumaini makubwa kwa Wazanzibari na Watanzania kwa mara ya kwanza hapa Zanzibar mwezi uliopita na umeleta mafanikio mengi na kuvuta watu wengi. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuipongeza serikali kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Rais mwenyewe kwa kulisimamia hili.

Mhe. Naibu Spika, kinginge ambacho nataka nizungumze ni somo la Historia, hili linakwenda kutokana na maelezo aliyoyazungumza Mhe. Waziri katika huu mswada unaoletwa hapa juu ya madhumuni na sababu. Somo la Historia, Mhe. Naibu Spika, ni kwamba historia yetu ya Tanzania, historia yetu ya Muungano wetu, historia yetu ambayo tulipotoka mpaka kufikia Mapinduzi yetu na kutoka Mapinduzi yetu mpaka leo kufikia hapa imekuwa inapotoshwa.Vijana wetu hawajui nchi yetu, uongozi wetu, wapiganaji wetu, mambo yetu yaliyotokea huko nyuma hadi tumefikia hapa leo.

Leo vijana wetu ukimuuliza kuhusu Mhe. Rais Karume, wanajua Rais Karume ambaye aliyemaliza awamu yake ya sita na hawamjui mwaka, siku, eneo alilozaliwa ambalo lipo katika jimbo langu kule Tunguu/Mwera, skuli aliyosoma, haya yote yameondoka. Juzi nilikuwa nasoma kwenye mtandao juu ya ripoti ambayo imeandikwa juu ya uchaguzi wa mwaka 2000 inasema kwamba mwaka 1977 wakati vyama vinaungana basi Rais Karume alikuwa

hataki vyama viungane. Hivi jamani Rais Karume kweli alikuwa yupo hai mwaka 1977?

Historia imekuwa inapotoshwa kwa makusudi, vitabu vinaandikwa haviangaliwi na katika historia hiyo pia inayoandikwa vitabu basi viangaliwe kama kweli hii ni historia ya kwetu au si ya kwetu na kama imechanganywa basi vitabu vyengine vinafaa vifungiwe, japokuwa nchi yetu haipendi kuleta mambo ambayo hayastahiki, lakini watu wanafanya kwa makusudi kupotosha. Kwa hiyo, mimi naomba sana katika hizo tafiti na hii taasisi itaposimama katika suala la historia basi juhudi zifanyike za makusudi ili vijana wetu wanaotaka kujua nchi yetu imetokana na kisiasa, kimaendeleo, vizazi vyao wazidi kufahamu, kwa sababu binadamu unapokuwa huna historia na kutojua wapi umetoka unaweza kuwa unatembea wewe kama mtu ambaye ni mlemavu wa macho ukitembea njiani hujui unapokwenda, humjui babu yako, humjui bibi yako, hujui wazee wako walikuwa wapi, hujui hata historia ya nchi yako na hivi vitu vyote vipo.

Kwa hiyo, ni muhimu historia yetu ya Zanzibar ikatambulika, kwanza ni historia ambayo yenye sifa, historia ambayo wageni wanatoka kutoka nje wanataka wazidi kuielewa. Leo unakuta vijana ambao ni watembezaji juu ya masuala ya usafiri wanasimama nje ya jengo la Beit-el-Ajaibu wanazungumza katika historia hii wanawaambia zile nguzo pale ni za mawe, lakini zile nguzo ni za chuma, kwa sababu hawajui lakini na chuma kile kimetoka wapi? Kwa hiyo, ni muhimu historia hii ikathaminika na pia ikatambulika vizuri na ikafanyiwa kazi nzuri ili vijana waweze kujua historia ya nchi yetu katika nyanja tofauti za kisiasa, kiuchumi na mengineyo.

Mhe. Naibu Spika, pia, ningependa kuzungumza suala la vipaji. Mhe. Naibu Spika, mimi kule jimboni kwangu juzi nilikuwa naangalia vijana ambao wanafanya sarakasi. Nina vijana wengi wana uwezo na ubunifu na nikiri kwamba juzi tulipokwenda kufungua Baraza la Vijana pamoja na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kule kwenye Kisiwa cha Uzi ameona mwenyewe jinsi vijana walivyokuwa na hamu ya kuweza kujua na kujifunza mambo tofauti.

Lakini elimu kama ni ufunguo wa maisha ya binadamu kwa kuweza kumsaidia kuweza kusimama na kuweza kujua ni muhimu tukaangalia moja kwa moja vijana wetu hawa vipaji vyao na juzi nilikuwa nasoma katika gazeti, jinsi gani Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. John Pombe Joseph Magufuli akisema kwamba anataka mtoto wa masikini aweze kupata ajira, aweze kupanda juu kama mtu mwengine.

Mhe. Naibu Spika, Lakini vipaji vyetu vilikuwepo katika maeneo tofauti, ukienda kule jimboni kwa Mhe. Mihayo Juma Nh'unga, Mwera utakuta vijana wake ambao wanamkubali yeye mwenyewe kama kijana, ukienda kule Chaani kwa Mhe. Nadir Abdul-latifu Yussuf, anao vijana wake wengi sana, ukienda kwa ndugu yangu kule Mhe. Suleiman Makame Ali, kule Pemba Ziwani ana vijana wake ambao wanamkubali na wengi wanataka kuona ubunifu wao katika maeneo ambayo waweze kutambulika.

Mhe.Naibu Spika, sasa katika hizi tafiti ambazo zitakazofanywa na taasisi hii hawa vijana wenye vipaji lazima tuwaangalie na tuwaendeleze katika maeneo ambayo wanastahiki, ikiwa ni elimu waangaliwe katika elimu, ikiwa ni michezo waendelezwe katika michezo, sio tunakuja hapa tunacharaza mabao 30, tunasema watu tupeane moyo, haiwezekani. Tunataka tafiti zifanyike za kielimu ya kisaikolojia ili tuweze kutambua vipaji vya vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, tuangalie katika mpango mzima wa dunia sasa hivi unavyokwenda. Suala la kutumia mtandao ni katika suala muhimu sana kwa vijana wetu kwa miaka ya mbele. Tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua mkopo na kuwaunganisha tena vyote visiwa vya Unguja na Pemba kwa kule Pemba wamejenga ile *fiber optic* ya *linear* kutoka Kaskazini mpaka Kusini na kuunganisha pamoja na hii *fiber optic* ya kutoka Tanzania Bara kuja mpaka Fumba na kuingia katika maeneo yote katika kisiwa cha Unguja. Hii *fiber optic* ambayo imegharimu serikali dola milioni 18 ambayo ina majukumu pia kuhakikisha vijana wetu wote kwenye maskuli yote wataweza kufaidika na kuweza kutumia hii *e-education* kutoka vyuo vikuu na shule za sekondari pamoja na hizo kompyuta ambazo zitakuja kuletwa katika maeneo yote.

Mhe. Naibu Spika, ili waweze kutumia huu mtandao kuweza kufanya *research*, kuweza kujiendeleza kielimu kwa masomo tofauti, kuweza kufahamu ni muhimu taasisi hii Mhe. Waziri, ukaweza kuisimamia katika suala zima la *e-education* waweze nao pia kujiunganisha hasa katika suala la elimu wanapomaliza nafasi zao za kusoma ili kupata ajira katika soko lilokuwepo huko nje isiwe na mashaka, wawe na kompyuta ya kufahamu, isifike pahala mtu anaangalia *keyboard* anapoanza kuangalia anaanza kuona pale kwamba pale hana uhakika, anajua lugha ya Kiingereza lakini *computer literate* bado ni *medium* au uwezo bado ni mdogo.

Kwa hiyo, suala la mtu kufahamu mtandao wakati serikali imeshaweka *fiber optic* ambayo imegharibu dola zaidi ya milioni 18, ni suala sio la maombi, ni suala la lazima kila kijana anastahiki kuwa ana uwezo wa kutumia *internet* na kuweza kutumia kompyuta ambazo wanazitumia.

Kwa hiyo, katika taasisi hii na kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri, ni vyema tukahakikisha katika miaka mitano hii haya yote yanafanyika katika visiwa vyetu Unguja na Pemba na tunakwenda kwa kasi ambayo tutakwenda sawa sawa na nchi zetu za Afrika Mashariki tutakuwa tuko mbali zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia napenda tena kutilia mkazo juu ya maombi yangu tena juu ya Chuo cha Karume. Nilizungumza katika vifaa ambavyo vilivyokuwepo katika Chuo cha Karume, chuo hiki ni muhimu *Karume Institute of Science and Technology* ambacho wanakiita (*KIST*) na katika vipaji na vijana wetu ambao wanataka kujiendeleza katika soko la ajira lilokuwepo huko nje hiki chuo tayari ni kitovu. Kwa hiyo, ninaomba sana Mhe. Waziri katika majumuisho yako unihakikishie, uniahidi wajumbe wote kwa pamoja na mimi mwenyewe kwamba katika hayo yote tuliyoyazungumza na katika tafiti zote utakazofanya basi mimi nitakuwa sina tatizo na nitaunga mkono yote ambayo Mhe. Waziri na serikali yetu imekusudia kuyafanya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumaliza hapo naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa nafasi uliyonipa na niwashukuru wote wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Mhe. Waziri, kwa kunisikiliza. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kunipa fursa hii kwa kuweza kuchangia juu ya mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Elimu pamoja na watendaji wake kwa juhudi kubwa wanazochukua katika utekelezaji wa kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaweza kujifunza na kwa kuwaekea mazingira mazuri ya kujifunzia.

Lakini pili niipongeze serikali kwa kuweza kutuletea mswada huu kwa lengo la kuleta maendeleo makubwa ya elimu kwa Zanzibar. Baada ya pongezi na shukurani hizo nianze kuchangia mswada huu kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umewekwa vizuri katika mazingira mazuri ambayo wanafunzi wa Zanzibar wataweza kujumuika vizuri kama nilivyoeleza mwanzo na wataweza kujifunza vizuri kwa maendeleo endelevu ya elimu. Lakini ili kufikia maendeleo hayo kuna mambo lazima tuyazingatie. Kwanza kujenga mazingira mazuri ya walimu ikiwemo kuwapatia vitendea kazi kama inavyohitajika, lakini vile vile walimu wana mazingira mengi ambayo yanawazunguka ili kupelekea lile lengo lisifikiwe. Kuna malalamiko ya walimu

ambao wanakuwa wanaekewa vituo vya mbali, pengine mwalimu anakaa mjini anasomesha shamba.

Lakini sasa mazingira yanakuwa yanampelekea mwalimu yule pengine kufika kule kituoni alipangiwa kuchelewa, lile linakuwa moja ya jambo ambalo linasababisha kudhorotesha elimu, kwa sababu pengine pale alitakiwa kuanza kufundisha saa saba, mwalimu anafika pale saa tisa. Katika hali kama ile yale malengo ya siku ile ya kufundisha yatakuwa hayawezi kufikiwa, hivyo basi, niiombe wizara kuwajengea mazingira hawa walimu kuhakikisha kwamba wanafika maeneo ambayo wamepangiwa kazi mapema na kuweza kufundisha kama walivyotakiwa.

Mhe.Naibu Spika, vile vile, kuwa na vifaa vya kufundishia vya kutosha kwa wale wanafunzi ikiwemo vitabu. Tukiwa na upungufu wa vitabu lengo la elimu halitofikiwa lile ambalo tunalitaka. Lakini kujenga mazingira ya kuwapatia wanafunzi vitabu vyote vya kujifunzia, lakini vile vile vitabu hivi vijumuishwe, tuelewe kwamba kuna wanafunzi wa aina nyingi. Kila siku nazungumza hapa watu wenye ulemanvu wanakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa vifaa vya kujifunzia vikiwemo mashine za *braille* pamoja na karatasi.

Aidha, vitabu vinavyochapishwa kwa maandishi makubwa kwa wale ambao wana ulemavu wa uoni hafifu vinakuwa havipatikani, jambo ambalo linakuwa linawakosesha wale ambao wana tatizo lile kujifunza. Mbali ya vile vifaa, vile vile wanahitaji kupata *lens* kwa ajili ya kuona mbali na suala hili pia halipo. Kuanzishwa kwa taasisi hii nina imani kwamba serikali itaweka mazingira mazuri ya kuhakikisha hawa wanafunzi wenye matatizo changamoto zao zinatatuka.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine nazungumzia juu ya ufuatiliaji wa walimu. Viongozi wa wizara wawe na ufuatiliaji wa karibu juu ya walimu ambao wanafundisha skuli zetu. Tatizo liliopo hivi sasa walimu wengi wanakuwa na ufuatiliaji mdogo, kwa hiyo mtu anafundisha vile ambavyo yeye mwenyewe anahisi. Kwa sababu sisi tumo katika jamii na watoto wetu wamo katika hizo skuli maendeleo tunayaona. Vile vile huwa tunafuatilia mule katika skuli na tunaona wale walimu, yaani kile kipaumbele chao cha kusomesha wanakuwa wengine wanahitaji wapate nguvu ya kusukumwa ili waweze kufundisha. Kwa ufupi wanakuwa hawako tayari na ile kazi yao.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kutokana na changamoto ambazo zipo hivi sasa za wanafunzi kuwa wengi madarasani, pia walimu unapowauliza hili wanasema hii ni moja ya jambo ambalo linasababisha kuwa watoto wale wasiweze

kujifunza vizuri. Kwa hiyo, wizara ifanye mikakati au iandae mipango ya kuhakikisha tunapunguza ule wingi wa wanafunzi madarasani ili kuondosha yale manung'uniko ya walimu kwamba watoto ni wengi na wanashindwa kuwafundisha.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea nimuombe Mhe. Waziri kuimarisha elimu mjumuisho, tunaanzisha taasisi ya elimu lakini mpaka sasa kwa upande wa watu wenye ulemavu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeanzisha elimu mjumuisho lakini bado elimu hii iko nyuma. Nathubutu kusema kwamba mimi mwenyewe ni shuhuda, nimepita katika yale madarasa kuna changamoto nyingi ambazo zinawakabili wale walimu wenyewe wanaofundisha.
Vile vile katika huu utoaji wa hivi vifaa, wizara inapotoa vifaa kwa skuli basi izingatie na haya madarasa ambayo yameanzishwa na wizara yenyewe, hili suala la elimu mjumuisho penye kugawiwa madaftari ya mahudhurio basi wanakuwa wanasahauliwa hawapewi hata lile daftari la kuorodhesha wale wanafunzi ambao wanasoma katika darasa la mjumuisho, jambo ambalo linamfanya yule mwalimu mwenye dhamana pale daftari lile alinunue yeye aje kuorodhesha watoto jambo ambalo sio zuri.

Pia katika huu ugawaji wa madawati uliofanyika, kuna wanafunzi wenye ulemavu wanasoma kutokana na ulemavu wao basi wamewekewa vile viti vidogo kabisa vya wanafunzi wa *nursery* ndivyo wanavyosomea watoto wale, mtoto ana miaka 17 au 18. Hapo hapo utamkuta mtoto huyo ana tatizo la kuona na kusikia, ana uoni hafifu, inabidi ainame, kiti kiko chini baada ya matatizo aliyonayo tutamuongezea na matatizo mengine.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri ili kuimarisha elimu tuangalie katika sekta au taasisi zote. Hii elimu mjumuisho imeanzishwa kwa nia nzuri na serikali, kwa hiyo isiifanye jamii tukaiona ni mbaya na haina faida kwetu, ili twende vizuri tuhakikishe walimu wanaofundisha tunawajengea mazingira mazuri. Vile vile na wanafunzi wanaosoma madarasa haya tuwajali.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie katika Bodi ya Ushauri. Katika Mswada huu kuna Bodi ya Ushauri, katika maelezo ya Mhe. Waziri alizungumza mengi ambayo yamejumuishwa na katika bodi mbali mbali zimejumuishwa watu kutoka katika taasisi mbali mbali. Niongezee kwa kusema kwamba, katika Bodi ya Ushauri ni vyema akaingia mjumbe kutoka taasisi za watu wenye ulemavu. Kwa sababu katika skuli zetu kama tunavyosema kuna watu wenye ulemavu wanakuwa na changamoto zao mbali mbali, lakini anayevaa kiatu ndiye anayejua namna gani au kiasi gani kinambana. Kwa hiyo, yeye ndiye atakayeweza kueleza lile tatizo ambalo linawakwaza wanafunzi wenye ulemavu au zile changamoto ambazo

zinawapata watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, ni vyema tukawashirikisha na wao katika zile bodi zetu za ushauri, ili na wao wakaweza kuleta yale ambayo wanayaona wao kwa ajili ya maendeleo ya wote.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii na baada ya hayo machache naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Mimi ningeomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nafasi hii kuweza kuchangia Mswada huu wa Elimu.

Vile vile nikushukuru sana na wewe kwa kunipatia nafasi hii ili kuweza kuchangia kidogo. Mimi nitachangia kwa ufupi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chaani walionituma nitaanzia na vipengele kama vinane hivi, lakini nitaenda kimoja baada ya kimoja kwa ufupi.

Mhe. Naibu Spika, suala la elimu ni suala zuri hakuna anayelikataa, ikiwa ni dini ya dunia na akhera elimu ni kitu muhimu kwa watoto wetu na sisi wenyewe kwa sababu elimu haina mwisho. Kama tunavyoona kuna wazee wanaendelea kusoma mpaka leo, na kuna watoto na vijana wanazidi kusoma, lakini tufahamu kwamba ili elimu tuiweke katika hali nzuri basi na nchi yetu kwanza tuhakikishe kwamba hata hizo skuli ziwe katika *standard* nzuri, hatuwezi kwenda kila siku tukatengeneza *plan* nyengine nzuri lakini huku skuli sio nzuri.

Siilaumu serikali, serikali inajitahidi sana lakini kutokana na kuwa skuli ziko nyingi, mambo mengi, ningeomba sana kwanza wizara inge-*focus* zaidi kwenye kuweka *standard* ya skuli na *standard* inayotakiwa kuwa mwanafunzi anaweza akasoma bila ya kupata matatizo. Kama tunavyoona hali ya nchi ilivyo skuli nyingi tulizonazo zina matundu katika mabati, wanafunzi wakati wa kusoma siku za mvua hakukaliki wanatoka nje au wanahamishwa kwenda darasa jengine.

Sasa vitu kama hivi elimu hata tuipandishe vipi tulete walimu ikiwa wenyewe wazalendo, ikiwa Wazungu au Wachina hakutosomeka kitu bila ya skuli kuwa katika hali nzuri. Ningeomba sana wizara kupitia Waziri muhusika ahakikishe kwa nguvu zote, na niishauri sana serikali kwamba iangalie haya majengo yaliyobakia, mengi wameshajenga nawashukuru sana, na niwapongeze kwa ujenzi wanaoufanya wa skuli na mambo mengine, lakini pia na skuli nyingi alizojenga Mhe. Rais wa Awamu ya Mwanzo, Mhe. Abeid Amani Karume ziko katika hali mbaya. Sasa ningeomba zile zishughulikiwe angalau kuzibwe

kwanza yale matundu, wapigiwe plasta kama nilivyozungumza kwenye Baraza lililopita. Serikali kama kwa sasa hivi haina uwezo wa ma-*desk* basi tununue mabusati tuwawekee kwa muda, sio vibaya, kuliko kukaa chini na kuna mashimo matupu, ni mtihani.

Vile vile, niende kwenye suala langu la pili kuhusu maslahi. Maslahi ya walimu sio mazuri. Walimu elimu wanazo lakini walimu wengine watapokuwa wanasomesha wamekuwa kama wanaumwa kwa sababu maslahi yao bado sio mazuri. Ningeomba sana kwa sababu nchi nyingi sana madaktari na walimu maslahi yao yanakuwa mazuri, sisemi kama wapandishiwe kama nchi nyengine, lakini angalau wangefikiriwa na wao wakajiona kuwa wanakumbukwa kuliko ofisi nyengine. Utakuta ofisi kama za mapato za muhimu zina mishahara mizuri lakini kwenye walimu mishahara yao mara nyingi huwa hawakumbukwi sana.

Ningemuomba Mhe. Waziri ili elimu izidi kupanda, kwa sababu elimu haipandishwi tu hivi hivi mpaka walimu na wao watoe elimu ambayo kwa nafsi yao wameridhika ndio elimu itakuja; bila ya mapato mazuri kushughulikiwa na wao na vipi watizamwe na wao katika hali nzuri, basi na elimu itakuwa nzuri, la sio hivyo kama hatukukaa na walimu vizuri katika njia iliyokuwa safi kabisa na elimu pia itazorota katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, suala langu jengine ni kuhusiana na kubadilisha mifumo. Mifumo mara nyingi katika nchi yetu inabadilika mara kwa mara na hii ita-*confuse* hata wanafunzi katika masomo yao; muda si muda utakuta mambo yanabadilishwa, muda si muda mambo yanaletwa mengine. Sasa hii mimi ningeomba kuwe na *stability* ambayo itawekwa kwa miaka kama mitano, haiwezi kubadilika au kama kuna mabadiliko basi yawe madogo madogo tu, lakini utakuta kila baada ya muda kuna mabadiliko. Leo tumepanga hivi baada ya miezi mitano, mwaka mmoja mambo yanabadilishwa katika elimu, ile itachanganya wanafunzi kwa sababu skuli ziko nyingi, mambo yako mengi, na kila kitu kinataka kiwekwe hivyo, iwe muda mrefu angalau watu wapate wafahamu, hii itaepusha kuchanganya wanafunzi na vile vile kuchanganya mambo mengine katika suala la elimu.

Suala la nne, wazee wengi watoto wetu hatuwaanzishi *nursery* tunawarukisha tu darasa la Kwanza kwa kutaka kwenda kusoma kuepukana na elimu ya chini kabisa. Ningeomba sana waziri akahamasisha kwamba wazee wakawaingiza watoto kuanza *nursery* ili kupata elimu nzuri. Kutokana na huu mfumo unaotaka kuletwa utasaidia sana, hata tukiamua kusema kwamba tunataka *STD. VI* kwenda *Form I* itakuwa ni suala zuri, kwa sababu tayari watoto

wameshapitia *nursery* na kuendelea na masomo mengine, lakini leo *nursery* watoto hawasomeshwi wanaingizwa *STD I,* matokeo yake elimu inazorota, inachukua muda mrefu na baadae linakuja kuwa tatizo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokwambia kwamba leo nitachangia kwa ufupi sana, suala langu la sita ni suala la *STD VI* kwenda *Form I*. Mheshimiwa mimi ningependa kujua ni mfumo gani ambao wao wamehisi ni mzuri wa kufuata utaratibu huu wa kuwepo *STD. VI* na baadae kuruka kwenda *Form I?* Kwamba hakuna darasa la saba. Kwangu mimi naona ni suala zuri lakini tunaona wenzetu.

Nitatoa mfano mdogo kwa nchi zilizoendelea ikiwa za Ulaya au nchi nyengine, mtoto mdogo keshamaliza *PhD* ana miaka 18, miaka 21 keshakuwa *professor*, lakini ukiangalia nchi za Afrika kutokana na yale masomo yanakuwa miaka mingi unakuta mtu anafika mpaka miaka 40 ndio anaikamata *PhD* tofauti yetu ndio hiyo.

Mhe. Naibu Spika, leo ukienda *university* nchi za wenzetu, ukienda katika *college* watoto wadogo miaka 17 au 18 ana *degree*, *master* mtoto miaka 20, lakini kwa masomo yetu ya Afrika sifikirii kama mtu ataipata miaka 20 *masters* akisoma Afrika. Lakini kwa muundo huu mimi naupongeza sana naamini kwamba wamepata utaratibu mzuri na wamepata mawazo ya watu wengi wenye elimu, na vile vile hawakuchukua tu kwenda ku-*copy* sehemu badala yake wamefanya utafiti wa kutosha kuhakikisha kuwa hili suala wanalolipendekeza litakuja kusaidia elimu nchini kwetu Tanzania pamoja na Zanzibar kwa ujumla.

Vile vile, kuna suala la lugha kama Mhe. Simai Mohammed Said alivyoligusia kidogo, wazo zuri sana na mimi nalichangia kama ni mtu wa pili hapa. Elimu kusomeka lugha ya Kichina, Kifaransa, Kiingereza na Kiswahili; lugha yetu muhimu isije ikasahaulika, tusije tukaegemea kwenye lugha nyengine lakini itiliwe mkazo pia na lugha ya Kiswahili katika skuli zetu na iwekwe *priority* nambari moja, kwamba inasomeshwa na wanafunzi wahakikishe kuwa wanasomeshwa. Hizi lugha nyengine za Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kichina ni vizuri zaidi, kwa sababu ukiangalia hivi sasa nchi nyingi zinazozungumza lugha nyingi Kifaransa kimo, Kiarabu kimo pamoja na Kichina. Hilo nimeligusia la Mhe. Simai Mohammed na nampongeza sana kuliingiza.

Mhe. Naibu Spika, suala langu jengine skuli ambazo zinaleta maombi ya kutaka kufungua skuli basi zifuate maadili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na masharti na sheria zake, hasa zile zenye dini nyengine.

Kwa ufupi mwaka uliopita Mheshimiwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya sasa hivi ni Mkuu wa Mkoa Mhe. Ayoub Mohammed Mahmoud aliikamata Skuli ya *Eden International*, skuli ambayo inasomesha wanafunzi Waislamu, Wakristo, lakini matokeo yake mule ndani wakawa watoto wa Kiislamu wanafundishwa mambo ambayo sio ya dini yao. Sasa ningeomba sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali hili suala alifuatilie, alihakikishe kwa sababu zile skuli ambazo zinasomesha mambo mengine basi tusijaribu kuwaingiza wanafunzi ambao dini yao ni nyengine wakawapeleka kwenye masomo ya dini nyengine. Kuna mfano nimeutoa siku ile ile na mpaka kwenye televisheni ilizungumzwa na ilitaka kufungwa kwa maana ya kwamba imevuka masharti iliyopewa, lile lengo ambalo wameomba silo wanalolifanya.

Sasa ningependa sana kila mmoja na dini yake na kila mmoja aheshimu dini yake. Sote tunapenda dini zetu, hakuna anayembagua mwenzake, lakini kwenye masuala ya dini basi mtu asijaribu kumuingiza mwenzake kwa ile dini iliyokuwa sio yake mpaka labda atapotaka mwenyewe.

Vile vile, suala langu la mwisho ningeomba sana elimu zifanane, kwa sababu ukiangalia hapa Zanzibar zipo skuli nyingi lakini utapokwenda utakuta *syllabus* tofauti, hawa wanasomesha vyengine, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanasomesha masomo mengine; tungejaribu sana masomo yakawa yanafanana au kama wanapangiwa basi yale masharti yawe yanafuatwa kwa pamoja, isiwe hawa hivi, hawa vile, au skuli hii labda inasomesha Kiswahili hii hawataki Kiswahili. Vitu kama hivyo ningependa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ikasimamia haya mambo kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kwa leo sina mchango mkubwa lakini ningependa sana kumsifu Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mhe. John Pombe Joseph Magufuli kwa bidii yake kubwa ya kuchangia madeski pamoja na kutaka elimu ije kwa nguvu ndani ya Tanzania. Nampongeza sana kwa jitihada yake aliyoanza nayo bila ya ubaguzi pamoja na visiwa vyetu vya Zanzibar Unguja na Pemba kutuletea madeski.

Vile vile nampongeza sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein pamoja na Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Idd kwa nguvu zao zote na wao wanazojitolea kuhakikisha kwamba elimu inakuwepo na vifaa vinapatikana.

Mimi nashukuru sana na ninaukubali mswada huu na ningependa baadae Mhe. Waziri aje anipe maelezo ya baadhi ya vitu nilivyoviuliza. Ahsante sana.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi mchana wa leo kunipa fursa ya kuweza kuchangia machache kwa mswada huu ambao upo mezani, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu hapa Zanzibar.

Vile vile napenda nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) kwa kutujaalia bado tukiendelea kuwa na afya njema na tukiwa tunatekeleza majukumu yetu kwa mujibu wa sheria na kanuni ambazo zinatuongoza.

Aidha, nichukue fursa hii fupi kuwashukuru sana wapiga kura wangu katika Jimbo la Micheweni kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kunifanya mimi leo nisimame hapa kwa ajili ya kuja kuwasemea yale ambayo yanawahusu.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja mimi mchana wa leo sina mengi nitazungumza mambo machache. Kwa mfano, nataka niende moja kwa moja katika kuchangia kwa kuanza na kazi za taasisi ambazo zimeainishwa hapa.

Mimi niseme kwamba, kwa ujumla nakubaliana nazo kwamba Mhe. Waziri pamoja na watendaji wenzake wamejitahidi sana katika kuupanga huu mswada, ambao kwa kweli dhamira yake ni kutaka kuisaidia nchi yetu katika suala zima la kuongeza ufanisi zaidi katika upatikanaji wa elimu.

Sambamba na hilo nilitaka niseme kwa ujumla kwamba kazi zilizoainishwa ni nzuri, lakini kubwa zaidi mimi ninachotaka kuboresha zaidi ni kuhimiza kwamba kupanga na utekelezaji ni vitu viwili tafauti. Kama hivyo ndivyo, ningeomba sana kwamba hili linaweza likafanikiwa sana iwapo kwanza pia na ofisi zinalazimika kuona kwamba yale ambayo yamepangwa yanaweza kusimamiwa kwa vitendo, na kuona kwamba kila mmoja anafanya kazi na kuangalia wajibu wake na majukumu aliyopangiwa.

Lakini kwa mfano kuandaa mipango ya kufundisha na kusaidia ufundishaji kwa walimu. Kwa kweli ukiangalia katika nchi yetu ya Zanzibar historia ya hapa ambapo labda tumetoka na sasa hivi tulipo ni kwamba unaweza ukahisi kwamba kuna tafauti. Tafauti hizi mara nyingi sana unaona kwamba sisi tumeona kwamba tumepiga hatua kwa kiwango fulani katika kuboresha mambo mbali mbali, ni kweli, lakini pamoja na kwamba juhudi hizi ukiangalia kwa ndani zaidi unaweza kukuta kwamba mambo kwa upande mwengine hayaendi

kama vile ambavyo yametarajiwa na serikali katika kuona kwamba suala zima linafanikiwa.

Nasema hivi kwa sababu gani, sasa hivi ukiangalia unaweza ukakuta kwamba wapo ambao wamesoma vizuri zaidi ukilinganisha na miaka ya nyuma. Lakini ukija katika uhalisia basi unaweza ukamkuta mwalimu ambaye ana digirii ya kwanza mfano, lakini ukimlinganisha na mwalimu ambaye amemaliza darasa la kumi na moja katika kipindi cha nyuma unaweza ukamuona kwamba anaweza kufanya kazi vizuri na katika kusaidia katika masuala ya kufundisha watoto katika ufahamu lakini na mipango mingine.

Sasa hili mimi naomba kwamba Mhe. Waziri tujitahidi kwamba hili tulisimamie kwa dhati kabisa, kwa sababu itakuwa mipango yetu tumeshapanga vizuri lakini tusije tukafeli katika upande wa pili katika utekelezaji wake. Huo ndio ukweli, kwa kweli ukiuangalia kwa kiasi fulani unaweza ukaukuta katika mazingira yetu.

Vile vile katika suala zima la kushauri kutekeleza sera za tafiti kuhusiana na mitaala na uboreshaji. Hili ni jambo ambalo kwa kweli ni vyema tulipe kipaumbele, kwa sababu ambazo kama nilivyozitaja kwamba hili linaweza kwa upande mmoja linatuathiri kwamba unakuta mabadiliko yanafanywa mara kwa mara, kwa mfano sasa hivi Wizara ya Elimu ukiangalia unakuta kwamba walimu ambao walikuwa wanapatiwa mafunzo ya kufundisha katika ngazi ya *certificate* sasa hivi nadhani tunaenda moja kwa moja tunaanza na Diploma.

Sasa nadhani kuwepo kwa taasisi katika mambo haya inaweza ikawashirikisha wadau na kuweza kuona kwamba hili nalo linaweza likaathiri katika ufaulu mzuri wa watoto wetu katika masomo yao. Sasa nadhani kwamba mambo kama haya yanaweza yakasaidia zaidi katika kuona kwamba tunaweza tukafikisha nchi hii katika mahali ambapo pako salama zaidi katika suala zima la elimu.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika hii Bodi ya Ushauri. Bodi ya Ushauri nimeona kwamba kuna wadau mbali mbali ambao wameshirikishwa katika suala hili ambao ukiangalia kwa upande mmoja wote ni kwamba ni muhimu sana na wanaweza wakasaidia. Lakini mimi ningependa nishauri kwamba mdau mmoja kuona kwamba na yeye kuweza kuingia. Kwa mfano ukiangalia kuna Mwenyekiti ambaye ametueliwa na Rais, kuna Mkurugenzi wa taasisi, kuna Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani la Zanzibar, kuna Mwakilishi kutoka Jumuiya ya watu wenye ulemavu, kuna Wawakilishi wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Mwakilishi kutoka Jumuiya za Skuli binafsi na Mwakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Wafanyakazi.

Hapa mimi ningeshauri kwamba sijui ni kwa nini Mhe. Waziri hakuona umuhimu kwamba watu ambao wako katika Jumuiya inayoshughulikia masuala ya Elimu (ZATU- Chama cha Walimu), kuweza kuingizwa katika bodi hii kwamba ikawa nao ni watu ambao wangeweza kusaidia katika kushauri jambo hili.

Sasa ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kwamba ni kwa nini zaidi pia hatukulizingatia kwa kina zaidi. Kwa sababu mimi nilifikiria pia na wao ni watu ambao wanaweza wakasaidia sana katika kufanikisha jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, mwisho katika zile sifa ningeshauri kwamba pamoja na sifa zote hizi au pamoja na kwamba sifa ambazo tunazihitaji lakini sambamba na hili tusimamie sana katika suala zima la uzalendo katika kutekeleza mambo kama haya, kwa sababu kweli ukiangalia sasa hivi taasisi mbali mbali unaweza kukuta kwamba watu ambao wanaweza kufanya kazi nzuri wapo lakini hatimaye kwa kuwa wamekosa jambo dogo la uzalendo inafika wakati tunafanya mambo yanaenda sivyo ndivyo.

Kwa hiyo, ningemuomba Mhe. Waziri na hili pia katika kufanikisha mswada huu nalo pia lingetolewa ufafanuzi. Pamoja na mswada huu kwamba ni mzuri, lakini bado kuna changamoto moja ambayo inaweza pia kuzorotesha katika ufanisi wa jambo hili, kwa mfano miundombinu tuliyonayo sasa hivi kama majengo yetu ya skuli kama ambavyo wajumbe wameweza kuzungumzia unakuta bado hayajaturuhusu ipasavyo.

Kwa mfano sasa hivi ukiangalia sera na mipango ya wizara ni kwamba sasa hivi mwanafunzi ili aanze skuli ni kwamba anatakiwa aanze elimu ya maandalizi. Lakini ukienda katika skuli mbali mbali hapa nchini unakuta bado suala hili halijafanikiwa ipasavyo kwa sababu bado katika skuli husika bado hata hilo jengo au sehemu ya kuwaweka wanafunzi hawa wa awali bado hawajapata sehemu za kuwaweka.

Kwa hiyo, kuwepo kwa mswada huu na hii taasisi ambayo itaundwa nadhani pia kunaweza kukasaidia katika kufanikisha na kuandaa mipango mizuri na kuona mambo kama haya yanaweza yakafanikiwa. Lakini niseme kwamba sambamba na hilo taasisi nadhani pia sina wasi wasi nayo Mungu akipenda utapita mswada huu, lakini ningeomba sana sambamba na kufanikisha hili zile fedha ambazo zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu katika taasisi ni jambo la msingi sana, kwamba zipatikane kwa muda muafaka, kwa sababu pia endapo kama hili linakuwa kama vile utaratibu mwengine baadhi ya wakati

linaweza likapelekea kwamba pia taasisi hii isiweze kufanyakazi vizuri na hatimaye kuja kufika wakati kwamba tukaja kutafuta namna ya kuleta mswada mwengine ambao kutokana na changamoto ambazo zimejitokeza.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba kwa leo haya yanatosha, na mimi nipongeze sana mswada huu ni mzuri lakini pamoja na uzuri wake ningeomba yale ambayo nimeyashauri kwa upeo wangu tuweze kuyazingatia na Mhe. Waziri kwa yale ambayo nimetoa kama ushauri basi ningependa zaidi kupata ufafanuzi kwa yale ambayo nimeyauliza.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na salama na wewe kuniruhusu na mimi nichangie alau kidogo katika mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi niseme kwamba mswada huu ulioletwa mbele yetu naona ni mswada mzuri ambapo una malengo mazuri kwa ajili ya nchi yetu na kwa vizazi vyetu ambavyo vinakuja, kwani mara nyingi sana tulikuwa tunapiga kelele kwamba baadhi ya mambo tunaburuzwa. Lakini sasa leo tukiwa na chombo kama hichi tunaweza kufanya mambo yetu tukijitegemea kama tunavyoendelea na mambo mengine, na yale yatakayobaki ya umoja yatabaki ya umoja na yale ambayo yatakayokuwa ya kwetu yatabaki ya kwetu.

Lakini pia chombo hichi ninavyoona mimi Mhe. Naibu Spika, kitaweza kuwapunguzia mzigo wale watoto wetu pindi ikiwa kitafanya kazi chombo hichi. Kwa sababu suala zima la mitaala lilikuwa baadhi ya walimu wanalipigia kelele kwamba mitaala inayotumika Zanzibar sio kama vile inayotumika kule Tanzania Bara hasa wakati wa mitihani unakuta kwamba wanapiga kelele kwamba mitihani inayotolewa sisi hatujasomeshwa, na kwa kweli walimu wanasema hivyo baadhi yao na wanafunzi wanathibitisha. Kwa sababu mtu anakwenda mpaka anafanya mtihani somo lile anakwenda unakuta kwenye *paper* tu kama darasa la 12 hii inatokana kwamba wenzetu kule Tanzania Bara tayari wana mtaala wanafuata na sisi huku tunafuata mwengine. Lakini kwa kuwepo kwa chombo hiki kitaweza kusimamia na kufanya utafiti mzuri kipi kitatufaa.

Vile vile chombo hiki ambacho tutakiunda ni miongoni mwa matakwa ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki ambayo kwa mara nyingi sasa tunafanya kazi kwa pamoja, na ni karibuni hata ajira zinatangazwa katika Jumuiya hiyo. Kwa hivyo, ni matakwa ya jumuiya ya Afrika Mashariki tunakwenda nayo basi

ni vyema na sisi tukaweza kujitengeneza na kujiandaa ili watoto nao wakaweza kufaidika na chombo hiki, baada ya kuwa tukae tu kila mmoja anakuja na utaratibu wake uliokuwa hauna msingi maalum.

Pamoja na kuwa chombo hichi tunacho lakini kuna jambo ambalo linatukwaza kidogo nalo ni jambo ambalo kuwa kama hatukuwa na mpango kama huu wa kuwa na chombo hiki wa kubadilisha badilisha wa kupitia misaada, misaada wanayotupa wafadhili hii baadhi ya vifaa mfano unaweza ukatoka nchi fulani ikaisaidia Zanzibar hapa vifaa vya elimu tayari tunaambiwa tufate mtaala huo. Leo ni kumbebesha mzigo mzazi kitu ambacho nyuma ilikuwa unaweza ukanunua kitabu ambapo mtoto wa darasa la tano au wa hivi sasa anaweza akakitumia na anayefuata nyuma anakitumia. Lakini kama leo utanunua vitabu vya laki moja ikifika miezi miwili unaambiwa havitumiki tena hivyo. Kwa kweli ni mzigo kwa wazazi ambao ni wakwezi na wakulima ndio walio wengi. Kwa hivyo, tukiwa na mitaala yetu tutajua kwamba huu kwa muda gani utatumia hatutakurupuka kwa kufuata misaada tu.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Naibu Spika, nauunga mkono sana mswada kama huu uendelee kuwepo, lakini tuchungue sana mambo ambayo tutaona kwamba yatatuharibia nchini mwetu. Lakini naomba sana taasisi hii ambayo tutaiunda kuna jambo ambalo tunalipigia kelele kwa kusema tu, tunasema *tutunze kilicho chetu*. Lakini sio kweli hatutunzi vilivyo vyetu, kwa mfano ni lugha yetu ya Kiswahili. Lugha yetu ya Kiswahili sisi wenyewe tunaidharau, lakini kimataifa sasa kila kukicha naona inaendelea kupata chati.

Sasa hili ni jambo ambalo taasisi hii tunayoiunda iangalie sana sana kuweza kutunza hichi chetu tulichokamata. Leo kila mmoja hapa anayeanzisha skuli hapa unasikia anaanzisha lugha ya Kiingereza, Kigiriki lakini hazungumzi lugha ya Kiswahili wakati kimataifa sasa inaambiwa izungumzwe hata Kiswahili, kwa nini iwe hivyo? Naomba sana taasisi hii iangalie hata mwanafunzi ambaye alikuwa anapasi Kiarabu na Kiswahili basi unakuta anadharaulika kwa humu mwetu, lakini akitoka nje mtu huyu anapata thamani. Kwa hivyo, naomba sana hii taasisi itakayoundwa iwe nayo inaangalia hichi chetu nacho tunakithamini.

Lakini jambo lolote linataka na mwanzo mzuri, skuli zetu ambazo tunaanza nazo sasa hivi zinakabiliwa na matatizo kama hayo wenzangu walivyosema ya Skuli za Maandalizi baadhi yao Skuli za Maandalizi zipo jirani ambazo zimeundwa na jamii kwa mfumo huu tunaokwenda nao uwepo wa karibuni nimeuona kwamba hizi skuli za jamii za maandalizi zinaanza kupigwa chenga, kwa sababu huku nyuma ilikuja kuambiwa kwamba skuli ambapo ipo ya jamii

basi isianzishwe skuli ya serikali ya maandalizi pale. Leo zinaanzishwa na utafiti wangu nilipoangalia nakuta wale watoto kule wanafika hawana walimu, walimu ni wale kule kwenye skuli za jamii, kule wanaendelea tu kuvishwa sare zile wakaenda wakakaa hakuna elimu yoyote wanayoipata baadhi yao nasema, skuli za jamii zinaendelea.

Kwa hivyo, hichi chombo kitakachoundwa ziangalie sana hizi skuli, mimi ninao mfano uko hai nauangalia kwa sababu ni miongoni mwa wasimamiaji wa skuli zetu zile za jamii zimekuwa zikitoa wanafunzi wazuri mpaka hivi sasa ndio wanaosomesha Vyuo Vikuu toka zilipoanzishwa skuli zile. Lakini serikali ilikuwa inaanza kuzipiga chenga kwa kuanzisha hizi skuli za serikali naomba sana chombo hichi nacho kiangaliwe.

Kwa upande wa wale walimu kuziangalia kwa kila hali kwa mitaala na maslahi, walimu wale hawana ajira huu ni karibu mwaka wa 20 au 15 wanaendelea kujitolea, na kama jamii tunavyoiona ukimwambia shilingi 2000 kwake ni mzigo, yuko tayari aambiwe pale ni bure lakini hapati chochote ni bure bure. Kwa hivyo, hili jambo tuliangalie sana, jamani hawa walimu tuwaangalieni na hizi skuli tuziangalie ili tuweze kupata kitu tulichokikusudia, chombo ambacho kuwa kinaweza kutuletea mafanikio na skuli hizi tuziangalie vizuri sana tusije tukazipuuza.

Kwa hivyo, imani yangu kwamba mimi kama tunataka tupige hatua miongoni mwao basi na hizi skuli tuziangalie pamoja na kuboresha baadhi ya mambo ambayo ni vikwazo kwa hivi sasa, kama wingi wa wanafunzi madarasani tutafute namna wananchi wahamasishwe baadhi ya mambo kuchangia, tusiiachie serikali peke yake na sisi wenyewe tuchangie baadhi ya mambo kwa huo huo unyonge wetu. Kwa sababu leo utashangaa mtu anakwambia sina fedha anamtoa mtoto pahali panaposomeshwa Skuli ya Maandalizi shilingi 2,000 anampeleka Skuli ya kulipia ya Maandalizi shilingi 15,000 au 50,000 na walimu waliotolewa pale wanaokwenda kusomesha kule ni wale waliotoka skuli hizi za maandalizi ya jamii lakini yuko kule. Kwa hivyo kumbe ukitizama uwezo wa kuchangia tunao lakini moyo tu ni mdogo. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, na mimi naona mswada huu na mimi naomba tukubali na naunga mkono sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuna mchangiaji mmoja wa mwisho ambaye atapata nafasi ya kuchangia tutakaporudi jioni, na baada ya hapo Mhe. Waziri atakuja kujibu hoja mlizozitoa na nina ombi kwenu kwamba leo jioni saa 11:00 Waheshimiwa Wajumbe tufike mapema kwa sababu kutakuwa na shughuli ya kupitisha vifungu.

Kwa hiyo, ningekuombeni sana mje mapema, kwa sababu kanuni inatutaka tuwe katika idadi maalumu ya kupitisha vifungu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe hilo ni ombi langu natarajia mtafanya hivyo, kwa hiyo niseme naahirisha kikao hadi leo jioni saa 11:00.

(Saa 6: 54 Mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mchangiaji wetu mmoja aliyebakia alikuwa ni Mhe. Omar Seif Abeid na....

Mhe. Omar karibu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Mswada huu wa Elimu na kuweza kutoa mchango wangu mdogo kwenye mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza sitaki nipoteze muda, ninataka niende moja kwa moja kwenye mchango kwamba ninaungana na wenzangu waliotangulia kuupongeza Mswada huu kwamba umekuja kwa wakati unaostahiki. Lakini pamoja na pongezi hizo kwamba Mswada huu umekuja kwa wakati, hatuna budi pia kuikumbusha Wizara inayohusika na mambo ya elimu (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali) kuangalia mambo ambayo bado ni kikwazo katika elimu yetu.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyofahamu sisi tupo katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Zanzibar sisi ni miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Watoto wetu wanafanya kazi kwenye Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwenye soko hili la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, lakini kwa kweli kiwango chetu cha elimu Mhe. Naibu Spika, bado hakijaridhisha, na ninasema hakijaridhisha kwa sababu gani.

Mhe. Naibu Spika, tukikosa kiwango kizuri kwa sababu Waswahili wanasema kwamba, "*Mti mzuri huzaa matunda mazuri*". Na ili elimu iwe bora na iwe nzuri yenye kiwango kinachoridhisha ilitakiwa mtoto umuandae kutoka elimu ya maandalizi. Pale unapopata kumfinyanga mtoto ukamuendeleza mpaka akawa mzuri.

Sasa utakuta tatizo hili kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ninavyoliona mimi kwamba wengi wa wanafunzi wetu au watoto wetu wanaosomeshwa katika *nursery* walimu wengi wao hawana viwango vinavyokidhi kusomesha hata hiyo *nursery*. Na haya utayaona wakati utakapochukua *nursery* zetu za serikali na *nursery* za watu binafsi wanazofundisha. Sasa huwezi kupata matokeo bora ya elimu ya msingi na elimu ya juu ikiwa elimu ya msingi au elimu ya chini hukuweza kuianzia katika kiwango kilicho bora.

Sasa wito wangu mimi kwa Wizara, waanze kujipanga kutafuta walimu bora kuanzia kiwango cha *nursery*, waweze kuwalea watoto wetu ili nao wanapoingia kwenye skuli ya msingi, wanapoanza darasa la kwanza wawe tayari wameshapata yale mafunzo mazuri ya elimu ya *nursery*. Na halikadhalika hivyo hivyo kiwango cha elimu ya msingi utakuta skuli binafsi na skuli za serikali kuna tofauti kubwa. Wanafunzi wanaosomeshwa katika skuli za watu binafsi utakuta upeo wao ni mkubwa zaidi kulikoni wanaofundishwa kwenye skuli zetu za serikali.

Mhe. Naibu Spika, tujiulize kuna nini. Mimi katika baadhi ya tafiti nilizozifanya kuhusu mambo ya elimu nimegundua kwamba kuna baadhi ya mambo ambayo yanarejesha nyuma mambo ya elimu hasa kwenye skuli zetu za serikali.

Mhe. Naibu Spika, moja kati ya mambo hayo ni upungufu wa walimu. Jambo ambalo wizara yenyewe inakiri kila siku kwamba wana upungufu wa walimu hasa wa sayansi. Lakini kila siku inakuwa ni nyimbo hatuna walimu. Sasa hebu Waziri tuambie lini utamaliza hili tatizo la walimu kwenye skuli zetu. Twambie kwa sababu na sisi tunahitaji tupate walimu waweze kufundisha watoto wetu, watoto wetu waingie katika soko la ajira la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kwa sababu tunapokwenda ni lazima *challenges* hizi watakutana nazo. Hivi sasa wamezianzia na kila tunapokwenda tunazidi kuzikuta.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema jambo la pili, pia kwa upande wa watumishi wenyewe; yaani walimu uzalendo umewashinda, moyo wa ufundishaji hawana. Pamoja na kuwa atasema kama hatuwapendi lakini wengine moyo hawana. Jambo hili mimi ninaiomba Wizara ya Elimu na ninataka akija Waziri aniambie sisi zamani tulikuwa na utaratibu skulini kila mwezi kulikuwa na Wakaguzi wa Elimu, wanakwenda maskulini wanakagua. Lakini leo baada ya kufanya utafiti wangu ni kwamba Wakaguzi wa Elimu wanaweza kutimiza miezi mitatu hawajapita skuli. Inakuwaje, kwa nini iwe

hivi. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi kwa jambo hili ninaiomba Wizara ipange mpango kazi juu ya kuwahamasisha, yaani kuwalazimisha na siyo kuwahamasisha, kwa sababu ni wajibu wao. Kuwalazimisha Wakaguzi wa Elimu na ikiwezekana ripoti za ukaguzi kila mwezi ziende wizarani, hii itamsaidia Waziri na ngazi zilizokuwepo za Wakaguzi kuweza kufahamu kama kweli ukaguzi wa walimu katika maskuli unafanyika. Hii itasaidia pia kukuza kiwango chetu cha elimu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile mimi ninachotaka chengine kukizungumza ambacho kinachangia kuporomoka kwa elimu pengine ni upungufu hasa wa madarasa. Mfano kama skuli yangu mimi ya Konde ya msingi ya "A". Kuna uhaba wa madarasa, uhaba wa walimu. Skuli ina watoto 1,375, ina walimu 20, ina mabanda manne. Unategemea utapata nini hapo Mhe. Naibu Spika, huwezi kupata kitu, huwezi kupata ufanisi. Matokeo yake wanafunzi wanarundikana wengi, walimu wanasomesha zaidi ya wanafunzi mia. Kukagua mabuku pia kwa walimu inakuwa dhiki hawawezi. Matokeo yake wanafunzi wanaendelea kufanya vibaya siku hadi siku.

Sasa Mhe. Waziri katika majumuisho yako pia ninataka ukija uniambie. Tulikuwa na banda moja lililozuiliwa na Wizara kwa ajili ya kuongezea pale Konde msingi "A", mpaka leo bado na jengine limevunjwa kabisa. Sasa ninataka ukija katika majumuisho yako uniambie Wizara itamaliza lini mabanda yale ili kupunguza ule msongamano wa wale wanafunzi na lini utanipa walimu, utaniongezea walimu katika skuli ile, ni kilio. Hivyo naomba katika majumuisho yako uje uniambie lini suala hili Mhe. Waziri utalisaidia kupunguza hilo tatizo.

Pia mimi sitaki kwenda mbali sana lakini ninataka niende kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Mhe. Naibu Spika, ninarudia tena kusema kwamba uzalendo katika nchi yetu sisi unatushinda. Serikali inatumia pesa nyingi sana kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi wanaosoma kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu. Waziri alipokuwa akijibu baadhi ya maswali kwenye hotuba yake ya bajeti, alisema kwamba kwenye bilioni 21 zilizokopeshwa ni bilioni 1 na nukta kadhaa ambazo zimerejeshwa hadi sasa. Hii ni dhahiri kwamba serikali inabeba mzigo mkubwa wa deni la kuwasomeshea watu hao. Lakini baada ya kusomeshwa hakuna faida inayopatikana kwa wale wanaosomeshwa, hawana uzalendo. Lau kama ingelikuwa kuna utaratibu wa watu wanapotoka Vyuoni wakajitolea kusomesha ndani ya zile skuli walizotoka tu angalau, basi tatizo la walimu lingekuwa hakuna. Kwa sababu mwaka huu wangetoka hawa, mwakani wakaja hawa na serikali tungeiomba ikaandaa huu mpango angalau wa posho kidogo la kusaidia wale wanaofundisha, lakini hakuna tofauti na wenzetu.

Kule Marekani wanafunzi wao wanapomaliza Vyuo Vikuu wanatolewa nchi mbali mbali kwenda kujitolea. Sasa hebu jamani tufikirini nchi kama Marekani inatusaidia sisi kutuletea walimu hapa kwetu. Watoto wetu ambao wamesomeshwa, wamepewa pesa na serikali hii wanashindwa kuwasaidia wenzao ambao ni ndugu zao wao wenyewe.

Sasa Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri mimi ninataka wakati utakapokuja uje uniambie. Je, huoni kwamba ipo sababu sasa ya watu wanaopewa mikopo ya elimu ya juu kuwekewa masharti kwamba munataka mkopo lazima ujitolee kwenda kufundisha baada ya kumaliza masomo, ili kupunguza hii *gap* ya kuwa na walimu hasa wa sayansi au hata na walimu wa masomo mengine.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika nne jikusanye vizuri umalizie.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba Wizara kwa sababu ina wataalamu, ushauri huu watauchukua waufanyie kazi ili kutupunguzia kile kilio cha kusema kila siku kwamba tuna upungufu wa walimu, vyenginevyo muwawekee masharti watu wanaohitaji mikopo. Ikiwa hawezi kukubaliana kwenda na masharti hana haja ya kupewa mkopo, kwa sababu mkopo ule ni wa wananchi wote wa Zanzibar, ni wa Wazanzibari wote wavuja jasho, maskini za Mungu. Anayekwenda kupata mkopo ule unamnufaisha yeye na familia yake.

Tumeshuhudia kwamba wengi baada ya kumaliza muda wa masomo yao, wanakimbilia kwenye soko Tanzania Bara, inakuwa serikali yetu na wananchi waliotoa mchango ule wanapata hasara. Kwa hivyo kwa sababu nimeambiwa muda umekwisha Mhe. Naibu Spika, mimi ninaunga mkono hoja ya Mswada lakini ninataka Waziri akija aje anijibu hayo masuala yangu ili na mimi niridhike na wananchi wangu wajue wa Jimbo la Konde lini tatizo lao litaweza kutatuka.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe nimepata wachangiaji watatu wa nyongeza. Nitawapa fursa hiyo kuchangia kwa dakika kumi kumi kila mmoja, na baadae nitamuomba Mhe. Balozi Amina na yeye atakuja kuchangia kwa upande wa Mawaziri na baada ya hapo Mhe. Waziri atakuja kujibu hoja.

Sasa ninamwita Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuniona kunipa nafasi hii ya kuweza kuuchangia Mswada huu wa Kuanzishwa kwa Taasisi ya Elimu hapa Zanzibar.

Nianze na kutoa shukurani kwa Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuweza kuwasilisha Mswada huu muhimu, ambao umekuja katika wakati muafaka pamoja na kuchelewa kwake.

Vile vile niishukuru Kamati husika kwa ripoti yao nzuri, lakini wametusaidia sana katika kufanya marekebisho mbali mbali ambayo na sisi tulikuwa nayo katika kuchangia hili. Nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wake Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini katika hilo. (*Makofi*)

Vile vile niwashukuru Wajumbe wenzangu ambao wametoa michango yao na maoni yao mbali mbali katika kuuchangia Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu ni muhimu sana na mimi kwa sababu ni mdau wa elimu nitangulize tu kuunga mkono asilimia mia kwa mia, baada ya wenzetu kuukalia kitako na kupokea maoni yetu na marekebisho ambayo tutawapa. Na nina imani kwa Wizara ya Elimu na watendaji wake ninavyowafahamu basi watawaweza kutukubalia maoni yetu na marekebisho yetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kitovu cha elimu katika nchi yoyote ni kuwepo kwa taasisi ya elimu. Taasisi ya elimu ndiyo ambayo inaratibu mafunzo yote ya ngazi mbali mbali. Lakini walimu, vifaa vya kufundishia na vyengine vinavyohusiana na suala zima la kuweza kuifanya elimu ya nchi hiyo iwe bora zaidi. Kwa hivyo suala la kuwa na Taasisi ya Elimu kwa Serikali yetu ya Zanzibar ni muhimu sana kwa wakati huu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuchelewa lakini tupo katika wakati mzuri. Cha muhimu sana Serikali iwe na udhati, Serikali yetu ya Mapinduzi na mimi ninaiamini, iwe na udhati katika kuanzisha kwa taasisi hii.

Nimshukuru sana Mhe. Waziri katika hotuba yake aliyoitoa amesifu nchi mbali mbali ambazo zina sheria nzuri za taasisi zao. Nina imani kwamba *research* imefanyika na kuweza kuona nchi mbali mbali ambazo zina sheria hii zinavyofanya. (*Makofi*)

Lakini niseme tu Mhe. Naibu Spika, kuna usemi unaosema kuwa "*Ukipenda waridi upende na miba yake*". Sisi Wazanzibari tunapenda sana waridi lakini miba yake huwa hatuipendi. Yaani tunapenda mambo mazuri ya kuiga lakini hatupendi kugharimika.

Mhe. Naibu Spika, kama tunataka kikweli kweli tuanzishe taasisi hii na iwe taasisi ambayo iwe na hadhi katika nchi yetu, basi tusiige majina tu kama tulivyoyaiga katika nchi ambazo tumefanya *research*. Lakini vile vile tuige na utekelezaji wa sheria zake. (*Makofi*)

Nchi za jirani tu kama Kenya na Tanzania Bara hapo, kama utakwenda na ukafanya ziara ya kuitazama Taasisi ya Elimu Tanzania basi ni aibu.

Leo tuna miaka minne toka tuanzishe taasisi hii, lakini taasisi hii ina gari moja tu ya Mkurugenzi, taasisi ina chumba cha Mkurugenzi na chumba cha watendaji. Maafisa na wataalamu wapo ndani ya chumba kimoja. Hii hatuwezi kwenda. Lazima tujipange vizuri, tuweze kuiona taasisi hii ina hadhi basi tuige mambo mbali mbali ili tuweze kuona kwamba taasisi yetu nasi tunaweza tukajigamba kwamba tuna Taasisi ya Elimu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri vile vile alizungumzia suala la ushirikishwaji wa wadau. Na mimi nimshukuru kwa kuwataja wadau mbali mbali, lakini nikiri tu kwamba miswada yetu mingi ina wigo finyu katika kuwashirikisha wadau, na hii nina imani kwamba, katika mswada huu wigo wake ulikuwa ni finyu.

Tuna wataalamu ambao wamesomea mambo ya mitaala, tuna walimu ambao ni wastaafu wanaelewa mambo ya mitaala, lakini tuna walimu katika vyuo mbali mbali, ushirikishwaji huu haukufanyika vizuri, nina imani hiyo tumewashirikisha wachache. Kama unataka mswada uweze kuchangiwa vizuri na kufanikiwa, basi uwe na mapana kabisa katika kuwashirikisha wadau wa aina mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, tuna wakurugenzi wetu waliongoza taasisi za ukuzaji wa mitaala, hawakushirikishwa katika suala hili, angalau kuuona huu mswada na kuuchangia. Hili natoa wito kwa serikali kwamba tunapopitisha hii miswada, tujaribu sana kupanua wigo wa kuwashirikisha wadau mbali mbali, kwa sababu tunachotaka kukijenga ni kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Naibu Spika, mimi niishauri Wizara ya Elimu na nafikiri ni sikivu, taasisi yetu ya elimu ili iwe ni taasisi ya kikweli kweli, basi kwanza tuanzie na kuwasomesha wataalamu. Taasisi ya elimu kama taasisi haiwezi kwenda kama

huna *philosophers*, taasisi ya elimu haiwezi kwenda kama huna *researchers* wa kutosha, taasisi ya elimu haiwezi kwenda kama huna *psychologists* wa kutosha, taasisi ya elimu haiwezi kwenda kama huna *evaluators* wa kutosha, lakini vile vile taasisi ya elimu haiwezi kwenda kama huna majengo, kama huna majengo huna taasisi, huwezi kuwa na taasisi ya vyumba viwili.

Mhe. Naibu Spika, taasisi haiwezi kwenda kama haina *facilities*, haiwezi kwenda, tutajidanganya, lakini taasisi haiwezi kwenda kama haina magari au vipando. Taasisi yetu hata vespa haina, unaweza vipi ukafanya *follow-up* katika maskuli kuona kwamba mtaala huu unatumika vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi niiombe serikali yangu tukufu kuweza kudhamiria kwa dhati, kuweza kuianzisha taasisi hii lakini tuiwezeshe ili kuona kwamba elimu ndani ya nchi hii inakua vizuri.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika karatasi hizi za mswada wenyewe. Katika kuchangia huku Mhe. Naibu Spika, katika suala la ufafanuzi wa maneno, kuna maneno kama *curriculum development*, kwa kweli hilo neno halikuwekwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika karatasi hizi za mswada wenyewe. Mhe. Naibu Spika, katika suala la ufafanuzi wa maneno, kuna maneno kama "*curriculum development"*. Kwa kweli hilo neno halikuwekwa vizuri, nashukuru kwamba Kamati imeliona, lakini kuna maneno kama "*instructional materials"*. Katika tafsiri za Kiswahili zilizotumika zinahitaji marekebisho, nafikiri wataalamu wangu wapo juu na hata Wakurugenzi wamo ambao wamenikuza mpaka kufikia hapa, nafikiri watakuwa wameyaona hayo mambo wanaweza kuyarekebisha.

Kwa suala zima la tafsiri ya *curriculum*, bado hiyo tafsiri iko finyu, ningependa wataalamu wa elimu wakaitazame zaidi, kwa sababu imeelea zaidi katika yale mafunzo yaliyoratibiwa skulini tu na *curriculum* ina mapana yake, hata mafunzo ambayo yako mitaani basi yanaingia katika tafsiri nzima ya neno *curriculum* kama mitaala.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo madogo madogo ya *printing mistake* au *typing errors* ambazo kamati imeziona sana hizi. Niwashukuru sana Kamati kwa kuziona, kwa sababu na mimi wamenipunguzia kazi katika hilo.

Mhe. Naibu Spika, katika ufafanuzi huu ningependa neno "vitabu rejea" basi liingie katika maneno ya kufafanuliwa. Vile vile katika ukurasa huo huo wa 39

katika kazi za taasisi. Moja kati ya kazi za taasisi ambayo sikuiona ni kuweza kutunza vifaa vya ufundishaji na kujifunzia, hii ni kazi moja muhimu sana.
Taasisi yetu ya Elimu lazima kazi hii iwenayo na lazima iwe na *store* za kuweza kuhifadhi hivyo vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Lililokuwepo hivi sasa taasisi ya elimu haina mamlaka hayo ya kuweza kutunza, na vifaa hivyo utavikuta kwanza vinatunzwa na idara ambayo haihusiani na masuala ya vifaa vya kufundishia.

Mhe. Naibu Spika, tatizo linalotokea ni wizi wa vitabu, kwa sababu Mkurugenzi wa taasisi hana mamlaka hiyo, hiyo kazi lazima iwepo, na taasisi kama itaanzishwa basi lazima vifaa vya kujifunzia na kujifundishia viwe chini ya Mkurugenzi wa Taasisi. Mkurugenzi anaelewa ni jinsi gani vitabu vinavyoibiwa na kuuzwa katika maduka binafsi. Mimi mwenyewe ni shahidi, na kuna kesi mpaka leo hazijaweza kufikia pahala juu ya wizi wa vitabu, leo tutakwenda vipi na taasisi ambayo haina uwezo wa kuweza kutunza vitabu vyake. Kwa hivyo kazi hiyo ningependa sana iingizwe katika msururu wa hizo kazi.

Lakini tukienda katika kifungu (d) cha kazi kuna neno "kuboresha", katika ile ya *version* ya Kiingereza imesema *develop*, kwa hivyo hapa hili neno haliendani, kwa hivyo liwekwe neno ambalo nafikiri ni muafaka kwa hapo, na hata waziri wangu Mhe. Haroun hilo neno hawezi kulikubali.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 41 kwenye kifungu cha 8, hapa imeorodheshwa kazi za bodi, hizi kazi za bodi nazikubali zote, lakini hazikupangika vizuri, zingepangika kwa mujibu wa vipaumbele vyake. Kwa hivyo, ningependekeza vitazamwe upya na viweze kupangwa vizuri *systematically* ili viweze kuleta mantiki. Niwaombe sana watendaji wa Wizara ya Elimu kuvitazama na kuvipanga vizuri.

Vile vile katika kifungu cha 10(2) inasomeka hivi:

Kifungu cha 10(2)
"Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi ikiwa mtu huyo ni",
napenda sana hilo neno 'ni' lije katika kifungu cha (a) kidogo iwe ni Mzanzibari, kwa sababu 'ni' hiyo haiwezi kufanya kazi katika vifungu vingine vya (b) na (c) na kuendelea. Ningependa sana ionekane hivyo.

Mhe. Naibu Spika, lakini tukija katika ukurasa wa 40 na 41 kuna neno makhususi limezungumziwa, hili neno linahitaji *consistency*, kwa sababu kuna

sehemu imeandikwa makhususi, kuna sehemu mahususi. Kwa hivyo, katika shughuli nzima hii ya huu mswada maneno hayo yangekuwa na *consistency* ikaeleweka makhususi ipi ambayo inakubalika.

Katika ukurasa wa 42 kifungu cha 13(d) kuna neno "kupitia". Kwenye *version* ya Kiingereza inasema *to review*, ningependa sana hapo neno muafaka liwe kufanya mapitio isiwe kupitia.

Vile vile katika kifungu (e) ukurasa wa 43, kuna programu za mafunzo ambapo hilo neno kwenye *version* ya Kiingereza ilikuwa ni *educational program*.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, una dakika tatu malizia.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Napenda labda litumike neno jengine la Kiswahili, ambalo lingekuwa na muktadha mzuri wa kielimu kuliko hilo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikushukuru, lakini naendelea kumalizia dakika zangu katika ukurasa wa 45 kwenye suala la jadweli kifungu cha 4. Lakini suala hili bahati nzuri wenzangu walilirekebisha, niseme tu kwamba kifungu (b) ilikuwa, "ikiwa kutohudhuria vikao". Hapo ilitakiwa isomeke kwamba "ikiwa hatohudhuria vikao".

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi uliyonipa na mimi kuweza kuichangia wizara yangu hii tukufu ninayoipenda sana. Niiombe tu serikali na wizara kuweza kuzingatia hayo.

Baada ya kusema hayo, ninasisitiza tena kwa kusema kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia, lakini marekebisho yafanyike. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Yussuf Hassan Iddi, na baada ya hapo atafuata Mhe. Balozi Amina Salum Ali; Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Yussuf Hassan karibu.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza na mimi kunipa fursa ili na mimi nitie baraka zangu katika mswada uliokuwa mbele yetu wa kuanzisha Taasisi ya Elimu Zanzibar.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu, japokuwa umechelewa, lakini tunasema umewahi. Vile vile

tumshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kwa kuweza kutupa muongozo wa namna gani tunaweza kuuchangia, hasa sisi wajumbe wapya wa Baraza hili la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba mswada huu utakapopita utaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu. Kama tunavyojua kwamba sekta hii ya elimu imekumbwa na changamoto nyingi, hasa katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia, lakini changamoto hizo nyingi zinaweza kutatuka iwapo mswada huu sisi tutaupitisha na kutiwa saini na Mhe. Rais.

Mhe. Naibu Spika, nianze kuchangia mswada huu katika kifungu cha 6(1)(d) kwa kuipongeza serikali kwa kuwaona watu wenye ulemavu na kuingizwa katika bodi ya taasisi hii. Ni dhahiri kwamba changamoto zinazowakumba watu wenye ulemavu katika sekta ya elimu zinaweza kupewa kipaumbele katika taasisi hii ya elimu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, lakini tukija kwenye ukurasa wa 41 kifungu (b) ambapo wajumbe wengine wa bodi watachaguliwa na Mhe. Waziri, naona kama haiko wazi zaidi imejifunga ni wajumbe wangapi, wanne, sita au kumi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho basi hawa wajumbe wengine waliobakia ambao wataingia katika hii bodi, basi atueleze ni wangapi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa huu huu wa 41 kifungu cha 8 kwenye kazi za bodi. Hapa mimi nina ushauri tu, kwamba bodi ni chombo kikubwa katika taasisi hii, sasa ningependekeza au ningeshauri niongeze jukumu la ufuatiliaji na tathmini, yaani *monitoring and evaluation*. Yaani chombo hiki nacho kiweze kufanya hiyo ufuatiliaji na tathmini katika shughuli zote za taasisi.

Nikiendelea Mhe. Naibu Spika, kwenye kifungu cha 10(2)(b) ambacho kimeelezea sifa za Mkurugenzi wa Taasisi, ambayo inasema kuwa, angalau awe na Shahada ya Kwanza. Lakini unapokwenda kwenye *version* ya Kiingereza hii, katika ukurasa wa 56 huku inasema angalau awe na *Masters Degree*. Sasa kuna sintofahamu baina ya huu mswada wa Kiswahili na wa Kiingereza, sasa ipi tuifuate? Ni awe na *First Degree* au awe na *Masters*. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja tunaomba tupate muongozo huo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nije kwenye ukurasa wa 42 kwenye kifungu cha 12. Katika kifungu hiki cha 12 kina vifungu vidogo 6, kifungu namba 1 mpaka kifungu namba 6. Lakini katika mswada huu wa Kiswahili kifungu namba 5 hakipo, lakini kwenye *version* hii ya Kiingereza

kipo. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri hii *error* airekebishe, ili mswada wetu wa Kiingereza na wa Kiswahili uwe unakwenda sambamba. Kwa hivyo, imeonekana kuna matatizo ya *uniformity* ya *version* ya Kiingereza pamoja na huu wa Kiswahili.

Mhe. Naibu Spika, nikiangalia vile vile ukurasa wa 44 katika kifungu cha 18, kwenye vifaa vya kufundishia, *teaching materials.* Kwenye mswada wa Kiswahili una vifungu viwili, namba 1 na namba 2, lakini *version* ya Kiingereza ina vifungu 3, upi ni sahihi. Kwenye *version* ya Kiingereza kuna 18, 1, 2 na 3, lakini huku katika mswada huu niliokuwa nao mimi, sijui kama na Waheshimiwa Wajumbe wengine mnao kama wangu, huku kuna 18,1 na 18, 2, hakuna usawa. Kwa hivyo, hii inaweza ikaja kuleta matatizo baadae. Naomba haya marekebisho yangefanywa.

Mhe. Naibu Spika, hata ukija katika utaratibu wa vikao vya bodi, kwenye kipengele cha 3, yaani ukurasa wa 45 kifungu hicho cha 3 ambacho kinaelezea vikao vya bodi, ile fursa ya wajumbe wa kikao cha bodi kuitisha kikao cha bodi katika mswada huu wa Kiswahili haimo, lakini ukija kwenye *version* ya Kiingereza imo. Kwa hivyo, kuna makosa haya ambayo yamejitokeza katika mswada huu, kwa hivyo tunamuomba waziri yafanywe marekebisho hayo ili isije kuleta mgongano wakati wa utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, mwisho tu nimalizie kwamba, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna wajibu mkubwa wa kupitisha miswada, na miswada tukishaipitisha hapa Mhe. Rais akishaitia saini inakuwa sheria, lakini kuna tatizo kubwa la utekelezaji.

Tuna sheria nyingi lakini *implementation* yake inakuwa sio nzuri. Kwa hivyo, ningeomba serikali iwe makini sana kusimamia na kuhakikisha kwamba sheria tunazozipitisha basi ziwe zinatekelezwa kama tulivyozipitisha hapa katika Baraza hili la kutunga sheria.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa leo bado tumo kwenye kujifunza, sitokuwa na mengi lakini nimeona niyaeleze hayo baada ya kupitia hii miswada.

Mwisho tu nimalizie, kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Fuoni tunaunga mkono Mswada huu wa Taasisi ya Elimu ya Zanzibar kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Yussuf Hassan Iddi. Sasa mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Balozi Amina Salum Ali; Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Mheshimiwa waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niseme mapema kabisa kwamba naunga mkono Mswada huu wa Kuanzisha Taasisi ya Elimu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu ni muhimu sana na kama walivyosema wachangiaji wengine, kwamba umekuja kwa wakati muafaka, ni muafaka kwa sababu umetukuta katika kipindi cha mpito kuelekea katika uchumi wa kati.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kama tuko njiani kuelekea huko, tunatakiwa wale wa kutufikisha kule nao watengeneze vile vile twende nao sambamba, ili kile ambacho serikali na wananchi wa Zanzibar wanakitaka waweze kukifikia.

Mhe. Naibu Spika, kwa safari yetu hii ya uchumi wa kati na uchumi wa viwanda kwa mujibu wa utaratibu wetu wa *Results for Prosperity (R4P)* na MKUZA, mipango yetu yote ya nchi tunaitekeleza sasa hivi. Taasisi hii imekuja kwa wakati kututengenezea rasilimali watu, ambao wataweza kutekeleza hili jukumu ambalo tumeliweka, nalo ni la kututoa hapa tulipo kwenda katika uchumi wa kati wa maendeleo wa Tanzania.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema, hili zoezi lilianza muda mrefu, lakini sasa hivi limekuja wakati ndio na ni wakati ambao tumo katika harakati za kufikia huko.

Mhe. Naibu Spika, ukisoma kazi za taasisi hii, nimejaribu kuziangalia na kuzisoma na nimevutiwa sana. Nizungumzie kuhusu kazi ya kwanza ya kubuni, kukuza na kufanya mapitio, kurekebisha na kutathmini mitaala kwa ajili ya skuli na vyuo.

Kazi ya pili ni kuishauri serikali kuhusiana na ukuzaji au uendelezaji wa mitaala.

Mhe. Naibu Spika, hizi kazi mbili pamoja na nyengine zote zilizopo, hizi mbili ndizo muhimu kwa sisi ambao tuko katika sekta hizi kwa ajili ya utekelezaji ambao utatuletea manufaa kwa Zanzibar. Katika kutengeneza, kubuni, kukuza, kurekebisha, kuthamini mitaala kwa ajili ya Skuli na vyuo lazima Mhe. Naibu Spika, sisi kama wachumi, na kama wapangaji wa mipango na mikakati ya

Taifa letu hili la Tanzania na hapa Zanzibar lazima tukubali kwamba tunakokwenda lazima tubadilike kimkakati.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu tukizungumzia uchumi wa kati lazima tuwe na rasilimali watu ambao wataweza kufanya kazi zile, lakini vile vile uchumi wetu tunatarajia tuutengeneze kwa ajili ya kuweza kutoa ajira kwa wananchi wetu. Kwa hivyo sera yetu ya elimu ambayo itakuwa inatengenezwa kupitia mitaala lazima iangalie mahitaji ya nchi, lakini vile vile iangalie mkakati na tunavyokwenda sio tu kwa nchi yetu kwa Afrika ya Mashariki na kwa kanda zote za Afrika na dunia nzima, tuangalie jinsi kama Zanzibar tutaweza kupata manufaa na kufaidika, na watu wetu kufaidika katika maendeleo ya kiuchumi, maendeleo ya kibiashara ya Zanzibar, Tanzania na nje.

Kwa hivyo, pale niliposema tubadilike kwamba mitaala na taasisi hii imepewa jukumu kubwa sana ya kututayarishia mitaala ambayo itaendana na hilo jambo ambalo tunataka tulifanye, mitaala ambayo itaweza kututolea vijana ambao wataweza kuja kuchukua nafasi mbali mbali ambazo zitatengenezwa na kuweza kuendeleza nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, chombo hichi maalum tunatakiwa tuwape vijana wetu elimu iliyokuwa na tija, na elimu iliyokuwa muhimu na iliyokuwa na manufaa kwa nchi yetu, nimesema hapa mitaala iendane na mahitaji kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tukiangalia kule nyuma tumepita saizi nyingi kama nchi Afrika, kama Tanzania kama Zanzibar. Huko nyuma tumesomeshwa mitaala ya ukoloni ulikuwa usomeshwe ufanye kazi ya kitawala umemaliza, tukaingia katika kujitawala, lakini sasa hivi tuko katika saizi nyengine ambayo inataka mitaala yetu iendane na saizi hii tuliyokuwa nayo ya kiuchumi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, karne ya 21 hii tunayokwenda nayo inatufanya tukimbie, sio kwenda pole pole, na ili tuweze kukimbia mitaala yetu ibadilike nayo iendane na wakati huu tuliokuwa nao wa Sayansi na Teknolojia, vile vile mitaala yetu itilie umuhimu sana suala zima la ugunduzi. Kwa sababu huko tunakokwenda biashara na viwanda inatakiwa wagunduzi ndio ambao wanaweza kuwa chachu ya maendeleo, kwa hivyo mitaala tunapoanzia tunaanzia skuli za chini za msingi, za Sekondari na Vyuo, na lengo kubwa la skuli masomo yetu ya mitaala yetu yaangalie suala zima la ugunduzi, vijana watumie vipaji vyao, vijana waendelezwe kwa aina mbali mbali ili wakitoka waweze kujitegemea na kuingia moja kwa moja katika soko hili la Zanzibar, la Tanzania, la Afrika ya Mashariki na kote.

Mhe. Naibu Spika, jengine tunapozungumzia suala zima la kufanya mitaala huko nyuma katika maisha yangu mengine kulikuwa kuna mkakati wa kuendeleza elimu Afrika, nafikiri sasa hivi tuko katika kipindi cha kumi la pili hili au tunaingia la tatu, katika mkakati huo suala kubwa lilikuwa limezungumzwa ni kwamba kuimarisha mitaala kwa Afrika, na suala hili limeonekana kwamba kubwa linalokwamisha mitaala ikawa inakwenda na wakati ni suala zima la utaalamu. Kwa sababu kutengeneza mitaala unatakiwa utaalamu sio kila mtu ataweza kutengeneza, kuna watu ambao wamesomeshwa wamebobea, wamepata *exposure,* wameonana wamenolewa na *instructors* mbali mbali, hao ndio ambao nchi nyingi za kiafrika zinakuwa tuna-*post*.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, matarajio yangu kwamba sisi kama Serikali tumejiandaa, na kwa kweli imebidi tujiandae hata kuwaomba marafiki zetu walioko nje, kuna kipindi *delegation* ilikuja Afrika kutoka kule Marekani, kuomba Serikali ya Marekani isaidie kuwasomesha watayarishaji wa mitaala, kwa hivyo na sisi hapa tusibweteke tukasema tunao wataalamu, lazima wataalamu watafutwe wasomeshwe na waunganishwe na washirikishwe na vyombo vyengine vya kimataifa ili waweze kwenda na wakati na kujua vile vile nini taifa linataka kwa wakati huo, nini mwelekeo wa uchumi kwa wakati huo, nini mwelekeo wa miaka ishirini ijayo, miaka hamsini ijayo ya Zanzibar, ili kuwa na mitaala ambayo itakuwa *sustainable* na itakayokuwa inaendelea, sio leo mtaala huu kesho unabadilishwa inakuwa hauendani kabisa na dhamira za mikakati mbali mbali ya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine na la mwisho Mheshimiwa nataka niliseme ni kuhusu hali nzima ya utaratibu wetu wa elimu ambao unakwenda na taasisi hii.

Taasisi hii inatakiwa vile vile kwa sababu ndio inayotizama ajira ya elimu inavyokwenda na kuweza kuishauri Serikali inatakiwa nayo vile vile iweze ku-*sense trend* ya uchumi na *trend* ya hivi vyombo mbali mbali, kwa mfano vyombo vinavyosimamia masuala haya wao nao wanahisia vipi, kwa sababu huko tunakokwenda vyuo na taasisi mbali mbali za elimu zinatakiwa nazo vile vile ziendane na wakati tunaokwenda. Kwa hivyo taasisi hii nayo inatakiwa vile vile iwe inafuatilia na kujua, iwe ina hisia inaweza kukaa na wabia mbali mbali, wahusika mbali mbali kuweza kujua nini hasa kifanyike ili nchi yetu iweze kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema nilikuwa naunga mkono lakini nilitaka nisemee kwa upande huu mwengine kwa sababu Wajumbe wengi hawajazungumzia, kwamba chombo hichi ni muhimu, chombo hichi ndicho

ambacho kitatuvusha sisi kwenda mbele, kwa sababu hao ndio watakaotutayarishia rasilimali watu na kuiwezesha nchi yetu iende sambamba na hii sera yetu ya viwanda, sera yetu ya mikakati ya kiuchumi n.k.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono Mswada huu, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua fursa hii kuchangia na kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa katika Baraza lako tukufu, naunganisha kusema Mhe. Balozi Amina kwamba hii ni taasisi muhimu sana, na umuhimu wake unatokana na kwamba inamiliki mfumo wa elimu, na kwa maana hiyo basi taasisi ambayo mtaipitisha sheria yake, kwa kweli katika zama hizi inapaswa kutayarisha mitaala ambayo italenga zaidi katika *liberation* ya watu. Amewahi kusema mtaalamu mmoja wa *Education* Paulo Freire amesema *"Education for liberation"*.

Kwa hivyo taasisi hii kwa kweli tunaipa kazi ya kutayarisha vijana ambao watakuwa wamekomboka katika ujumla wake; katika masuala ya siasa, uchumi na mengineyo ya kijamii. Kwa hivyo ni taasisi muhimu sana kwa lugha nyengine ndio roho katika jamii yoyote.

Baada ya kusema hayo niseme kwamba michango mingi imetolewa, michango ambayo mingine imelenga zaidi katika kuimarisha mswada na mengine imekwenda mbele zaidi ya kutoa maoni ya namna bora ya kutekeleza mswada huu, zaidi mengi sana yametuelekeza wakati wa utekelezaji tufanye nini ili kuona kwamba taasisi hii inakuwa hai na inatekeleza majukumu yake.

Sasa nianze kujibu suala hili la hoja iliyotolewa na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) juu ya ushauri wake ambao uko katika hatua ya pili kama nilivyosema ya utekelezaji, kwamba suala la ufuatiliaji mzuri ili kufanikisha ufundishaji kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa hapa atakuwa anatukumbusha tu, kwa sababu sasa hivi Wizara ya Elimu kupitia Idara zake mbali mbali, Idara zote tumezielekeza kwamba kufuatilia kwa karibu masuala ya usomeshaji, tokea Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu mpaka chini, na kuna ratiba maalumu imewekwa ya ufuatiliaji. Kwa hivyo hapa ni kwamba anatukumbusha tu, lakini ajue kwamba nyakati hizi suala hili la ufuatiliaji tunafanya na wakati mwengine tunapopata taarifa kwamba labda skuli fulani walimu hawafanyi kazi kama inavyotakiwa huwa tunafanya ziara za kushtukiza, na wakati mwengine

tunapeleka ukaguzi maalumu na tumeifanyia Skuli ya Kidongo Chekundu baada ya kupata taarifa, tuliifanyia ukaguzi maalumu, tunaita wa kushtukiza.

Kwa hivyo Mhe. Mjumbe suala lako tunalifuata na tutalifuata zaidi ili kuona kwamba ubora unapatikana. Kufuatilia hakuna mwisho, kwa hivyo umetukumbusha na tutaendelea kufuatilia ili kuona kwamba Zanzibar inaendelea kutoa elimu bora, ufuatiliaji huu kwa kweli umetiwa nguvu zaidi kutokana na falsafa yetu mpya tuliyoianzisha katika Wizara ya Elimu ambayo tunaita "Elimu bora kwanza". Na kila Idara inaitekeleza kwa namna yake, kwa hivyo suala la ufuatiliaji tuko pamoja, tunasema kwamba idara inayohusika na ukaguzi wa wanafunzi, kwa hivyo, kwao mtazamo wa mwanzo ni elimu bora kwanza. Taasisi ya elimu ni elimu bora kwanza, hata kitengo cha fedha elimu bora kwanza, hiyo ndiyo kauli mbiu tuliyonayo katika Wizara ya Elimu sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, kuna hoja iliyotolewa na Mhe. Machano Othman Said; Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini anauliza je, kuna faida gani kwa wanafunzi kutumia mfumo wa kumaliza darasa la sita halafu kwenda darasa la tisa. Tunasema kwamba faida ya mfumo huu ni kuwawezesha wanafunzi kumaliza elimu ya Sekondari katika umri utakaowawezesha kupata fursa mbali mbali za kujiunga na masomo na mafunzo ndani na nje ya nchi. Kwa lugha nyengine huu ni mfumo wa kiduni hatuwezi kuendeleza mfumo ambao pengine utatuweka nyuma hasa inapokuja fursa za masomo ya elimu ya juu, na hasa pale tunapotaka kupeleka watoto wetu katika nchi za nje, kunakuwa na masharti ya kiumri, wakati mwengine mbali na masharti ya kielimu lakini pia kuna masharti ya kiumri, ili tusiwekwe kando nafikiri ikaonekana katika sera ni busara kufuata mfumo huu.

Lakini hata hivyo kitaalamu, *very interesting* matokeo ya wanafunzi wa darasa la sita walioingia darasa la tisa na wale wa darasa la saba wanaoingia darasa la tisa. Hawa darasa la sita wamefanya vizuri zaidi kuliko la saba, na tunaendelea kufuatilia maendeleo yao. Wako *Form I* lakini tumewatenganisha kidogo kwa ajili ya utafiti wale waliotoka darasa la sita na wale waliotoka darasa la saba, ili kuona hatimaye watamaliza katika *performance* ya aina gani.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la walimu kupatiwa mafunzo kuhusiana na mabadiliko yanayotokea katika mfumo wa elimu. Kwa kweli Wizara hili inalifanya, na tumekuwa tukipata misaada mbali mbali katika kufanya suala hili, kwa mfano tunapata misaada kutoka *GPE, World Bank, Agakhan, Milele* na *SIDA* ili kuona walimu wetu tunawapatia mafunzo kutokana na mabadiliko

yanayotokea. Hili ni jambo la lazima ili mwalimu aweze kusomesha kwa ubora zaidi anahitaji kusomeshwa kila siku.

Kwa hivyo mabadiliko ya kimitaala yanapotokea basi walimu huwa tunawapatia mafunzo hatua kwa hatua, lakini pia wakaguzi na viongozi mafunzo haya yanahusu mpaka katika masuala ya *Education Leadership* tunawafundisha nao viongozi kuwapatia mafunzo ili wajue kusimamia mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine la Taasisi ya elimu kushirikiana na Baraza la Mitihani bila ya shaka mashirikiano yapo karibu, hata mswada wenyewe huu unaonesha mjumbe mmoja wa bodi ya ushauri anatoka katika Baraza la Mitihani, lakini pia kuna mashirikiano mengine yanayofanywa na Wizara kupitia vikao vyake vya kamati tendaji ambayo Wakurugenzi wa taasisi zote hizi ni wajumbe na huwa tunakaa pamoja kuzungumzia maslahi ya Wizara ya Elimu.

Hoja nyengine ni ada kwa Skuli binafsi, hapa kulikuwa na ushauri labda kuweka bei au ada elekezi, Wizara ya Elimu tarehe 6 Januari, 2016 ilitoa toleo maalumu kwa Skuli binafsi kuhusu kutoongeza ada kiholela na kutowatoa wanafunzi wafanye vizuri katika skuli zao hilo ni toleo, waraka wa Wizara ya Elimu kutaka si kudhibiti lakini kuwasihi wenye kumiliki skuli binafsi kuweka ada ambazo zitawanufaisha zaidi watu walio wengi kuliko watu walio wachache.

Hoja ya mwisho ilikuwa ni malimbikizo ya fedha za usafiri na likizo. Hapa nipende kusema kwamba Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha imekusudia kuliondoa deni hili la walimu katika mwaka huu wa fedha, dalili zimeshaanza Wizara ya Fedha inatutengea fedha kila mwisho wa mwezi ili kuwalipa walimu na zoezi hilo linakwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya mchangiaji Mhe. Simai Mohammed Said; Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu, yeye ana hoja kwamba ufundishaji wa masomo ya lugha ya Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kichina yatiliwe mkazo yazingatiwe.

Suala hili ni la kisera. Ukiangalia sera ilivyo ya mwaka 2006 inahimiza ufundishaji wa lugha za kigeni, kwa hivyo hili ni suala ambalo limo ndani ya sera na sisi kama Wizara ya Elimu tutaendelea kulifanyia kazi. Lakini hata hivyo kwa somo la Kiarabu linasomeshwa katika ngazi zote hapa Zanzibar na Kichina kwa sasa kinasomeshwa katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar katika

ngazi ya Diploma, na Kifaransa pia kinasomeshwa na lugha nyengine za kigeni. Kwa hivyo katika kutekeleza sera ya elimu masuala ya lugha tutayapa nafasi yake.

Kuhusu kuimarishwa upatikanaji wa vifaa vya maabara katika maskuli. Ni kwamba Aprili, 2016 Wizara kupitia taasisi ya elimu ya Zanzibar imenunua na kusambaza vifaa vya kufundishia Sayansi na Hisabati katika skuli za msingi na Sekondari, kadri pesa zitakapopatikana basi Wizara inanunua vifaa vya kusaidia usomeshaji huo, na pia wakati mwengine tunapopata wafadhili huwa wanatusaidia na tunafanya hivyo. Sasa hivi kidogo naweza kusema *alhamdullillahi,* unapokwenda baadhi ya skuli wanasema wanavyo baadhi ya vifaa.

Kuhusu suala la kuongeza mjumbe wa bodi ya ushauri kutoka Idara ya *Diaspora*. Masuala haya kila mmoja ni muhimu, kila idara ni muhimu, kila taasisi ni muhimu kuingia katika bodi ya ushauri wa mitaala, lakini kupanga ni kuchagua, kwa hivyo katika awamu hii tumeona kwamba kwa kuwa ujumbe wa bodi una idadi yake maalumu, kwa hivyo sisi tunahisi kwamba wajumbe waliotajwa kwa sasa wana nafasi muhimu zaidi kuliko ambao hawajatajwa.

Kuhusu kupotoshwa kwa historia ya Zanzibar au somo la historia. Ni kwamba Wizara ya Elimu imeandaa mihutasari na vitabu vya kufundishia somo la historia kuanzia ngazi ya msingi hadi vyuo vya walimu vinavyoendana na hali halisi ya historia ya Zanzibar. *Syllabus* ziko zinazosomesha historia, na vitabu vipo vya historia, lakini kwa nini kuna upotoshaji, au kwa nini kunadhaniwa kuna upotoshaji.

Tatizo liliopo tunaita *Approach of Teaching,* yaani mkabala wa usomeshaji, *content* ipo, vifaa vipo, lakini kutokana na fikra za yule mwalimu anayesomesha ana nafasi muhimu sana ya kupotosha.

Kwa hivyo kuanzia sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itasimamia kwa karibu sana sana usomeshaji wa somo la historia na somo la uraia, ili kuona kwamba malengo yake yanatimizwa, hatutomwachia mwalimu hata mmoja ambaye atasomesha kwa namna anayotaka yeye. Hivi karibuni tunataka kufanya mapitio ya muhutasari wa masomo haya mawili, Historia na Uraia kuona kama kweli yanakwenda na wakati wa sasa, na kama kwamba mkabala unaotumika kusomesha unaendana na kumjenga raia mwema wa Zanzibar na Tanzania.

Hoja ya Mhe. Mgeni Hassan Juma; Naibu Spika, ushauri wako umepokelewa na utafanyiwa kazi ni zaidi unahusu masuala ya upangaji wa *editing.*

Mhe. Juma Ali Khatib Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum, kuwe na ufuatiliaji mzuri ili kufanikisha utekelezaji. Nafikiri suala hili tumeshalieleza tutaendelea kuimarisha siku hadi siku ufuatiliaji.

Kwa kweli tuna kitengo maalum ambacho kimepewa kazi hiyo kinaitwa Kitengo cha *Monitoring and Evaluation*, ambacho kinafanya kazi kila siku kufuatilia masuala mbali mbali ya kielimu.

Mhe. Mohammed Mgaza Jecha Mwakilishi wa Jimbo la Mtambile na Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Jimbo la Konde hoja zao ni kwamba kuna uhaba wa wakaguzi katika skuli zetu.

Katika kufanya mabadiliko katika Wizara ya Elimu tumeandaa mswada, sasa hivi tuko katika rasimu lakini baadae tutaleta mswada wa kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi. Lakini kabla ya wakati huo Kitengo cha Ukaguzi kimeandaa mipango mingi ya ufuatiliaji wa ukaguzi, na kwa sasa kinaendelea kutoa mafunzo kwa wakaguzi ili waweze kufanya kazi katika kiwango kinachohitajika. Pia tutaanzisha vitengo vya ukaguzi katika kanda, katika Wilaya, ambao watakuwa karibu zaidi na walimu na itakapofika wakati huo na si muda mrefu, sasa hivi tunatoa mafunzo basi ukaguzi utakuwa mara kwa mara katika skuli.

Hata hivyo tumejaribu kuimarisha maeneo ya ukaguzi na baadhi ya maeneo ambayo tumeimarisha katika ukaguzi hatutomalizia tu katika kuangalia uwezo wa mwalimu katika kufundisha lakini pia uwezo wa walimu katika kutunza mali na miundombinu ya skuli.

Kumetokea tabia kidogo ya baadhi ya walimu kupuuza, kama anaweza kumuona mwanafunzi anaharibu kifaa hata hashughuliki lolote. Kwa hivyo sasa itakuwa ni wajibu wao na ukaguzi tutapofanya tutaangalia masuala haya, kama tumetoa kifaa kwa muda fulani tunakwenda kuangalia kipo au hakipo, kinatumika au hakitumiki. Hatuwezi kuacha vifaa vikafanywa pambo, tunataka vitumike lakini pia vidumu kwa wakati wake uliokusudiwa.

Mhe. Hidaya Ali Makame, Mwakilishi Nafasi za Wanawake, je, wizara inatuthibitishia vipi kuhusu kutoa mashirikiano ya ufundishaji na upatikanaji wa vifaa wa kufanyia *practical* katika skuli au Vyuo vya Amali, mfano magari mabovu, mbao, vitambaa vya kujifunzia na kushona.

Wizara iko tayari kushirikiana na wadau wa elimu katika kufanikisha ufundishaji katika skuli na vyuo na vituo vya mafunzo ya amali kuvipatia vifaa vinavyohitajika. Ni kwamba suala hili linahitaji nguvu ya pamoja. Sisi Serikali yaani wizara lakini na kila mwenye hamu na hamasa ya maendeleo, basi wizara inaomba ashiriki katika kuvipatia vifaa hata vichakavu kwa ajili ya mafunzo ya watoto wetu wanaojifundisha mafunzo ya amali.

Mwisho kulikuwa na masuala maalum ya Mhe. Omar Seif Abeid kuhusu walimu wa sayansi, kwamba hivi karibuni wizara imetangaza nafasi za ajira ya walimu wa sayansi, mchakato unaendelea na mchakato utakapokamilika walimu hao watagawiwa kwa mujibu wa mahitaji, ikiwa skuli yako ina mahitaji makubwa zaidi kuliko nyengine utapewa nafasi hiyo, lakini ikiwa haina mahitaji makubwa kuliko nyengine tutaangalia sehemu nyengine. Lakini nataka nikuhakikishie kwamba, hivi karibuni tulipata fursa ya kuajiri walimu 38 Pemba kule, basi Wilaya yako Wilaya ya Micheweni tuliwapatia walimu 15, wakati wilaya nyengine Mkoani, sita, saba, nane kutokana kwamba tunajaribu kuangalia yale mahitaji. Hatukupendelea Wilaya ya Micheweni lakini wao wana mahitaji makubwa zaidi kuliko wengine, lakini Wizara katika kutoa vifaa na walimu inazingatia sana wapi pana mahitaji makubwa zaidi kuliko pengine.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono kwa asilimia zote. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nami fursa hii kuweza kujibu hoja mbali mbali zilizojitokeza kama ambavyo wajumbe wengi wamechangia.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru wale wote ambao wamechangia mswada huu wa sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar ya mwaka 2016 kwa maelezo na kwa maandishi baadhi yao, na nitapenda kuwataja wale wote ambao wamechangia.

Kwanza kabisa napenda sana kuipongeza Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mashirikiano yao na mchango wao mkubwa ambao wametupatia wakati tunafanya kazi nao kwa pamoja.

Kusema kweli ni kwamba mchango wao umezidi kuimarisha mswada wetu huu wa sheria na mawazo yao yote yale ambayo yametoka katika Kamati basi tutayafanyia kazi katika kuendeleza na kuimarisha mswada wetu huu.

Vile vile nipende kuwatambua wale wote ambao wamechangia kwa mdomo.

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
2. Mhe. Machano Othman Said
3. Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi)
4. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
5. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
6. Mhe. Shamata Shaame Khamis
7. Mhe. Shehe Hamad Mattar
8. Mhe. Rashid Makame Shamsi
9. Mhe. Yussuf Hassan Idd
10. Mhe. Balozi Amina Salum Ali

Mhe. Naibu Spika, napenda niwatambue wale ambao wamechangia kwa maandishi akiwemo

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma
2. Mhe. Juma Ali Khatib
3. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
4. Mhe. Omar Seif Abeid amechangia kwa maandishi lakini vile vile alipata nafasi ya kuchangia kwa kusema. Kwa hivyo namtambua kuwepo kwake kote kote katika kuchangia kwa kusema na vile vile kwa maandishi.
5. Mhe. Hidaya Ali Makame
6. Mhe. Ali Khamis Bakari
7. Mhe. Miraji Khamis Mussa
8. Mhe. Maudline Cyrus Castico
9. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Tunawashukuru wote kwa michango yao.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kabla ya kujibu hoja nyengine ambazo zimejitokeza za Waheshimiwa Wawakilishi kutoa ufafanuzi wa mambo mawili yafuatayo.

Kwanza ni ukomo wa Taasisi inayopendekezwa katika kufanya kazi zake. Ukomo wa Taasisi hii ni kwa Skuli za Maandalizi, Msingi na Vyuo vya Walimu vya Zanzibar tu. Kwa ngazi ya Sekondari Taasisi hii inashirikiana na Taasisi ya Elimu ya Tanzania.

Lakini pili kubadilika kwa mfumo wa elimu huwa unapita muda baina ya mabadiliko, kwa mfano baada ya tukio la mwaka 1992 lilipoondoshwa darasa la nane wanafunzi walifanya mitihani makundi mawili, darasa la saba na darasa

la nane na mpaka mwaka 2015, mwaka jana lilipoondoshwa darasa la saba ndipo wanafunzi walifanya mitihani tena yaani kwa makundi mawili darasa la saba pamoja na darasa la sita.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nataka kusema kwamba mpango huu mabadiliko huwa hayaendi tu kiholela holela, bali huwa yanachukuwa muda katika kwenda na mabadiliko yake, na mabadiliko haya hutokezea baada ya kufanyika utafiti na kuona ile hali ya mabadiliko ya kielimu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee katika kujibu hoja za baadhi ya waheshimiwa ambazo wamezichangia.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, Mwakilishi wa Viti Maalum, katika kuchangia kwake alikuwa anahoji kwamba vifaa vya kufundishia havitoshelezi kwa wanafunzi na kukosekana vitabu vya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mhe. Naibu Spika, napenda sana kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yetu imechapisha na kusambaza vitabu na viongozi vya walimu vya kutosha kwa wanafunzi pia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, vitabu vya nukta nundu na hati kubwa vyote wizara yangu imeweza kuchapisha na kuvisambaza katika maskuli.

Vile vile kwa upande wa *lens* kwa wanafunzi wenye uoni hafifu, taasisi suala hili italifanyia kazi zaidi na kuweza kuona wanafunzi wetu hawa nao wanaweza kupata vifaa hivi.

Suala la kuimarisha elimu ya mjumuisho kwa kuzingatia upatikanaji wa walimu, vifaa na miundombinu. Wizara yangu inachukua jitihada kubwa ya kuimarisha elimu mjumuisho katika kufundisha walimu na katika Chuo cha Kiislam Mazizini tunayo *course* hii ya elimu mjumuisho, lakini vile vile katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar pia nako kuna diploma ya elimu mjumuisho. Yote haya ni katika kuona kwamba upatikanaji wa elimu unakuwa mkubwa wa kuweza kuwasaidia vijana wetu.

Katika kusambaza vifaa mbali mbali zikiwemo mashine za *braille* na kuimarisha miundombinu ikiwemo ukarabati wa majengo ya skuli. Tunaweza kukiri kwamba labda hapo nyuma katika ujenzi wetu tulikuwa hatuzingatii sana suala hili, lakini hivi sasa na hasa katika majengo mapya yetu yote ambayo tunayajenga basi suala hili linazingatiwa.

Kwa zile skuli za zamani ni kwamba tunajaribu katika kubomoa sehemu ili kuona napo tunaweza kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum. Lakini hata katika vyoo ni kwamba tunatengeneza vyoo maalum vya kuweza kuwasaidia wanafunzi hawa ili na wao weweze kuwa katika mazingira salama wanapokuwa katika eneo la skuli.

Mhe. Mwakilishi pia alikuwa na pendekezo kwamba miongoni mwa wajumbe wa bodi awepo mjumbe kutoka taasisi ya watu wenye ulemavu. Suala hili Mheshimiwa ni kwamba tayari limo katika huo mswada wetu wa sheria katika kifungu cha 6(1)(e) ametajwa mjumbe mmoja kutoka Baraza la Watu wenye Ulemavu. Kwa hivyo Mheshimiwa ni kwamba suala hili tumelizingatia sana na tayari limo, lakini inawezekana katika kuangalia pengine ulililiruka, lakini tayari hili suala tumelizingatia.

Hoja nyengine ilitoka kwa Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chaani, ambapo yeye alikuwa anashauri mfumo wa taaluma uwe muda maalum kabla ya kufanyiwa mabadiliko, na nilijibu ule mfumo kwamba tunaufanya kwa kuzingatia muda maalum.

Vile vile ushauri wake umezingatiwa lakini tukiangalia mfumo wa elimu ambao ulikuwa una miaka 7 kwa msingi 2,2,2, umeanza kutumika mwaka 1993 na mfumo huo ndio uliobadilishwa na sera mpya ya elimu ya mwaka 2006 ambapo mfumo huo kwa sasa una miaka 2, 2, 6, 4, 2. 2 kwa maana ya elimu ya maandalizi, 6 elimu ya msingi, 4 elimu ya sekondari na 2 ni elimu ya sekondari ya juu yaani *advance*.

Mfumo huu umeanza kutumika kwa wanafunzi walioanza darasa la kwanza mwaka 2010 na wanafunzi hawa hawa ndio ambao wamefanya mtihani wa darasa la 6 mwaka 2015 na kwa mwaka huu wameanza masomo yao ya *form one*.

Vile vile Mheshimiwa alisisitiza kwamba elimu ya maandalizi itiliwe msisitizo. Hilo ndio lengo kubwa la wizara yetu katika kusisitiza elimu ya maandalizi. Hivi sasa katika kila skuli ya serikali ya msingi tunaweka darasa la maandalizi, lengo ni katika kusisitiza na kuimarisha skuli hiyo. Kwa sababu tunafahamu kwamba *udongo upate ulimaji*, na tunapoimarisha elimu ya maandalizi ndipo ambapo tunamjenga mtoto wetu vizuri. Kwa hivyo wizara yetu madarasa haya tayari imeanzisha, lakini vile vile tuwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi tuwe tunawahamasisha wananchi wawaandikishe watoto katika haya madarasa ya maandalizi. Kwa sababu bado kuna baadhi ya wanajamii ambao wanadhani kwamba kumpeleka mtoto skuli katika umri wa miaka 4 anahisi bado ni

mapema na haoni umuhimu huo. Kwa hivyo sisi Wawakilishi wa wananchi tuchukuwe jukumu hilo la kuelimisha wananchi wetu umuhimu wa kuwapeleka watoto katika madarasa ya maandalizi katika umri ambao unastahiki.

Vile vile Mhe. Mwakilishi alikuwa anasisitiza suala la somo la lugha ya Kiswahili lipewe kipaumbele zaidi kati ya masomo ya lugha yaliyopendekezwa kufundishwa.

Wizara yetu inaendelea kulitilia mkazo suala la ufundishwaji wa somo la Kiswahili na ndio maana katika elimu ya maandalizi wanafunzi wetu wanafundishwa kwa lugha ya Kiswahili, wanapoingia msingi wanaanza Kiswahili ingawa wanasoma na somo la Kiingereza lakini lugha ya kufundishia inakuwa inatumika lugha ya Kiswahili. Lakini somo hili hili hadi elimu ya sekondari linatumika kama ni somo, lakini hata katika elimu ya juu basi pia linatumika kama ni somo na ni lugha ambayo imeibua ajira kwa vijana wetu walio wengi.

Tuna vijana wengi ambao sasa ni walimu katika nchi mbali mbali wanaosomesha somo la lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo ni kweli kwamba matumizi ya Kiswahili ni mazuri na sote kwa nguvu zetu tuunge mkono jambo hili na tuipende lugha yetu hii, tuienzi, kwa sababu *mkataa asili ni mtumwa* na sisi tusiwe watumwa wa lugha za watu.
Mhe. Nadir pia amesisitiza elimu zinazotolewa katika skuli za serikali na binafsi maudhui yake yafanane.

Napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi ni kwamba lengo la kuanzishwa sheria ni katika kuipa nguvu Taasisi yetu ya Elimu iweze kusimamia Mitaala ipasavyo. Katika usimamizi huu ni kwamba iweze kuona mitaala inayofundishwa katika skuli za serikali, lakini vile vile na skuli za binafsi basi yote inafanana. Kwa hivyo tutapoipitisha sheria hii Taasisi ya Elimu itaweza kuwa na nguvu na kuweza kusimamia ipasavyo sheria hiyo.

Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni yeye alikuwa anahoji suala zima la ajira kwa walimu na maslahi yao yazingatiwe na tayari suala hili limeshajibiwa, lakini serikali yetu inajitahidi sana katika kutoa ajira kwa walimu wake kadri hali ya fedha inavyoruhusu.

Tunahitaji walimu wengi kweli lakini fedha ndizo ambazo zinaamua waajiriwe walimu wangapi, kwa kipindi gani na kwa eneo gani. Kwa hivyo ni kwamba kila hali ya fedha itakapokuwa inaruhusu basi wizara yetu itapeleka maombi

haya katika Wizara ya Utumishi ili kuona kwamba walimu walio wengi wanaweza kupata ajira ili kuondosha tatizo la uhaba wa walimu.

Vile vile Mhe. Mattar alikuwa anatoa angalizo kwamba misaada kutoka kwa wahisani inabadilisha mfumo wa elimu yetu. Napenda nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba mfumo wa elimu yetu haubadilishwi kwa kufuata misaada ya wahisani. Misaada ya wahisani inapokuja ni kwamba sisi ndio tunaoamua kutokana na msaada huu utumike pahala gani na si kwamba msaada uliokuja ubadilishe elimu yetu, na ndio maana unaweza kukuta kifaa kinakuja kinapelekwa pengine kinaweza kukaa kikasaidia katika masomo mengine ya ziada na hakitokuwa katika yale masomo ya lazima ya mwanafunzi kwa sababu inakuwa iko tofauti na ule mfumo ulivyo. Wakati mwengine tunaweza kupata msaada ukawa pengine haufai kwa msingi wala kwa maandalizi wala kwa sekondari, lakini tukauchukua msaada ule ukatumika kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu. Kwa hivyo ni kwamba msaada wowote ambao unakuja haubadilishi mfumo wetu, bali ni kwamba mfumo wetu unakwenda kama ambavyo ulivyo, ila msaada unapokuja tunautumia kwa pale ambapo panastahiki na panapokuwa ile haja ipo.

Vile vile wakati mwengine tunakuwa tunaomba msaada kwa mujibu wa hilo hitaji letu sisi lilivyo. Kwa hivyo msaada ule unapokuja tayari unakuwa umezingatia mahitaji ambayo tunayahitajia.

Mhe. Shamata Shaame Khamis yeye alihimiza suala zima la utekelezaji wa majukumu kwa wafanyakazi wa Taasisi ya Elimu. Mheshimiwa ni kwamba ushauri huu unazingatiwa na kwa sababu ndio lengo letu kwamba katika kusimamia majukumu yetu yote kwa hilo nalo tunalizingatia sana.

Vile vile katika Bodi ya Ushauri awepo mjumbe kutoka Chama cha Walimu ZATU, tulivyotaja wajumbe kuna mwakilishi kutoka Jumuiya ya Vyama vya Wafanyakazi, mwakilishi huyu au mjumbe huyu katika ile sheria ni kuwa yeye atakuwa anawawakilisha wafanyakazi wote wakiwemo hawa wafanyakazi wa ZATU; ni Chama cha Wafanyakazi. Kwa hivyo kama Chama kinawakilishwa na mjumbe mmoja kwa hivyo mjumbe huyu ambaye yupo tayari, basi tayari na yeye pia anawakilisha hawa wanachama wa ZATU. Kwa hivyo hatujawa na haja ya kuongeza mwakilishi wa ZATU kwa sababu tayari mwakilishi huyo yupo na ambaye anawakilisha hilo kundi.

Pia alikuwa anaomba fedha za Taasisi zitoke katika kifungu cha fedha cha serikali na kupatikana kwa wakati.

Mhe. Mwakilishi tunakushukuru sana kwa hili na Wizara ya Fedha inasikia na itajitahidi sana katika kutupatia fedha kwa wakati ili kuona kwamba shughuli za taasisi ya elimu, lakini na shughuli nyengine zozote za wizara yetu zinatekelezwa kwa wakati muafaka.

Pia Mheshimiwa alishauri sifa za Wajumbe wa Bodi zizingatiwe. Mheshimiwa suala lako vile vile nalo tumelizingatia sana na hizo sifa nazo zitazingatiwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Miraji Khamis Mussa ambaye alichangia kwa maandishi, Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni yeye alishauri kwamba tuunde chombo cha pamoja kati ya SMZ na SMT ambacho kitasimamia changamoto za maeneo ya pamoja ili elimu yetu ikue zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuhakikishie kwamba suala hili nalo tumelichukua na kwa sababu tayari tunafanya kazi kwa pamoja, lakini kuwepo kwa taasisi hii na kule Bara tayari ipo Taasisi ya Elimu, kwa hiyo ni kwamba mashirikiano yetu yatazidi zaidi na zile changamoto za kielimu tutaweza kuzitatua kwa pamoja.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto yeye vile vile alipongeza hatua nzuri ya kuanzishwa mswada huu kwa sababu ni hatua ambayo itaendeleza sana suala zima la elimu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa kwa mchango wake.

Mhe. Ali Khamis Bakar wa Tumbe alitoa hoja kwamba tutafute walimu wa kada mbali mbali ili waweze kusomesha maskuli yetu. Mhe. Mwakilishi ni kwamba wizara yetu kupitia vyuo vya walimu tunafundisha kozi mbali mbali, na lengo la kufundisha kozi hizo ni katika kupata hao wadau mbali mbali. Kwa hiyo, suala hili wizara yetu inalizingatia sana na ndio maana kuna kozi nyingi katika vyuo vya ualimu ambavyo vinatoa walimu mbali mbali na ndio tunapata walimu wa sayansi, walimu wa *art* na vile vile tunapata walimu wa masomo ya ufundi.

Vile vile alishauri kwamba kutolewe vyeti kwa wakati, wakati wa *teaching practice* kwa wale ambao wanakwenda mafunzo. Mhe. Mwakilishi ni kwamba vyeti hutolewa baada ya mtu kuhitimu masomo yake, mwanafunzi anapokwenda kufanya mazoezi anakuwa ni sehemu ya mafunzo yake. Kwa hiyo, katika mafunzo yale cheti hakitoki pale, bali anapomaliza kufanya *teaching practice* yake pale anapewa ripoti ya kile ambacho amekifanya. Na kawaida mwalimu anapokwenda *teaching practice* ni kwamba chuo ambacho anatoka kuna walimu ambao wanakuwa wanakwenda kumsimamia, na walimu

wale wanakuwa wanaandaa katika matokeo ya mwanafunzi, na ndio maana mwisho mwanafunzi anapopewa cheti chake na matokeo haya pia yanakuwemo.

Suala jengine Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni alitushauri kwamba tuige wigo wa utekelezaji wa taasisi za nchi nyengine kama tumeziainisha katika hotuba yetu.

Mhe. Mwakilishi tunakuhakikishia kwamba uanzishwaji wa taasisi hii basi utafuata wigo wa sehemu mbali mbali duniani ili kuona kwamba na sisi tunapiga hatua kubwa ya maendeleo ya kielimu katika nchi yetu.

Vile vile Mheshimiwa ameshauri kuwepo kwa majengo na ofisi kwa taasisi, ni kwamba kwa sasa ofisi ina chumba kimoja cha Mkurugenzi na gari moja tu. Ni kweli Mheshimiwa kwa sababu wizara yetu inakabiliwa na ufinyu wa majengo, kwa hiyo kutokana na hali hiyo kwa sasa tunatumia kwa vile ambavyo tunayo. Lakini wizara yetu ina lengo la kujenga jengo jengine la wizara katika eneo letu la Mazizini kwa sababu eneo tunalo na tumeweza kutafuta wafadhili na tayari wameweza kujitokeza, hivyo tumo katika hatua za kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo jengine. Kwa hiyo, tutakapojenga hilo jengo jengine litaweza kusaidia taasisi zetu nyingi kupata ofisi ndani ya eneo letu, na hali hiyo itatupelekea kwamba sote wizara yetu itaweza kuwa katika sehemu moja na kazi zetu zitaweza kwenda vizuri zaidi tukipata jambo hilo. Kwa hiyo, waheshimiwa tunakuombeni sana tukisema kwamba kuna siku ya kujitolea basi tunakuombeni muje mutuunge mkono ili tukajitolee kulisimamisha hilo jengo la ofisi yetu.

Vile vile Mheshimiwa alisema kwamba kulikuwa na ufinyu wa ushirikishwaji wa wadau. Mhe. Mwakilishi ni kwamba kwa sababu tayari mswada sasa umefika katika hatua hii, lakini katika miswada mengine ambayo itakuwa inaendelea katika wizara yangu basi suala hili tutalizingatia sana na tutajitahidi sana kushirikisha wadau mbali mbali, kwa sababu imeonekana kwamba kwa muono ambao mwakilishi ameuonesha kwamba mswada huu wadau ambao tumewashirikisha si wengi sana, ingawa sisi tumejitahidi. Lakini tutajitahidi kushirikisha wadau wengine katika miswada mengine ambayo tunayo ili kuona kwamba mawazo mengi na michango mingi tunaweza kuipata.

Pia Mhe. Mwakilishi alitushauri tusomeshe wataalamu mbali mbali, na tuwe na wanafilosofia, watafiti, wanasaikolojia, wakaguzi na wakuza mitaala. Mheshimiwa nalo vile vile tumelizingatia. Lakini alitaja neno moja, neno mahasusi yaani liko tofauti tofauti, lakini katika mapendekezo ya kamati tayari

neno hili limewekewa usahihi wake, na kama lilivyo kwa mujibu wa lugha yetu ya Kiswahili tunatumia neno "mahususi". Kwa hiyo, katika mswada kila pahala ambapo pana neno "mahsusi" au "mahasus" basi kote litatumika kama ni "mahususi".

Pia kuna mapendekezo mengine ambayo aliyatoa Mhe. Mwakilishi kwa mfano kama neno "*curriculum development*" katika ile miswada ya Kiingereza, "*instruction materials*" katika tafsiri ya Kiswahili. Tayari neno hili katika yale mapendekezo ya kamati tayari limewekwa, na maneno mengine ambayo Mheshimiwa umeyaonesha ni kwamba katika ile ripoti ya kamati ambayo ameitoa, marekebisho ya vifungu basi maneno haya yote yamo. Lakini kwa lile ambalo labda litakuwa kwa bahati mbaya halimo basi litaingizwa, lakini mengi ya maneno haya tayari katika ile ripoti ya kamati yamo, kwa sababu baada ya kukaa nao kwa pamoja waliyaona na wao na wakayafanyia marekebisho. Kwa hiyo, maneno haya tayari mheshimiwa marekebisho yake yamefanyika.

Katika zile kazi za bodi kwenye kifungu Nam. 10 (2) neno "ni" lije katika kifungu (a), hilo tumelichukua na tutaliweka sawa kwa sababu tunadhani katika ule utaratibu mzuri wa kuweka lugha husomeka vizuri. Kwa hiyo, hili mheshimiwa tumelichukua.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Yussuf Hassan Iddi wa Jimbo la Fuoni michango yake mingi ambayo ameitoa ni kuhusiana na vifungu, basi tayari pia katika mapendekezo ya kamati vifungu hivi marekebisho yake yamo. Kwa mfano, kama katika sifa ambazo zimeoneshwa za Mkurugenzi katika *version* ya Kiingereza imesema kwamba awe na elimu ya *masters* lakini katika *version* ya Kiswahili kwenye *degree* ya kwanza. Tayari rekebisho hilo nalo limefanyika, na katika ripoti ya kamati ukisoma vizuri utakutana nalo kwamba limewekwa katika usahihi wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo masuala mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyaainisha tumeyajibu kama ambavyo wao wameyauliza na mapendekezo yote ambayo yametolewa katika kamati yetu, lakini vile vile yametolewa na Waheshimiwa Wawakilishi basi yote yatazingatiwa vizuri katika utekelezaji wa sheria hii, na tunaomba sana waheshimiwa ni kwamba tuunge mkono sana hizi juhudi za serikali ambazo tunachukua katika sekta ya elimu.

Sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto nyingi kama ambavyo baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walichangia suala la uhaba wa elimu, tatizo la madawati katika maskuli mengi waheshimiwa wengi wamelisema mpaka wengine tuweke mabusati. Ni kwamba serikali yetu inatambua matatizo kama

haya na ndio maana Mhe. Rais aliunda ile kamati ya madawati, lakini nimefurahi sana kuona Waheshimiwa Wajumbe wanapongeza juhudi za Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli katika kutoa madawati kwa wananchi wa Tanzania.

Katika madawati haya ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wamechangia kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano, na kila Mbunge wa Jimbo amepata madawati 100. Tunashukuru sana juhudi hizi. Katika kuunga mkono basi na sisi Wawakilishi tulitoa kauli ya serikali hapa katika Baraza hili tukufu ni kwamba Mhe. Rais ameunda kamati ya madawati kwa hiyo na sisi Wawakilishi tuone kwamba hili jambo ni letu sote na sisi tuchangie. Tunasifu ya Wabunge lakini ya kwetu sisi bado hatujayatoa, na tulitoa mapendekezo hapa kwamba kwa waheshimiwa tuchangie na sisi milioni tatu na waheshimiwa mlikiri kwamba mtatoa milioni moja kwa kila mmoja wenu. Kwa hiyo, tunaomba sana hili suala nalo tulifanye angalau kabla ya kufika mwezi wa Disemba kila mmoja wetu awe tayari ule mchango wake amekwishautekeleza ili serikali yetu iweze kupambana na suala hili la uhaba wa madawati.

Tunajitahidi sana katika masuala ya kupata watoto wengi, watoto kila wakiwa wengi mahitaji yanazidi kuwa makubwa. Kwa hiyo, tayari kamati ipo Mhe. Rais ameiunda, inaonesha kwamba hili tatizo ni kubwa, kwa hiyo sisi basi Wawakilishi wa wananchi hili suala nasi tuliunge mkono vizuri kama ambavyo wenzetu wa Bunge wao wamelianza.

Tunaomba sana basi kila mmoja wetu kabla ya mwezi wa Disemba tunapokwenda katika sherehe za Mapinduzi basi sote kila mmoja awe na risiti yake tayari ya kuonesha kwamba ameshachangia mchango huo wa madawati, kwa sababu hili ni suala letu sote.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri malizia.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana namalizia sentensi moja.

Waheshimiwa Wajumbe, ni kwamba Taasisi yetu ya Elimu itaweza kufanya kazi zake vizuri zaidi endapo miundombinu ya skuli itakuwa ni imara zaidi, na itakuwa imara pale ambapo sisi sote tutaonesha mashirikiano.

Kwa hiyo, waheshimiwa tunaomba sana mashirikiano yenu ili kuona kwamba sekta ya elimu inafanya kazi vizuri, lakini kuona kwamba taasisi ya elimu inafanya kazi zake vizuri muda ambao baada ya kumaliza kutiwa saini

inasimama vizuri. Waheshimiwa tunaomba sana mtuunge mkono ili sheria hii iweze kupita na Mhe. Rais aweze kuitia saini. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja, sasa niwaulize wanaokubali hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Katika mchango wangu kwenye sehemu hii ya kwanza nilitoa pendekezo juu ya tafsiri ya mtaala, lakini nashangaa kwamba Mhe. Waziri hakuweza kugusa…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hatujafika huko bado.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Hatujafika.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Hatujafika, ahsante.

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika

Kifungu 2 Matumizi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 3 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Katika mchango wangu nilisema suala la neno mitaala ufafanuzi wake ambayo hiyo tafsiri kwa mtizamo haina mtizamo mpana, kwa sababu imeegeshea sana katika mafunzo yaliyoratibiwa katika skuli, wakati neno "mtaala" lina upana zaidi wa hiyo. Kwa hiyo, ningependa Mhe. Waziri alipokee hilo, kwa sababu katika majumuisho yake sikumsikia.

Vile vile nilipendekeza liongezwe neno la ufafanuzi vitabu vya rejea, nalo vile vile sikumsikia na sina hakika katika mapendekezo ya kamati hicho kitu kama kimeingia. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana ushauri wake tumeupokea, na hilo neno vitabu vya rejea litatolewa ufafanuzi wake. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mhe. Waziri hebu tusaidie kwenye hili. Mheshimiwa alichokizungumza ni kwamba alitaka marekebisho sasa watendaji hapa hawajajua ni kipi ambacho kimerekebishwa. Nafikiri kinataka kutolewa kama kilivyo katika hayo marekebisho yake.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante ni kwamba Mhe. Mwakilishi alitaka neno sahihi la mitaala tafsiri yake, yaani kwa tafsiri hiyo kwa hapa haipo vizuri sana, kwa hiyo kutokana na maelezo ambayo ametoa na ushauri wake ni kwamba nimefafanua vizuri zaidi hili neno "mitaala" badala ya hii tafsiri ambayo hapa inasomeka. Lakini neno jengine ni katika neno la "vitabu vya rejea" liwemo katika maneno haya ambayo yanatoa ufafanuzi wa maana za maneno.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mhe. Waziri naomba Mjumbe upendekeze sasa ni vipi unataka tafsiri ya mitaala iwe pamoja na…

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu islahi hii ni ya kitaalamu inahitaji *reference*, mimi nilichodokeza tu ni hicho kwa sababu siwezi kuitoa hapa halafu ikaja ikawa na makosa *otherwise* nipewe muda ili niwasiliane na Mhe. Waziri kuweza…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hilo haliwezekani, kwa sababu hapa tuko katika kupitisha vifungu, tunatunga sheria na sheria tunayoipitisha hapa ndio

itakuwa sheria kamili. Kwa hiyo, kwa upande huo hatuwezi isipokuwa ilikuwa marekebisho yako uyalete yakiwa kamili ili yaingizwe ndani ya sheria hii.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante Mheshimiwa.

UTARATIBU

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako tu ili kumpa uwezo Mhe. Waziri wakati mwengine wa majibu wale watendaji wake wawe karibu ili wamsaidie baadhi ya kazi. Ilikuwa hilo tu Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mara nyingi sana hasa katika kupitishwa miswada watendaji wanakuwa wanabakia juu, isipokuwa ni wakati wa bajeti tu. Lakini hata hivyo nitawaruhusu waje kama kunaonekana kuna umuhimu huo, lakini sidhani kama kuna umuhimu huo, waheshimiwa eeh! Tuwaachie wawepo pale pale, tunaendelea.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, nataka kuzungumza yale yaliyozungumzwa kwamba kwenye Kamati ya Kutunga Sheria, kwa hivyo marekebisho au kama kifungu kilivyo lazima kijulikane hapa.

Sasa Mheshimiwa yeye alitaka kufikiria lakini ukamwambia kwamba hiyo haiwezekani. Sasa kama haiwezekani ina maana tunapitisha kama ilivyokuja sasa hivi, kwa sababu huwezi kusema kwamba mzigo huu unakuja kufikiria ofisini au vipi lazima kamati hii ndio iamue. Kwa hivyo, ina maana tunapitisha kifungu kama kilivyo.

Kifungu 3	Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 4	Kuanzishwa kwa taasisi pamoja na marekebisho yake

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia mswada huu katika Sehemu hii ya Pili nilipendekeza kwamba miongoni mwa kazi za taasisi ambazo ni muhimu sana ni suala zima la kutunza na kuhifadhi vifaa vyote vya kufundishia na kujifunzia, ambapo kitu hiki hakipo. Kwa sababu bila ya taasisi kuwa na kazi hiyo, maana yake inaweza ikabuni, ikachapisha lakini mwisho wa habari ikawa hakuna suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hicho kifungu kinachoelezea kazi za taasisi ni kifungu cha 5.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Samahani, nije hapo katika kifungu cha 4 kuna neno 'kunaanzishwa', ilikuwa lisomeke 'kuanzishwa'. Halafu vile vile itakuwa ni wakala wa serikali. Mapendekezo nilipendekeza kwamba iwe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, hilo neno 'Wakala wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar' tutaliingiza, lakini neno 'kuanzishwa na kunaanzishwa' bado maana yake inafanana. Kwa sababu yote hayo tunasema kwamba katika lugha yote ni nomino, kwa hiyo kwa hapo tunaanzisha taasisi si neno ambalo labda pengine litaharibu maana yake, lakini kama anahisi kwamba labda neno 'kuanzishwa' ndio liko bora zaidi tunaweza kusema kwamba tuliweke lakini hata hili lililokaa hapa bado ile maana yake haijaharibu maana. Kwa sababu yote mawili yana maana ambayo inalingana. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Neno hilo lilikuwa linasomeka 'kunaanzishwa', mimi mapendekezo yangu ni 'kuanzishwa'. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wakati wanachangia wapitie pia ripoti za kamati. Kwa sababu mengi ya mapendekezo ambayo wanayatoa tayari yameshafanyiwa kazi kwenye kamati na Mhe. Waziri wakati anafanya majumuisho amekubali mapendekezo ambayo yametoka kwenye kamati. Sasa neno ambalo Mhe. Rashid Makame Shamsi anapendekeza tayari limeshazungumzwa kwenye kamati na kamati wameshatoa ushauri na Mhe. Waziri amekubali. Mimi nadhani tungefanya hivyo ingetusaidia pia na kuokoa muda.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 4	Kuanzishwa kwa taasisi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5	Kazi za taasisi pamoja na marekebisho yake

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti ahsante. Wakati Mhe. Waziri anafanya majumuisho yake alitaja hoja mbali mbali ambazo nilizungumza katika mjadala, lakini katika sehemu moja ambayo nilizungumza ni katika suala zima la kutambua vipaji kwa vijana wetu.

Sasa Mhe. Waziri sijui amelichukulia kwa upande gani, lakini mimi ninavyoona ni kwamba katika eneo hili, na baada ya kupitia ripoti ya kamati pia sikuliona na nilishauri kwamba katika kazi moja ambazo taasisi itakuwa

nazo ni kuweza kuvitambua na kuvifanyia kazi vipaji vya vijana wetu katika nyanja tofauti. Sasa labda ningepata majibu kidogo halafu tukaendelea.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti ahsante, labda nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba hayo marekebisho anayodhani angependekeza tuyafanye ni katika kipengele gani anapendekeza yakae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeshauri kwamba katika kazi moja ya usimamizi katika eneo la taasisi itakuwa nazo ni kuweza kutambua vijana wetu wenye vipaji katika nyanja tofauti, ili waweze kukuzwa na kuendelezwa katika masuala ya kielimu na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa, hicho kitakuwa kipya au unaweka katika kifungu, unapendekeza kiwe ni kifungu kipya au kiingie ndani ya kifungu kile.

Mhe. Simai Mohammed Said: Kifungu kipya.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa basi ukisome hicho kifungu unachokipendekeza, ukirejee tena kwa kukisoma upya.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningependekeza kifungu kipya kiingizwe na kile kifungu ambacho nilikuwa nimekiandika sikioni hapa, lakini nilikiandika katika mazingira kwamba: Vijana wetu katika kazi ambazo taasisi itakuwanazo moja ni kuzisimamia, kuweza kuwatambua vijana wetu wenye vipaji katika kuwaendeleza katika nyanja tofauti ya kielimu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hicho sio kifungu. Kwa sababu hapo ni kazi za taasisi, sasa hicho sio kifungu, hayo ni maelezo, pengine katika utekelezaji yatakuja mambo hayo, lakini hapa tunatunga sheria huwezi kuandika Mheshimiwa kifungu kama hivyo. Tunaendelea amekubali tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha 5 Sehemu ya Pili katika kazi za taasisi nilipendekeza kwamba kazi hii ya utunzaji na kuhifadhi vifaa vyote vya kufundishia na kujifunzia viwemo kutokana na umuhimu wake. Mhe. Waziri sijamsikia kuweza ku-*respond* na ushauri wangu huo. Naomba ufafanuzi, ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ukitizama kifungu cha 5(s) kuna kazi nyingi ambazo nyengine inawezekana pia ni muhimu za kamati ambazo pia hazikuingizwa.

Sasa ukisoma kifungu cha 5(s) kimetoa fursa pana kwa taasisi hii kuweza kufanya kazi nyengine zozote ambazo zitakuwa ni muhimu katika utekelezaji wa kazi zake. Inawezekana hapa kila mtu akaona ana jambo lake ambalo ni muhimu liingie tukajaza ukurasa mzima, ndio maana kifungu hiki kikawekwa maalum kwa kutoa fursa pana kwa taasisi pale ambapo wanaona kuna mengine ambayo hayakuingizwa na ambayo ni sehemu ya kazi zake basi iweze kufanya kwa kupitia kifungu hiki.

Mawazo yake ni mazuri, lakini pia yanaweza kufanyiwa kazi kwa mujibu wa kifungu hiki Mhe Mwenyekiti. Ahsante.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Mwanasheria Mkuu lakini kuna kazi ambazo tunaziita kazi za msingi na kuna kazi ambazo tunaweza tukasema zina umuhimu mdogo. Suala la utunzaji na uhifadhi kwa sababu taasisi kama taasisi inatakiwa kuweza kubuni, kuandaa na hatimaye kuweza kuchapisha kazi mbali mbali zinazohusiana na ufundishaji na kujifunza. Lakini bila kuwepo kwa kazi hii muhimu ijitokeze hapo, mimi ndipo nilipo. Nakubaliana na mawazo yake ya kifungu cha 5(s) lakini kutokana na umuhimu huo na kasoro ambazo zimejitokeza kwamba taasisi hivi sasa vifaa vyake ambavyo vilitakiwa vihifadhiwe na taasisi vinahifadhiwa na idara nyengine. Kwa hiyo, unatokea upoteaji na wizi wa vifaa hivyo, ndio maana nikaona kwamba kazi hii ingewekwa mkazo iwepo na hicho kifungu cha 5(s) sikikatai kiwepo. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, sisi tumemsikia mawazo yake ambayo ameyatoa lakini na sisi kama ambavyo tumetoa ufafanuzi. Sisi kama serikali na kama wizara ambayo imeleta mswada huu kwa kifungu cha 5(s) kilivyo mimi nadhani kinatosheleza na kinatoa fursa pana ya haya mengine yote kuingia. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

La pili, waziri pia kapewa uwezo wa kutunga kanuni kuna mambo mengine pia yataingia kwenye kanuni ambayo hayakuingizwa kwenye sheria. Sasa hatuna haja ya kuingiza kila jambo kwenye eneo hili, madhali sheria kifungu cha 5(s) kimetoa uwezo mpana zaidi kwa taasisi kuweza kufanya kazi nyengine mbali ya hizi ilizopewa. Sisi mawazo yetu ni kwamba hiki kifungu kama kilivyo kinatosheleza ku-*accommodate* kazi nyengine zozote ambazo taasisi itatakiwa ifanye kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, naomba liendelee kama litakavyoendelea. Ahsante.

Kifungu 5 Kazi za taasisi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 6 Bodi ya ushauri pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti ahsante. Mimi katika kifungu hiki nina ushauri tu. Katika Bodi ya Ushauri miongoni mwa wajumbe imeandikwa ni mwakilishi mmoja kutoka katika Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu. Ushauri wangu ni kwamba hivi sasa kuna jumuiya za watu wenye ulemavu zisizopungua 13. Kwa hiyo, badala ya Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu tuweke Jumuiya za Watu wenye Ulemavu. Kwa maana hiyo, hapa ikiwa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu zile jumuiya zote zina shirikisho lao, kwa hiyo wao wenyewe ndio watampendekeza yule mtu ambaye wanahisi huyu anaweza kutuwakilisha katika hii bodi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, tumepokea hilo pendekezo lake na badala ya kusema jumuiya ya tutasema jumuiya za, au lakini pia kwa taarifa tuliyoipata kwamba kuna Baraza la Watu wenye Ulemavu. Sasa nadhani pengine hilo Baraza ni ambalo linajumuisha jumuiya zote, sasa tutatumia lile neno Baraza nadhani itakuwa muafaka zaidi, Baraza la Watu wenye Ulemavu ili ionekane kwamba hizi jumuiya zote zimo ndani yake. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ningependa pia kusaidia kutoa ufafanuzi kwenye kifungu hiki.

Nadhani dhamira iliyokusudiwa kwenye kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti, ni kuishirikisha ile jumuiya ambayo inabeba taasisi hizi nyengine zote, ndio dhana ambayo ipo hapa. Tunatambua kwamba ziko nyingi, sasa huwezi ukataja moja moja, lakini inawezekana ina jumuiya yao ambayo inabeba hivi vyama vyengine vyote. Kwa hivyo, ndio dhamira iliyowekwa hapa, kama vile ambavyo kuna ANGOZA ambayo inabeba taasisi nyengine kama ambavyo kipo Chama cha Wafanyabiashara na hapa dhamira yake ilikuwa ndio hiyo na sio kuvitaja kimoja kimoja.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii tena. Nakubaliana na Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini sasa kwa ufafanuzi tu Jumuiya za Watu wenye Ulemavu kama nilivyozungumza ziko nyingi na hizi jumuiya zina shirikisho lao. Kwa hiyo, hapa tukiweka Jumuiya za Watu wenye Ulemavu kwa maana hiyo zile zina shirikisho ambalo linaitwa SHIWAZA, wao wataweza kukaa na kumchagua huyo mtu ambaye anaweza kuwawakilisha katika hiyo bodi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mimi nadhani tunazungumza lugha moja hatujafahamiana tu kidogo, lakini nadhani mawazo yake ni mawazo ya kwetu. Sisi tunachosema tulichokikusudia hapa ni hilo ambalo yeye anasema ile jumuiya yao ambayo ipo *Apex Organization* ndio ambayo inatakiwa itoe mwakilishi mmoja.

Sasa katika kutoa wawakilishi hii jumuiya itawasiliana na hizi jumuiya *Individual Organization* ambazo zipo, labda angetusaidia ile jumuiya yao inaitwaje, ili tuijue vizuri. Kama anaona uandishi haujatosheleza ile dhamira ambayo imekusudiwa, lakini dhamira iliyokusudiwa ni hiyo Mhe. Mwenyekiti, na nadhani sisi na yeye tunazungumza lugha moja, ni mahala padogo tu tunahitilafiana katika kuweka lugha hii vizuri. Sasa atusaidie kama anaona tuweke ile jumuiya yao ambayo ndio kusudio letu basi tuweke, lakini dhamira ni hiyo kuishirikisha hiyo jumuiya yao kubwa ili ishirikiane na hizi taasisi moja moja katika kutoa mjumbe mmoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu nilivyomfahamu mimi Mhe. Mwantatu Mbaraka kwamba jumuiya za walemavu ziko nyingi, lakini wao wana *umbrella* moja ambayo inajulikana kama shirikisho. Sasa nafikiri kwamba neno 'shirikisho' ndilo ambalo linatakiwa ku-*appear* hapa kwenye kifungu.

Kwa hiyo, Mjumbe ambaye una hoja hii tunaomba utupe hayo marekebisho ambayo unayazungumzia.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti, tukiweka neno 'shirikisho' itakuwa ni sawa lakini vile vile tukiondoa hii 'ya' baina ya jumuiya na watu hii 'ya' tukaondosha tukaweka 'za' pia itakuwa sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa toa ushauri mmoja.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Tuondoe 'ya' tuweke 'za' iwe jumuiya za, kwa maana hiyo ndio itakuwa lile shirikisho.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nafikiri tunakubaliana bora iwe Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ili tuweke lugha sawa ni kama lipo hilo ambalo tunalizungumza. Kwa sababu kama lipo limeshasajiliwa, linafanya kazi yaani tuandike kitu ambacho kipo, tusije tukaandika kitu halafu

baadae kikaja kutukwaza katika utekelezaji wake, ndio maana tukamuomba Mheshimiwa atusaidie neno sahihi linalotumika ni neno gani. Sisi tunaona kwa hivi ilivyo imekidhi dhamira ambayo imekusudiwa. Inawezekana tumekosea mawazo haya yanayotoka tuweke sawa, lakini tuweke kitu ambacho tutapoanza kuteua hao wajumbe tusije tukakwazika tukasema kumbe taasisi hii haipo haijasajiliwa. Ndicho tunachozungumza Mhe. Mwenyekiti. Lakini mawazo ni mazuri na sisi ukituuliza nadhani tumechukua ile dhamira pana ambayo imekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwantatu Mbaraka naomba utusaidie tuimalize hii hoja. Mhe. Mwanasheria Mkuu ana hofu kwamba shirikisho inawezekana halipo lakini tupe neno ambalo litakuwa sahihi na hayo ambayo unayajengea hoja.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimthibitishie Mwanasheria Mkuu kwamba hili shirikisho lipo na tayari limeshasajiliwa. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilitoa ushauri kuhusu *composition* ya bodi na katika maeneo mawili ambayo niliyataja moja ni tayari Mhe. Waziri amelijibu, ni kupata mwakilishi awe mkurugenzi kutoka *Diaspora* na nimeridhika na maelezo yake.

Jengine nilizungumza katika *spirit* ambayo nchi yetu tunakwenda na hasa katika shabaha na dhamira ambayo imetajwa, nikashauri tupate mwakilishi mmoja kutoka sekta binafsi kama ni kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wakulima na Wavuvi au katika sekta binafsi katika Jumuiya ya Wawekezaji katika Sekta ya Utalii au wasafirishaji. Lakini uwakilishi wa sekta binafsi ni vizuri ukawepo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mwakilishi kutoka sekta binafsi yupo, mwakilishi kutoka skuli za binafsi. Kwa muktadha huu wa skuli tunadhani mwakilishi kutoka skuli ni muafaka zaidi kuliko kumtoa *Chamber of Commerce* au sehemu nyengine.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimhakikishie tu kwamba wakati naangalia hilo niliangalia suala la kwenye elimu kwamba yupo mwakilishi katika maeneo ya skuli. Lakini nilichokizungumza kutoka sekta binafsi ambapo ni watu ambao tayari hawa vijana wetu wanapomaliza elimu yao wao ndio wanakwenda kuwaajiri nje huko na kuweza kutoa ushauri katika

mitaala ya mambo mengi, ambayo katika hizo ajira zinakuwepo. Sasa ikiwa Mhe. Waziri anaona uwakilishi huu unatosheleza mimi kwangu ni sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Ina maana kwa hiyo tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti narudia tena. Jukumu la Mwakilishi ni kushauri serikali, kazi yangu hapa ilikuwa ni kushauri ikiwa Mhe. Waziri ameridhika na kwamba anaamini kwamba uwakilishi huo kutoka sekta binafsi unatosheleza kwa maskuli basi tuendelee.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia katika bodi hii ya ushauri nilishauri kwamba katika Jumuiya ambayo inashughulika na masuala ya elimu ZATU ikashauri kwamba hawa waingizwe, lakini Mhe. Waziri wakati ananijibu alisema kwamba kuna shirikisho au chama cha Wafanyakazi kwamba ndio ambao kwa kweli hapa wameweza kuwakilisha katika sekta zote hizi. Lakini nilikuwa naona kwamba bado umuhimu upo kwa sababu hawa ZATU ni jumuiya inayoshughulika na masuala ya elimu moja kwa moja, na hawa pia nadhani kwa vile taasisi hii ndio ambayo itakuwa ni tegemeo letu ambalo tutakuwa tunaiangalia katika ufanisi.

Mimi nadhani kwa ushauri wangu ningeomba kwamba iko haja sana, kwa sababu Chama cha Wafanyakazi kinaingia katika *broad* kabisa, lakini hawa wao wana-*specialize* katika suala moja tu, suala la sekta hii ya elimu.

Kwa hiyo, bado namuomba Mhe. Waziri kwamba nibakie na hoja yangu kwamba tuone kwamba uko umuhimu wa kuingiza hawa moja kwa moja ili kuona kwamba tunaweza tukafika wakatushauri mambo ambayo yanaweza yakasaidia zaidi, kwa sababu wao ndio jambo ambalo kwa kweli wanalisimamia *direct*. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ningependa kurekebisha kwamba hiyo ni jumuiya ya waajiri sio jumuiya ya wafanyakazi, jumuiya ya waajiri na kwa maana hiyo sasa umuhimu sasa ndio ile hoja aliyosema Mhe. Simai Mohammed Said, ule umuhimu wa kuwepo Uwakilishi katika Bodi ya Ushauri ya Mitaala, Wawakilishi ambao watakuwa wanahusiana na masuala ya ajira na wataweza kutoa mchango wenye maana zaidi katika hali ya soko ya ajira itakavyokuwa tunahisi ni muhimu zaidi kuliko Chama cha Walimu ambao mchango wao utakuwa zaidi labda katika maslahi ya walimu.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyo taratibu kwamba Mwakilishi anatakiwa aishauri serikali, na mimi kwa vile nimeshashauri na bado sababu zimetolewa kwamba zina msingi na mimi moja kwa moja nimuombe Mhe. Waziri tuendelee. (*Makofi*)

Kifungu 6	Bodi ya Ushauri pamoja na marekebisho yake
Kifungu 7	Sifa za Mwenyekiti pamoja na marekebisho yake
Kifungu 8	Kazi za Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9	Mwenendo wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10	Uteuzi wa Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, hili neno mimi linanipa wasi wasi hili neno kila tunapolitamka kwenye miswada yetu inakuwa neno "kutakuwa" sisi ni waswahili, sote Kiswahili tunakifahamu. Unaposema neno kutakuwa hivi sasa kwa sababu halijakuwa ndio litakuwa. Lakini likishakuwa ina maana lile neno litakuwa halipo.

Sasa ni vyema ikatafutwa lugha nzuri ikatumika kwenye vipengele vyetu vya sheria, kwa sababu hata huo Mswada wa Sheria na Mafuta na Gesi umejaa haya maneno "kutakuwa" ina maana ukishapita ile neno kutakuwa halipo tena.

Kwa maana hiyo mimi napendekeza kwamba hilo neno "kutakuwa" liondoke liwepo "Itakuwepo au ipo", kwa sababu tukishapitisha hiyo Tume itakuwepo tayari, hiyo bodi itakuwepo. Sasa ukisema "itakuwa" wakati umeshapitisha mswada mpaka ije tena baada, ninavyofahamu mimi Kiswahili. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hili neno kutakuwa wewe mwenyewe umesema lugha ya sheria. Sasa kwa kuwa ni lugha ya sheria haiwezi hapa kubadilika Mheshimiwa. Kwa sababu lugha nyengine inabidi uikubali kutokana na ile fani yenyewe Mheshimiwa. Kwa hiyo, tuachie tuendelee, kwa hilo sidhani kwamba kama kuna yeyote ambaye atakubali hapa.

Kifungu 10	Uteuzi wa Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11	Kazi za Mkurugenzi
Kifungu 12	Kamati pamoja na marekebisho yake
Kifungu 13	Kazi za Kamati pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14	Uwezo wa waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tuwe na *discipline*, naomba sana, hatuwezi kusema ndio kabla ya kifungu hakijaulizwa. Kwa hiyo naomba mnipe nafasi niulize halafu ndio mseme ndio, sawa.

Kifungu 15	Fedha na rasilimali pamoja na marekebisho yake
Kifungu 16	Kutumika kwa sheria ya fedha pamoja na marekebisho yake
Kifungu 17	Uwezo wa kutunga Kanuni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 18	Vifaa vya kufundishia pamoja na marekebisho yake
Kifungu 19	Wafanyakazi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20	Kuhaulishwa mali na madeni pamoja na marekebisho yake

(*Baraza lilirudia*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja, wale ambao wanakubali wanyooshe mkono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria wa Taasisi ya Elimu Zanzibar
wa mwaka 2016

(*kusomwa kwa mara ya tatu)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu Zanzibar ya mwaka 2016 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja wale ambao wanakubali wanyooshe mkono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Muswada wa Sheria ya Serikali umepitisha rasmi na Baraza)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana kwa kuupitisha mswada huu. Vile vile nimpongeze Waziri wa Elimu pamoja na timu yake yote pamoja na kamati ambayo kwa kweli imefanya kazi vizuri sana, ni matarajio yetu kwamba mswada huu utasaidia katika kuleta maendeleo ya taifa letu.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda wetu wa kumaliza shughuli zetu za leo haujafika ninashauriwa niakhirishe tu, lakini nilikuwa nataka kumpa Mkuu wa Kiongozi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aweze kuakhirisha. Kwa hiyo, nachukuwa fursa hii adhimu kuahirisha sasa kikao hichi hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:12 usiku Baraza liliahirishwa mpaka
tarehe 22/09/2016 saa 3:00 asubuhi)